ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 05 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2012/2013 naomba kuwasilisha.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

NAM. 18

Ukiukwaji wa Sheria ya Mazingira katika baadhi ya Miradi ya Maendeleo

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Aliuliza:-

Baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa hoteli na barabara hukiuka Sheria ya Mazingira kwa kuharibu mazingira, na baada ya uharibifu huo Idara ya Mazingira hutakiwa kufanya tathmini ya Mazingira ili kubaini uharibifu huo, na ikibaini uharibifu huo hutakiwa kwa mujibu wa Sheria kudai 1% ya fidia.

(a) Je, ni miradi mingapi ya barabara na hoteli, kuanzia mwaka 2000 hadi sasa iliyokiuka Sheria hiyo.

(b) Ni sababu zipi zinazopelekea miradi hiyo kutekelezwa kwa kuharibu mazingira wakati Sheria na taratibu zinawataka Wawekezaji hao kutekeleza miradi yao bila ya kuharibu mazingira.

(c) Je, Serikali kupitia Idara ya Mazingira kuanzia muda huo hadi sasa imekusanya shilingi ngapi kama ni mapato yaliyotokana na fidia iliyotokana na uharibifu huo wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Alijibu:-

Mhe.Naibu Spika, kwa ruhusa yako, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 18 naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Naomba nikiri kwamba bado kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa hoteli na barabara hukiuka Sheria ya Mazingira kwa kuharibu Mazingira. Sehemu ya tano ya Sheria ya Mazingira inaeleza mambo yanayohusu Tathmini za Athari za kimazingira. Hata hivyo kwa bahati mbaya sheria hiyo haikuweka madai ya fidia ya 1% isipokuwa katika sheria hiyo kuna kifungu cha kuanzishwa kwa Mfuko wa Tahadhari wa Mazingira yaani "environmental *performance bond"* na katika kanuni ya mwaka 2002 ya Mfuko wa Tahadhari imeelezwa kuwa dhamana ya mfuko huo itakuwa ni asilimia 10%.

Aidha Sheria hiyo pia imeambatanishwa na Jaduweli mbali mbali, Jaduweli namba 1 na 2 zinahusika na mambo ya Tathmini za Athari za Kimazingira. Jaduweli namba 1 inazungumzia shughuli ambazo moja kwa moja hazihitaji Cheti cha Mazingira. Na jaduweli namba 2 imetaja shughuli ambazo moja kwa moja zinahitaji cheti cha mazingira. Aidha miradi ya hoteli iliyotajwa kwenye jaduweli namba 2 ambayo inahitaji cheti cha mazingira ni miradi ya hoteli yenye vitanda 100 na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 18 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Kuanzia mwaka 2000 hadi sasa jumla ya miradi 231 ya hoteli imeanzishwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa miradi ya barabara Afisi yangu kupitia Idara ya Mazingira imekosa kupata takwimu za kutokea mwaka 2000 kwa miradi yote iliyoanzishwa. Hii inatokana na ukweli kwamba kwa miaka iliyopita miradi mingi ya barabara ilikuwa haizingatii sheria ya mazingira. Lakini napenda niainishe kwamba, kwa miaka hii ya karibuni baada ya kuielimisha, na Idara na Wizara ya Mawasiliano kwa ujumla tumeweza kusimamia jumla ya miradi 18 ya barabara imefanyiwa Tathmini ya Athari za Kimazingira kwa mujibu wa sheria ya Mazingira. Aidha kati ya miradi ya 231 ya hoteli ni miradi 25 tu ndio ilipaswa kufanyia Tathmini ya Kimazingira kwa kuwa ndiyo iliyoanza ikiwa na jumla ya vitanda 100 au zaidi ya hapo, ambapo miradi yote 25 ilifanyiwa tathmini za athari za kimazingira kwa mujibu wa sheria.

b) Miongoni mwa sababu zilizopelekea miradi hiyo kutekelezwa kwa kuharibu mazingira ni pamoja na:-

Upungufu wa kisheria uliopo kwenye Sheria ya Kimazingira. Jaduweli namba 4 Sheria ya Mazingira inaeleza faini mbalimbali, kwa bahati mbaya faini za Tathmini za Athari za Kimazingira, au kwa yule ambaye atakiuka Amri za Zuio (*Stop orders*) hazimo kwenye jaduweli hiyo.

- Mwamko mdogo wa wawekezaji juu ya umuhimu wa kuhusisha masuala ya Mazingira kwenye miradi ya maendeleo.

- Mara nyingi miradi ya barabara inakuja kama ni misaada, kwa hivyo inakuwa ni vigumu mara nyingi masuala ya mazingira kuzingatiwa kwa ukamilifu wake hasa katika suala zima la kupata asilimia 10.

- Mashirikiano madogo miongoni mwa Taasisi zinazohusika na Uwekezaji na Miundombinu.

- Pia upungufu wa nyenzo za kufanyia ukaguzi wa kasi na mfumo stahiki kwa miradi ya maendeleo.

c) Idara ya Mazingira haikusanyi mapato yake kutokana na fidia za uharibifu wa mazingira, bali Idara hukusanya mapato ya Serikali kutokana na mchakato wa Tathmini za Athari za Kimazingira. Kila mwaka Idara huwa inakusanya kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa kama yalivyopitishwa na baraza lao hili tukufu, kwa mfano kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni mwaka huu wa 2011/2012, Idara ya Mazingira ilipangiwa kukusanya jumla TZ shilingi 5,000,000 kutokana na makusanyo ya usajili wa miradi pamoja na utoaji wa vyeti vya kimazingira, na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2012, Idara imeweza kukusanya jumla ya TZ shilingi 5,970,000 sawa na asilimia 120% kwa maana ya kuvuka lengo la makusanyo kwa asilimia zaidi ya 20%.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa miradi ya hoteli na barabara ni miongoni mwa miradi yetu ya maendeleo na kukuza uchumi wetu. Lakini pia kwa kuwa miradi hii mara nyengine inasababisha uharibifu wa mazingira kutuletea matatizo katika nchi yetu. Je, Ofisi yake ina mpango gani kabambe kwa kushirikiana na taasisi nyengine ili kuhakikisha kwamba miradi hii inakuwepo lakini na mazingira hayachafuliwi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba changamoto hiyo ipo kama nilivyokiri katika kujibu swali mama, na hivi sasa Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais inajipanga katika njia mbili kuu.

Ya kwanza tumegundua kuwa kuna mapungufu katika Sera, lakini pia katika sheria ya mazingira. Ambayo sera ya mwaka 1992 miaka 20 imepita lakini sheria nayo ni ya mwaka 1926 kwa hivi sasa tunavifanyia marekebisho ili

ziendane na wakati, lakini pia kuweza kuingiza vipengele vya kuwalipisha faini au kifungo wale wote watakaokiuka kanuni zilizowekwa kwa ajili ya kuzingatia utunzaji wa mazingara.

Lakini pili, ofisi yangu inafanya jitihada zote kuwasiliana na taasisi mbali mbali zinazohusika, taasisi ya uwekezaji ambayo ndiyo inayosimamia miradi ya hoteli. Lakini vile vile Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu kuhakikisha kwamba pale inapoendelezwa miradi ya hoteli au barabara basi panarejeshwa katika hali yake ya uwasili, kwa kutumia nyenzo tulizonazo sisi wenyewe na *resources* ambazo zimo ndani ya Serikali yetu.

Nam. 158

Kuvirejesha Vyoo Mikononi mwa Serikali

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Pamoja na ahadi ya muda mrefu ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa mara kadhaa katika Baraza la Wawakilishi ya kuchukua hatua ya kurejesha vyoo vilivyokuwa vikimilikiwa na Serikali kupitia Baraza la Manispaa katika maeneo ya Mji Mkongwe, na ambavyo vimemilikishwa kwa watu binafsi na kutumiwa kwa shughuli za kibiashara, bado hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Ni lini Waziri atasimamia utekelezaji wa ahadi zake anazozitoa kwenye Baraza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake nambari 158 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimjulishe Mhe. Mwakilishi kwamba Mji Mkongwe kuna jumla ya vyoo 9. Katika vyo hivyo si vyote viliopo chini ya uangalizi au mkataba wa Baraza la Manispaa kwa asilimia mia moja. Kuna vyengine haviko moja kwa moja chini ya Baraza la Manispaa.

Tatu naomba nimjulishe kwamba hivi vyoo vimekodishwa kwa mikataba, hivyo si rahisi kuvunja ile mikataba moja kwa moja lazima tuwasiliane ne aliyekodishwa na havikumilikishwa kama alivyosema kwenye swali lake vimekodishwa kwa mikataba. Sasa kuivunja lazima tuende katika taratibu ili kuepuka kwenda mahakamani. Lakini hata hivyo wako waliokwenda mahakamani. Sasa naomba kwa kifupi upesi upesi nikichambue kimoja baada ya chengine.

Kwanza choo cha Forodhani, choo hiki kipo chini ya bodi ya *Forodhani Park*, hakipo chini ya Manispaa kimkataba.

Pili, choo cha *Africa House*, choo hiki kipo chini ya Manispaa na yule aliyekodi mwanzo alishindwa kwa sababu ya kutoweza kufuata masharti yeye alitaka atoe huduma peke yake bila ya kuweka choo, tukakataa ndio ikawa muda mrefu kile kimefungwa. Lakini baadae tumepata mkodishaji mpya kakitengeneza na mimi nimekwenda kukagua kuna vyoo vitatu pale. Lakini pia utaona masanduku ya soda yapo kwa sababu ile biashara ya choo peke yake haikhalisi. Kwa hivyo tutaendelea na mkataba naye tukubaliane.

Choo cha *Majestik* ndio vile nilivyovisema, choo hiki kina matatizo sasa hivi takriban miaka 4 tokea Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Mabrouk Jabu, huyu bibi aliyekodi pale kakataa kufuata hayo masharti kenda mahakamani. Kwa hivyo bado kesi iko mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, choo cha Kinazini na Choo cha Darajani hivi vimekodishwa kwa mkataba na Ndugu Sultan Khelef anaendelea vizuri na mkataba wake.

Choo cha mabuluu hiki kipo chini ya Zawa kama nilivyosema hakiko chini ya Manispaa moja kwa moja.

Choo cha samaki Malindi Zayadesa kipo chini Manispaa kinakwenda vizuri, na choo cha Malindi madagaa nacho kinaendelea vizuri.

Na choo cha mwisho choo cha wafanyakazi Malindi nacho hakina matatizo kinaendelea vizuri. Tatizo lazima tufanye hivyo kwa sababu hali yetu ya kuviendesha vyoo, tumeweka pale mkataba aendeshe choo na biashara ndogo ndogo kusaidia *income generating activities* kukiendesha kile choo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, ninamkushukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi alioutoa. Naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba hafatilii kazi zilizokuwa chini ya Wizara yake, ndio maana mpaka leo anaamini kwamba choo kilichopo *Africa House* bado kina sehemu ya kuuzia soda wakati tayari kimefungwa baada ya aliyepewa kushindwa kazi, na hivi sasa hakitoi huduma ya choo wala huduma ya biashara?

(b) Nilikuwa naomba anisaidie kwamba ikiwa Baraza la Manispaa linashindwa hata kuendesha vyoo tisa katika mji haoni kwamba litakuwa limeshindwa kazi, kiasi ya kutoa kazi muhimu ya huduma hii kwa watu binafsi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, mimi nashangaa Mwakilishi wa Mji Mkongwe mji mdogo tu kwamba yeye ndio haujui mji wake. Mhe. Naibu Spika, choo cha *Africa House* tuliyemkodisha zamani nimesema kashindwa, kilifungwa zaidi ya miaka 2 kavunja mkataba kakirejesha. Sasa sasa hivi kama umepita mimi naomba tutoke mimi na wewe twende tukatizame, choo kimetengenezwa upya ndani mna vyoo vitatu kaweka na makontena ya kuuza soda. Mimi naomba Mhe. Naibu Spika, tutoke mimi na wewe twende *physical* tukitoka tu hapa nani mkweli yeye Mwakilishi au mimi tutamjua nani mkweli.

Mhe. Naibu Spika: Mimi ninashauri Mhe. Mwakilishi na Waziri mkimaliza mwende.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, swali langu la (b) halijajibiwa katika kuhamaki kwenye swali (a) kalisahau la (b).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Naomba alirejee kidogo samahani sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshauri Mhe. Waziri naye ainamie, mambo yaliyokuwa chini ya Wizara yake ili apate kuyajua vizuri kama choo cha *Africa House* akijua kwamba hakifanyi kazi. Lakini nakubali ushauri wako kwamba tutakwenda mimi na yeye akathibitishe kama hakifanyi kazi.

Swali (b) nilimuuliza kwamba kwa Baraza la Manispaa kushindwa kuhudumia vyoo 9 viliopo katika maeneo ya mji mpaka kufikia hatua ya kutaka kuvikodisha kwa watu binafsi waviendeshe, haoni kama Baraza la Manispaa litakuwa limeshindwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ninafikiri utakubaliana na mimi Mhe. Jussa hali ya vyoo vyetu vya *public* vinavyoendeshwa, kwa kweli unapotaka kwenda kujisaidia mwenyewe utaona tabu kwa sababu ya ile hali vile vyoo sisemi lakini ule mwenendo wetu sote tunajua. Sasa tumeonekana kwamba kuviweka ndani ya mikono yetu ya Serikali si jambo jema, bora tumuache mtu akikodi tunalipa kidogo na hiyo si Zanzibar tu *Internationally*. Wewe nenda London, nenda Paris, nenda Dar es Salaam, nenda Nairobi ndio ilivyo, unalipa pesa kidogo pale *pocket money* tu ile inasaidia na *discipline* ya vile vyoo. Na sisi twende kwa wakati kidogo ndio kimataifa hivyo, tubadilike Mhe. Jussa.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nilikuwa nataka kujua utaratibu uliotumika katika kukodisha vyoo hivi, muda wa mkataba, fedha zinazopatikana katika mikataba ile, na ni nani aliyekodishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, namuomba hiyo mikataba sinayo hapa lakini kwanza mikataba imeitishwa, tena watu wame-*apply* kwenye tenda ndio wakakodishwa kwa utaratibu. Bei zake zipo na mikataka ipo namuomba Mhe. Mtando kama Mjumbe wa PAC namkaribisha anaweza kwenda kuiona hiyo mikataba.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, hakuwa amejibu yale ambayo nimemuuliza anasema nikaione mikataba, mimi mikataba sawa kuiona nilikuwa nataka kujua ule utaratibu uliotumika, anasema tenda zimeitishwa nakubaliana nae kama tenda tutaenda kuona. Lakini nataka kujua ile *amount* ambayo inakusanywa katika ukodishaji ule hakuwa amenijibu, na nani ambaye amekodishwa hilo nilikuwa nataka kujua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Choo kile nilichosema cha *Africa House* amekodishwa bwana mmoja anaitwa Norman Baloo kwa Laki moja na hamsini kwa mwezi, na huyu ndio kwanza tunaendelea na mkataba nae na choo cha Majestic yuko bibi mmoja anaitwa Firdaus yeye kashindwa mkataba kesi iko mahakamani. Choo cha Forodhani kama nilivyosema kile wapo watu watatu pale, yaani haiko chini ya mamlaka ya Manispaa moja kwa moja. Kuna *Aghakhan*, *Stone Town Conservation* na Manispaa. Lakini choo cha Kinazini na choo cha Darajani anaendelea na mkataba kakodishwa kwa shilingi laki nne kwa mwezi vyoo viwili vile. Choo cha Mabluu kama nilivyosema kiko chini ya Zawa, na vyoo vya Malindi Zayadesa na choo cha Malindi madagaa hivi kakodishwa Ndugu Mohammed kwa laki moja na hamsini elfu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Bado Mhe. Waziri hajanipa umri wa mikataba yaani ukomo wake ile mikataba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mwaka mmoja.

Nam. 166

Kuchimba kokoto na kuchonga matofali Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aliuliza:-

Wananchi katika Majimbo ya Kiwani, Tumbe na Micheweni wamekuwa wakiishi kwa muda mrefu kwa kutegemea kazi ya kuchimba kokoto na kuchonga matofali.

a) Je, kwa nini Serikali imeamua kupiga kazi yao marufuku kabla ya kuwatafutia kazi mbadala.
b) Kwa kuwa wananchi walikuwa wakiishi kwa kazi hiyo na familia zao. Serikali ina mpango gani wa kuwapatia taaluma na mitaji ili waweze kufanya kazi ambazo haziharibu mazingira.
c) Je, Serikali ilifanya utafiti gani kabla ya kuzuia kazi hizo na watu wangapi wanaathirika.
d) Kwa kuwa Serikali inatoa mkopo kupitia mifuko ya kusaidia wajasiri amali. Je, wachimba kokoto na matofali wangapi wamenufaika kupitia mikopo hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kabla ya sijajibu swali hili naomba kwa ruhusa yako nieleze jambo ambalo limekuwa likisambazwa katika jamii, na mimi nikiwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Naomba nitumie nafasi hii hasa kwa vile taarifa hizo ziko tayari hapa Barazani baadhi yake. Kwa hivyo naomba ruhusa yako uniruhusu nieleze kwa muhtasari japo kwa dakika moja.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tuko katika mchakato wa kutoa maoni ya Katiba mpya ambayo hivi sasa kazi yake imeshaanza. Kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza watu wachache wanasambaza taarifa zinamgusa Mjumbe wako wa Baraza la Wawakilishi ambaye ni mimi hapa niliyesimama mbele yako, kushtumu kwamba nimekuwa nikishiriki kuandikisha barua katika Jimbo la Makunduchi, na si hivyo tu kutoa pesa shilingi elfu kumi kwa kila anaekwenda kutoa taarifa hizo huko jimboni. Mhe. Naibu Spika, nimesimama hapa kulaani vitendo hivyo na naomba waache mara moja kwa sababu wanaharibu taswira ya nchi yetu. Mimi naelewa Wazanzibari wanataka nini, najua umuhimu wa masuala haya yanayoendelea na naomba sana basi suala hilo lisiendelee, na si tabia nzuri imeenezwa kwenye mitandao hata baadhi ya Wajumbe wako humu ndani wameletewa mitandao hiyo kwa kutumia *meseji* maalum. Naomba niishie hapo nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na mimi angalau nitapata pumzi kidogo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 166 lenye vifungu a, b, c na d kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipiga marufuku uharibifu wa mazingira, na ndio maana Serikali hii ya awamu ya saba katika Wizara ambayo inasimamiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeanzisha Idara Maalum inayohusiana na suala la mazingira. Kwa hivyo haikupiga marufuku kwa sababu ya kupiga marufuku kwa sababu wananchi wetu wapate matatizo isipokuwa ni kwa ajili ya kuhifadhi mazingira yetu.

Mhe. Naibu Spika, juhudi kadhaa zimechukuliwa kwa upande wa Wizara yangu ikiwa ni pamoja na kuzungumza na CRDB kutoa mafunzo na kuwawezesha katika maeneo mbali mbalil ikiwemo masuala ya mwani, kilimo na masuala yanayohusiana na hayo. Tutaendelea kutoa mafunzo hadi pale ambapo tutahisi wananchi wetu wameelewa kwamba wasiendelee kuleta uharibifu wa mazingira. Lakini pia hivi sasa tayari tumeshaandaa utaratibu maalum Mhe. Naibu Spika, ili kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa wanaotumia maeneo hayo ambayo wanavunja kokoto, wanapiga matofali lisiendelee tena kwa kuwapa utaratihu wa kupata mikopo.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kwa bahati mbaya sana vijana hawa ambao wanatoa mikopo hawajaweza kuleta maombi yao pale Wizarani kwangu wa kuwapatia mkopo. Utafiti hatujafanya juu ya suala hilo, na *Inshaallah* Mungu akipenda siku si nyingi tutafanya utafiti huo lakini athari zake zinajulikana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa kuwa Serikali inahamasisha wananchi kujiajiri ili kuondokana na umaskini, hatua za kuzuia wananchi hao kabla ya kuwapatia kazi mbadala inasaidia vipi kufanikisha mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa wananchi wake.

(b) Serikali hii ilikuwa ikipiga marufuku, lakini Serikali hii inatoa vibali kuchimba. Na hivi sasa utakuwa tayari kwenda Pemba Vitongoji kunako sehemu inayoitwa Makaani, kwenda kuona mashimo yaliyochimbwa na Wizara ya Miundombinu na kutoka maji ya chumvi. Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu aliahidi hapa hapa kuwa tayari kwenda na mpaka sasa hivi hajawa tayari kwenda kuhakikisha hiyo. Je, *mkuki kwa nguruwe tu kwa binaadamu unauma.*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:
Mhe. Naibu Spika, naomba sana vijana hawa ambao wanafanya kazi hii na mimi nitawaelekeza vijana wangu wanaohusiana na masuala haya ya vyama vya ushirika wende watoe taaluma. Na mimi niwaahidi kabisa Serikali itawapatia mkopo kufanya kazi mbadala sio hii ya kuharibu mazingira.

Suala la kufanya ziara kwenda kutembelea maeneo yale sisi kama mawaziri tunaweza kufanya kazi hiyo, lakini ombi hili alipeleke Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa sababu yeye ndie mdhamini wa shughuli alizopewa za mambo ya mazingira. Niko tayari kushirikiana naye Mhe. Fatma lakini pia Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa niaba ya maeneo aliyoyauliza Kiwani, Tumbe na maeneo mengine nitashirikiana naye. Tunaweza kwenda huko tukafanya ziara maalum sawa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri Wizara yake ni Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, na kwa kuwa Jimbo langu la Micheweni ni Jimbo ambalo mara kwa mara linakuwa ni Jimbo kame, na mara kwa mara huhitaji watu wao kupata misaada na kusaidiwa. Na kwa kuwa Wizara yake sasa hivi imejipiga kifua kuwasaidia wananchi kuwainua kiuchumi. Je, Serikali kupitia Wizara yake imejipanga vipi kuwasaidia wananchi wa Micheweni kitu ambacho kitakuwa ni endelevu cha kuwasaidia ili kuepukana na mambo haya ya ukame mara kwa mara.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Subeit ninamuahidi mwache aorodheshe mahitaji ya wananchi wa Micheweni, kwa sababu yeye ni Mwakilishi pale aniletee halafu nitajua utaratibu wa kufuata.

Nam. 172

Upatikanaji wa Huduma Muhimu

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Wizara ya Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati kupitia Idara ya Ardhi na Usajili imekuwa na mpango wa kuwapimia viwanja wananchi katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Hata hivyo wananchi walio wengi huchelewa kujenga maeneo hayo kutokana na ukosefu wa huduma muhimu zinazoharakisha ujenzi.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasogezea (miundombinu muhimu inayojumuisha maji, umeme na barabara) wananchi hao katika maeneo mnayowapimia kwa mfano Tunguu kwa Unguja na Mfikiwa kwa Pemba ili kuweza kuwaondoshea usumbufu huo na kujenga kwa urahisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 172 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Taasisi zake za *ZECO*, Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) ambazo ziko chini ya wizara yangu na *UUB* ambayo iko chini ya Miundombinbu na Mawasiliano zina wajibu wa kuwasambazia huduma ya umeme, maji safi na salama na ujenzi wa barabara wananchi wake wote wa Unguja na Pemba na huduma hiyo iko katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, ni weli kwamba serikali imekuwa ikitoa viwanja maeneo mbali mbali bila ya kuwepo kwa huduma hiyo kama vile maji, umeme na barabara jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu na tatizo katika maeneo hayo.
Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kuliona hilo imejiandaa na kushughulikia suala hilo kwa kila sehemu ambayo itatoa viwanja basi itatanguliza kupeleka huduma hizo kwanza.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kumekuwa na migogoro mingi ya wananchi hasa kwa wale ambao wanatangulia kujenga katika maeneo ya viwanja wanayopewa, pengine ni kwa makusudi au kwa kutokujua huwa wanaingia katika viwanja vya wenzao. Je, wizara ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi hao juu ya utumiaji wa ramani ili waweze kuepusha migogoro ambayo inatokea na ambayo si ya lazima.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, nafikiri suala hili nimejibu juzi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar italisimamia ipasavyo suala la kuondoa migogoro ya ardhi hususan maeneo ambayo wamepewa wananchi na yale ambayo wamepewa wawekezaji. Kwa hivyo, serikali iko makini juu ya suala hili na tutajitahidi kulishughulikia.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake ameonesha nia ya kusogeza miundombinu katika maeneo ambayo watu wamegawiwa viwanja na wamo katika shughuli za kujenga. Sasa naomba nimuulize kwa mfano kule Tunguu ambako sasa hivi watu wana *speed* ya kujenga lakini tatizo kubwa linalosumbua ni maji, umeme na barabara, anaweza kutwambia kajipangia ni muda gani ataweza kusogeza zile huduma kule ili watu waweze kupata unafuu wa kujenga.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, kupitia Shirika la Umeme lengo na madhumuni ni kusambaza maji katika vijiji ambavyo havijafikia huduma hiyo na lengo ni kusambaza huduma ya umeme katika vijiji ambavyo havijafikia huduma hiyo. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi nakuomba stahamili na huduma hizo zitafika pale hali ya fedha itakaporuhusu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba kuongezea jibu la nyongeza baada ya majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri wangu. Suala la kufikisha huduma za barabara, maji, umeme katika maeneo mapya ambayo wananchi wamekatiwa viwanja wanajenga ni suala ambalo hatutaweza kumpa tarehe hasa kwamba ni lini litafika kwa sababu ni suala la mashirikiano baina ya wizara inayohusika na njia na wizara yangu

inayohusika na maji tukae pamoja na tuanzishe mpango huu kwamba, tunapokata viwanja basi tuweke miundombinu kabisa ili kuwarahisishia wananchi wetu kujenga. Ni suala ambalo tunaendelea nalo na mazungumzo hivi sasa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, wizara katika kuwahudumia wananchi pia iligawa viwanja kwa wananchi katika eneo la Matemwe na kama sikosei wewe mwenyewe ikiwa ni mmoja waliopatiwa viwanja hivyo. Lakini la kusikitisha mpaka leo vile viwanja baada ya kutolewa zile nyaraka wenyewe hawakuoneshwa tuseme ni kwa sababu kuwa kule Matemwe wizara inajipanga kupeleka hiyo miundombinu hasa mwanzo ndio watu wapewe au kuna sababu gani zilizosababisha mpaka leo kuwa hawajapewa viwanja vile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara yangu imepima viwanja katika maeneo ya Matemwe na tayari ilikuwa inataka kuwakabidhi wale watu ambao wanataka kukabidhiwa. Lakini kutokana na tatizo lililojitokeza la wananchi wa kijiji cha Matemwe kuzusha fujo na vurugu serikali imesimamisha kwanza na suala hili serikali inalifuatilia na baada ya kuondoa migogoro hii basi wananchi hao watakabidhiwa maeneo yao kama vile walivyoahidiwa na wizara yangu.

Nam. 99

Bodi ya Usafiri wa Barabara

Mhe. Salma Mussa Bilali (Kny: Mhe. .Shadya Moh'd Suleiman) - Aliuliza:-

Bodi ya usafiri wa barabara ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 na Sheria ya usalama barabarani. Chombo hiki kinatakiwa kukutana kila baada ya miezi mitatu ili kutatua changamoto zinazoikabili lakini pia kufanya tathmini ya hatua zilizofikiwa katika kukabiliana na changamoto hizo.

Je, Mhe. Waziri ni mafanikio gani yaliyopatikana kupitia Bodi hiyo katika suala zima la usafiri wa barabara kwa mwaka 2011-2012.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 99 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Bodi ya Usafiri Barabarani ni chombo cha kisheria kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Barabarani Nambari 7 ya mwaka 2003 kikiwa na jukumu la kumshauri waziri kwa mambo mbali mbali yanayohusiana na usafiri na usalama wa barabarani. Bodi iliyokuwepo imemaliza muda wake toka mwezi Oktoba, 2011. Hata hivyo, Bodi hiyo iliyomaliza muda wake ilimshauri mambo mengi na mafanikio yote yaliyopatikana uimarikaji wote wa huduma za usafiri pamoja na usalama wake ni miongoni mwa faida zinazotokana na ushauri wa bodi hiyo. Sote tunakiri kwamba kwa hivi sasa sehemu nyingi mjini na vijijini huduma za usafiri zimeimarika vya kutosha.

Halikadhalika uwekaji wa matuta, alama za barabarani, *route* za magari, mpangilio kwa maana kwamba gharama za nauli pamoja na mambo mengine yote ni miongoni mwa ushauri unaotokana na Bodi hii ya Usafiri barabarani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri anasema bodi imemshauri kuhusu masuala ya matuta. Je, katika ushauri huo tunarudia katika suala letu la Pete, Kitogani na Muyuni zile skuli zinahatarisha wanafunzi na mmoja sasa hivi yuko hospitali mguu unaning'inia una msimamo gani kwenda kujenga matuta katika skuli za vijiji hivyo nilivyovitaja. Kama wizara itakuwa haina uwezo mimi mwakilishi niko tayari kujitolea kwa suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, suala la msingi lilikuwa ni faida zinazotokana na ushauri wa Bodi kwa wizara yetu. Miongoni ambayo Bodi imemshauri waziri na kuleta mafanikio ni suala la uwekaji matuta, alama za barabarani, *route,* nauli na mengineyo. Sasa suala la Mhe. Mwakilishi kwamba tukaweke matuta Skuli ya Muyuni, Pete na mwenginemo hili suala limejibiwa juzi na ameambiwa hasa kwamba yeye aende kwa Mhe. Waziri huu utaratibu wa hii Bodi itaendelea kutushauri sheha ataleta barua na yeye Mhe.

Mwakilishi ameshapewa hiyo *offer* ende kwa Mhe. Waziri tutakaa na tutazungumza na hayo matuta kama kuna uwezekano wa kuwekwa yatawekwa. Sasa msingi wa suala lake mimi sikulifahamu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wizara yake ndio msimamizi mkuu wa usafiri wa barabarani kumekuwa na ajali nyingi zikiongezeka mara kwa mara katika nchi yetu ambazo husababisha vifo, maafa na mambo mengine. Je, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ni ajali ngapi zimetokea katika nchi yetu.

Je, wizara yake kwa kuwa ndio msimamizi mkuu inashirikiana vipi na askari wa barabarani kupunguza ajali hizo ambazo zinaongezeka mara kwa mara.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, suala la idadi ya ajali nitamjibu kwa maandishi, lakini msingi wa jukumu la Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2003 inayohusiana na Usalama Barabarani jukumu lao Polisi ni kusimamia na kuona kwamba sheria hii inatekelezwa. Kwa hivyo, Wizara ya Miundombinu tumekuwa kama wasimamizi tunao-*regulate* shughuli za usafiri barabarani.

Sisi tuna jukumu la msingi la kushirikiana na Jeshi la Polisi na hata hizo kumbukumbu za ajali Jeshi la Polisi ndio waliopewa dhamana na jukumu kwa mujibu wa hii sheria wao kuziweka kumbukumbu hizo na sisi kutupatia. Hivyo basi, namuomba Mhe. Mwakilishi atupe muda tutamjibu takwimu hizo kwa usahihi wake kwa maandishi baada ya kuwasiliana na wenzetu wa Jeshi la Polisi ili kutupatia kumbukumbu hizo kama walivyoziweka.

Nam. 169

Kuunga Mkono Nguvu za Wananchi

Mhe. Salma Mussa Bilali - Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzíbar katika mfululizo wa ziara zake katika Mikoa ya Unguja na Pemba amekuwa akisisitiza uungaji mkono wa nguvu za wananchi katika kujiletea maendeleo katika maeneo yao. Katika kuona azma hiyo inatekelezwa ameitaka Wizara ya Afya kufuata mfumo wa Wizara ya Elimu kusaidia nguvu za wananchi katika umaliziaji wa majengo na vituo vya afya pale ambapo wananchi wameonyesha juhudi kubwa.

Katika utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais. Ni lini Wizara ya Afya itapeleka nguvu zake kumalizia kituo cha Afya kilichopo Mpapa, kituo ambacho kimefikia takribani asilimia 70% ya kumalizika kwake. Na kwamba kituo hicho kinatarajiwa kuhuduma watu (zaidi ya 7000) wanaojumuisha maeneo makubwa zaidi ya kumi na mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako tukufu swali lake Namba 169 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida, wananchi wanapotakiwa kujenga vituo vya afya hutakiwa kuja kuwasiliana na uongozi wa wizara kwa kukubaliwa kujenga kituo, kupewa ushauri na kupewa maelekezo pamoja na ramani ya ujenzi huo.

Wizara haikuarifiwa kuhusiana na ujenzi huo, lakini bado wizara iko tayari kushirikiana na Uongozi wa Wilaya, Jimbo na Wananchi wa Mpapa kukimalizia kitua hicho.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nataka kujua ni lini atatuma ujumbe wake au yeye mwenyewe atakwenda kufanya tathmini ya hatua ya jengo hilo lilipofikia ili aweze kumalizia jengo hilo na kuwaondoshea usumbufu wa maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, baada ya kuletwa suala hili timu yetu ya afya ya Wilaya ya Kati ilikwenda imeliangalia na inajua hiyo sehemu. Imeangalia vituo vyote vya afya, timu zote za afya za Unguja na Pemba zimetembelea sehemu zao na wanajua ni vituo vipi ambavyo vinatakiwa kumalizwa. Vituo ni vingi, kuna vile ambavyo viliripoti kwetu na hivyo ambavyo havikuripoti kwetu. Sasa inategemea ni kiasi gani tutakachokipata

na tutakavyoweza kuvitengeneza vituo hivyo, kuna vile ambavyo viko katika hali mbaya hivyo tutaanza navyo hivyo na tutatizama, tunaweka vipaumbele vipi tuanze navyo. Sasa inategemea chako kitakuwa katika kipaumbele kipi, wingi wa watu, ubaya wa kituo, tatizo liliopo hivyo ndivyo vitakavyokuwa vigezo vyetu na *Inshaallah* itafika wakati tutakijenga hicho lakini siwezi kukwambia kwamba nitakipa kipaumbele bila ya kukifanyia tathmini hiyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini napenda kumuuliza kwamba, utaratibu alioueleza ni mzuri sana na kwa kuwa wananchi wetu hawana ujuzi wala hawajapata elimu ya kujua hayo. Je, wizara yake imejipanga vipi kuwaelimisha zaidi wananchi ili wajue kwamba wanapoanzisha vituo vya afya kuna utaratibu unaopitwa ili kupata kuhakikisha kwamba kituo chao kinachojengwa kinafaa kujengwa au hapafai na kupewa hizo ramani za ujenzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza Mhe. Subeit nataka nikuulize hukushiriki semina ya kuambiwa kwamba vituo vya afya visijengwe? Kwa sababu kama unajua kwamba vituo vya afya sasa hivi havitaki kujengwa usingeniuliza suala hilo. Vituo vilivyopo vimetosha na kuna vingine ambavyo vishajengwa tunahitaji kuvimaliza tatizo tulilonalo hata tukivijenga hivyo vipya wafanyakazi hatuna na vitendea kazi hatuna. Lakini hata hivyo, hapo walipoambiwa walipewa maelekezo waende Wizara ya Afya wakaelekezwe, wakaambiwe kama panafaa kujengwa au hapafai. Kwa sababu vituo vingine labda viko karibu na kama panafaa wataambiwa sasa chukueni ramani hii utaratibu ni huu tuufuate.

Mimi napenda nichukue nafasi hii kuwafahamisha wawakilishi iliitwa semina maalumu kwa ajili ya hili na nafikiri sote tunaelewa, mimi ningependa iwe kama skuli vile zilivyojengwa kila kijiji na kituo chake, lakini kwa hali halisi ilivyo sasa hivi lengo la Umoja wa Mataifa tumelifikia kwa kujenga vituo lakini hatujalifikia kwa wafanyakazi wala kwa vitendea kazi, tumalize hiyo kazi kwa sababu hiyo itampa nafasi kila mtu kuweza kupata uwezo wa kufika kwenye kituo katika masafa yaliyokubalika. Baada ya hapo sasa ndio tutaanza kujenga kila ilipo skuli jengeni kituo kama haya yatakuwa yamekamilishwa tutaweza kutoa ruhusa hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hatuwezi kufanya hivyo, tupeni nafasi turekebishe, tujaze wafanyakazi, tuweke vitendea kazi baada ya hapo tutatoa tamko jengine kwamba jamani sasa tumekamilisha na kazi ni nzuri sasa na tuweke sera nyengine kuhakikisha kwamba kila mtu anajenga kituo kwenye shehia yake, kijiji chake ikiwezekana.

Nam. 109

Utumiaji wa Matrekta Katika Kilimo

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:-

Miongoni mwa ahadi za Mhe. Rais ni kuwasaidia zaidi wakulima. Kwa kuwa baadhi ya mabonde hulimwa kwa matrekta na matrekta yamepatikana wakati ardhi imekauka kutokana na uhaba wa mvua.

(a) Je, Mhe, Waziri utawasaidia vipi wakulima hawa wakati pesa zimeshachukuliwa.

(b) Je, pesa hizi zimepelekwa ofisi gani.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 109, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa baadhi ya mabonde yalikauka sana baada ya mvua na kipindi cha jua na upepo mkali, kiasi ambacho matrekta mwanzo yalishindwa kuingia. Hata hivyo, baada ya kuanza tena mvua ndogo ndogo wizara ilitilia nguvu kwa kununua matrekta mapya kuongeza nguvu ile iliyokuwepo, sehemu kubwa ya mabonde hayo yalipatiwa huduma hizo za kulimiwa kwa matrekta. Lakini hata hivyo, nakiri kuwa wapo wakulima kidogo ambao hawakuwahi kulimiwa na tayari maafisa wa kilimo wa Wilaya wameagizwa kuwaorodhesha wakulima hao ambao waliwahi kutoa fedha na hawakulimiwa. Hata hivyo, baadhi ya wakulima hao waliwahi kuchimbiwa mashamba yao kwa mkono

wamepanda mpunga na wameomba Wizara ya Fedha, fedha zao ziwekwe na zije kutumika kuwachimbia kwa ajili ya kilimo cha baadae.

b) Mhe. Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa fedha za wakulima hazipotei. Fedha hizo zilikusanywa na kutolewa risiti na kwa hivi sasa zinahifadhiwa katika *account* ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwa kuwa wakulima wa Jimbo la Muyuni wameitikia wito wa Mapinduzi wa utekelezaji. Je, ana mpango gani wa kuwakabidhi trekta liwe la kudumu baada ya kilio chao kwa kulalamika kwa Mhe. Rais alipotembelea Jimbo hilo kwa kuona kuna ekari nne hazikuburugwa na trekta kuondoka.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, sijamsikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wameitikia wito wa utekelezaji wa mpango wa Mapinduzi ya Kilimo hasa wananchi wa Jimbo la Muyuni. Alikwenda Mhe. Rais akatembelea na wananchi wakalalamika, kuna kama ekari nne zao hazikulimwa. Ili kukimbia tatizo hili ana mpango gani kuwakabidhi trekta wananchi hao likawa ni lao la kudumu ili wasije wakapata usumbufu kama uliotokea na kumlalamikia Mhe. Rais.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwa Jimbo la Muyuni limelimwa kwa wakati ambao ulikuwa umewekwa na katika kutekeleza hayo Mhe. Rais amejaribu kuongeza matrekta zaidi ya hapo na kuagiza *planters* 30 pamoja na *investors* 14 kutoka China, matrekta mengine mapya karibu kumi. Kwa hivyo, vifaa vingi ambavyo vinaelezewa hapo vitaweza kuongeza uwezo wa wakulima wengi ambao hawawezi kumiliki vitu hivyo. Hata hivyo, wizara yangu kwa kushirikiana na Mhe. Rais bado inaendelea kupata vifaa ambavyo vitaweza kuleta ufanisi katika eneo la Muyuni na sehemu nyengine kadhalika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nimeuliza mimi ana mpango gani wa kuwapa trekta la kudumu wananchi wa Jimbo la Muyuni ili kukimbia usumbufu uliotokea katika kipindi kilichopita baada ya eneo lao kutokuburugwa kwa kuitikia wito wa Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Hatuwezi kutoa ubaguzi kwa Muyuni tu, matrekta haya ni kwa nchi nzima Unguja na Pemba.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa serikali nyingi hususan zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara huwa zinatoa fidia kwa wananchi wake pale kwa makusudi zinaposababisha maafa au matatizo kutokana na uzembe, na kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kuna wakulima ambao fedha zao walitoa lakini hawakuwahi kulimiwa. Je, waziri anaweza kunijibu kwamba serikali ina mpango wowote wa kuwafidia wakulima hao ambao fedha zao walitoa lakini serikali kutokana na uzembe haikwenda kuwalimia mashamba yao. Moja

Pili, waziri anaweza akakubaliana na mimi kwamba serikali katika kauli yake ya Mapinduzi ya Kilimo ilikuwa haikuwa makini katika kutoa kauli ile.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, fedha za wakulima hao zipo na ndizo zitazowasaidia kupata ukulima huo kwa haraka kulingana na kipindi kilichopita. Swali lake la pili sijalisikia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, swali la pili nilisema kwa kuwa serikali nyingi hususan zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara kama sisi hivi huwa zinafidia pale zinapofanya uzembe na wananchi wake kuathirika. Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa ina mpango wa kulipa fidia kwa wananchi hawa baada ya uzembe walioufanya.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, watapewa fidia kutokana na kesi yenyewe ilivyo.

Mhe. Bi Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakulima hawa fedha zao zipo na msimu huu wamekosa kulimiwa

wizara ina mpango gani wa kuwapa kipaumbele wakulima hawa msimu ujao kwa kuzingatia msimu huu wamekosa mavuno.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Serikali itahakikisha kwa wale wote ambao fedha zao zipo wizarani kwetu, kuhakikisha wanapata huduma hiyo ya mwanzo kwa haraka iwezekanavyo.

Nam. 52

Matengenezo ya Nyumba za Kihistoria
Mji Mkongwe kupitia *MACEMP*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Aliuliza**:-**

Kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2011/2012, chini ya Mradi wa *MACEMP*, Wizara ilijumuisha katika Mradi huo matengenezo ya majengo mawili ya kihistoria yaliyopo Mji Mkongwe ambayo ni Jumba la *Beit-el-Ajaib* (sasa ni Makumbusho ya Taifa), na Jumba la Makumbusho ya Kasri (*People's Palace*). Hadi sasa hakuonekani matengenezo yoyote yaliyofanywa na majumba hayo mawili ya kihistoria yanaendelea kuharibika kiasi cha kutishia kuendelea kuwepo kwake.

(a) Fedha zilizotengwa kwa malengo hayo kwa nini hazijatumika kukamilisha kazi hiyo hadi sasa.

(b) Wizara itawachukulia hatua gani watendaji wanaohusika na Mradi wa *MACEMP* kwa kushindwa kutekeleza dhamana zao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 52 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kupitia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2011/2012, chini ya mradi wa *MACEMP* Wizara ilijumuisha matengenezo ya majengo ya kihistoria ya *Beit el-Ajaib* na Jumba la Makumbusho la Kasri (*people's Palace*) pamoja na *Peace Memorial* (*Beit el aman*). Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi ya kwamba kazi ya kutengeneza majengo hayo imeshaanza na inaendelea. Kwa upande wa jengo la peace memorial, kasri liko katika hatua za mwisho kumalizika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mimi mwenyewe karibuni nilitembelea majengo haya mawili niliyoyataja kwenye swali langu, jumba la Beit el Ajaib na jumba la makumbusho ya kasri, na hiyo kuwathibitishia Mawaziri kuwa tunafanya kazi nzuri ya kuyatembelea majimbo yetu na kuyatambua ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana na Mhe. Waziri kuwa jengo la makumbusho ya zamani (*Beit el Aman*) hivi sasa linafanyiwa marekebisho na matengenezo, lakini majengo haya ukienda hakuna matengenezo yoyote ya maana ya kiasi cha fedha ambacho kimetajwa katika bajeti iliyopita katika mradi wa *MACEMP* kwamba yamefanyika.

Na kinyume chake katika jengo la makumbusho ya kasri unakuta kuna matengenezo yanafanyika, lakini kuna kibango kinachoonesha kuwa kuna taasisi binafsi ambayo imejitolea kufanya kazi ile.

Nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie kwamba ujenzi huo unaozungumzwa umefanyika maeneo yepi katika majengo haya mawili, kwa maana ya Beit al Ajaib na makumbusho ya kasri, na kwa nini matengenezo hayo hayaakisi lile fungu ambalo tumelitenga mwaka jana katika bajeti hii kwa matengenezo hayo mawili ya kihistoria kwa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ninashukuru Mhe. Naibu Spika, kama nimemfahamu vizuri.

Kwa ufupi kama nilivyosema awali kwamba jengo la *Peace Memorial* lipo katika hatua za mwisho, na mimi mwenyewe binafsi nilitembelea hilo jengo, na ni kweli hivi sasa wameanza sehemu za ndani na hivi sasa wapo sehemu za nje katika kupaka rangi.

Na jengo la Beit el Ajaib kidogo lilikwama kwa sababu mkandarasi alileta bati ambazo si sahihi, na badala yake ameagizia bati nyengine kutoka Mombasa na wakati wowote zitafika. Kwa sababu matengenezo ya pale ni suala la umeme, *roof* pamoja na paa. Lakini wiki inayokuja wanaanza kufunga majukwaa na wataanza na *fitting* ya umeme, na bati zitakapofika ghalani basi yatakwenda sambamba na majengo hayo.

Kwa hivyo imani yangu ni kwamba kwa kweli miradi yote hii miwili inakwenda vizuri na itamalizika kwa wakati. Sasa kama kuna masuala mengine zaidi sina upeo zaidi, lakini nitafuatilia kama alivyosema nione kuwa yanakwenda sahihi na kwa wakati uliopangwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 112

Mfumo wa Digital katika Mitambo ya Televisheni Zanzibar

Mhe. Abdi Mossi Kombo - Aliuliza**:**
Hivi sasa utaalamu wa kutumia mitambo ya televisheni ambayo ijulikanayo kwa jina la *Analogi* umeshapitwa na wakati na itakapofika mwaka 2013 mitambo mipya ijulikanayo kwa jina la *Digital* itatumika.

Je, Serikali kupitia Wizara yake imeshawaelimisha wananchi wa Unguja na Pemba kuhusu suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe Naibu Spika, Kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 112 kama ifuatavyo;-

Mhe. Naibu Spika, Serikali kwa kupitia Tume ya Utangazaji ilianza kuwaelimisha wananchi wa Unguja na Pemba kuhusu suala hili tokea kupitishwa kwa maamuzi ya kuanza utangazaji wa televisheni za *digitali* mwaka 2006, kwa kupitia warsha na semina kwa watendaji wa vituo vya utangazaji, Maofisa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, aidha wananchi wameelimishwa kupitia vipindi mbali mbali vya redio na televisheni vinavyorushwa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar na Vituo binafsi. Aidha, kupitia Tume ya Utangazaji Serikalini imeandaa kampeni maalum kwa umma ambapo wananchi watafikiwa katika maeneo yao mijini na vijijini, kwa ajili ya kufikishiwa elimu hii. Kampeni hiyo inatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza.

Ni vipindi vingapi vya televisheni vimetolewa kwa kuelimisha wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu imeelimisha jamii kwa vipindi 18 kwa *ZBC* na redio binafsi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar imeingia katika mfumo mpya wa *digital*, tumetoka kwenye *analogue* na kuingia huko, na kwa kuwa mfumo huu ni mpya katika nchi yetu ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri. Jee ni wafanyakazi wangapi wa TVZ wamefaidika na mafunzo ya *digital* kutokana na *analogue*, na jee kama wamefaidika ni wafanyakazi wa kada gani na kama bado ni lini serikali itaona umuhimu wa kuwapa mafunzo wafanyakazi wetu wa TVZ ili waende na wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwakilishi kwenye swali mama tumeeleza kuwa tumewapatia mafunzo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji mbali mbali wa wizara zote za Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwakilishi kwa kweli suala hili ni zuri na swali umelifahamu vizuri, lakini Mhe. Mwakilishi wewe pia ukiwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi uelimishe jamii ili kujua kutoka kwenye mfumo wa *analogue* na kuingia kwenye *digital*.

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nimemuuliza Mhe. Naibu Waziri wafanyakazi wangapi wa TVZ wamepata mafunzo ya digital na sio wananchi na kada gani, na kama bado ni lini, ndivyo nilivyomuuliza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwanza naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa ufafanuzi wake katika swali mama na swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, masuala haya ya mafunzo ya kuelekea katika digital ni suala ambalo linaendelea hivi sasa katika wizara yangu kwa nguvu sana. Wizara kwa kushirikiana na Sauti ya Ujerumani inaendesha mafunzo katika ZBC televisheni kwa wafanyakazi wote na wa section zote, kuanzia waandishi, watengenezaji vipindi na mafundi wa televisheni.

Kwa hivyo idadi kamili tutamletea kwa maandishi lakini naomba nimuarifu yeye na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukufu kuwa suala hili la mafunzo tunaenda nalo, tunalishughulikia na linashughulikiwa kwa ujumla.

Hivi majuzi tu kikosi cha mwisho cha wafanyakazi wafikao 30 walikuwa na darasa pale kwa muda wa wiki tatu iliyoendeshwa na wataalamu kutoka Ujerumani. Tunategemea kwamba mwezi wa Agosti watakuja wataalamu pia kutoka Sauti ya Ujerumani na watakuwepo hapa kwa muda wa miaka miwili kwa ajili ya mafunzo ya jumla kwa ajili ya wafanyakazi wote wa ZBC, redio na televisheni.

Kwa hivyo tumeanza kwa kiwango kikubwa na pia tuna mpango wa kuona kwamba wafanyakazi wote wameelimika katika suala hili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, alau na mimi kunipatia fursa ya mwisho kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Waheshimiwa Manaibu Waziri na Waziri mwenyewe, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hivi vyombo vya digital ni ghali sana na kwa kuwa Wazanzibari zaidi ya asilimia 80 wanatumia hizo televisheni za analogue, na kwa kuwa televisheni hizi zikishafungwa ving'amuzi zinaweza zikafanya kazi vizuri.

Jee Mhe. Waziri wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wana mpango gani wa kupunguza ushuru kwa wafanyabiashara watakaoleta ving'amuzi hapa nchini, kusudi wananchi wavinunue kwa bei nzuri kuweza kufunga ving'amuzi hizo televisheni zao.

Swali la pili kwa sababu kuna baadhi ya televisheni za analogue zitakuwa hazifanyi kazi tena na itakuwa ni *a sort of waste products* ambazo zina matatizo ya kimazingira. Jee wizara yenu ya habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais muna mpango gani kuona hizi televisheni zilizokuwa hazifai tena mutazifanya nini ili zisije zikaathiri mazingira ya hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake zuri lenye vifungu (a) na (b).

Suala la kupunguza ushuru. Mhe. Naibu Spika, hili ni suala la kibiashara. Wafanyabiashara wanaoleta bidhaa hizo wanapata faida kubwa. Kwa hivyo sioni kwamba kuna umuhimu wa kupunguza ushuru wakati wenyewe wanafaidika na faida nzuri inayotokana na biashara hii. Kwa hivyo hili ni suala la maana.

Suala lake linalohusiana na uchafuzi wa kimazingira. Kwanza ninataka nimwambie kwamba televisheni zote ambazo zinatumia mfumo wa analogue, zikipata ving'amuzi hivi vitaweza kutumika kwa kuonesha kwa kutumia huu mtindo mpya wa digital.

Sasa sahihi kwamba televisheni zote ambazo hivi sasa zinatumia mtindo wa analogue zitakuwa hazitumiki tena. Zikipata king'amuzi basi zitakuwa zinatumika. Kwa hivyo hakutakuwa na televisheni nyingi ambazo zitakuwa hazitumiki.

Lakini la msingi ni kweli kwamba kwa ujumla uletaji wa vifaa vya *electronics* katika nchi unasababisha ile inayoitwa *E-wastes* ambazo kimazingira ni matatizo makubwa. Kwa hivyo hili ni jukumu la wizara inayoshughulikia mazingira kuandaa utaratibu wa namna gani vifaa hivi vinaweza kuwa-*deposited* bila ya kuathiri mazingira.

Ninaamini kwamba Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ina utaratibu mzuri na sisi watu tunaoshughulikia utaalamu, tupo tayari kushirikiana nao kuona kwamba athari ya kimazingira haitokani na matatizo na vifaa hivi vya *electronics.*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 –
Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma malizia dakika kumi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii nikamalizia dakika zangu 10, nitajitahidi niende haraka haraka ili nimalize.

Mhe. Naibu Spika, jana nilimalizia nilipotoa pongezi kwa Mhe. Waziri kwa kuweka *database* ya mahitaji ya wafanyakazi katika serikali yetu. Tunashukuru kwa kutuletea hili.

Sasa vile vile kwamba ametangaza kwa mwaka huu atakuwa na nafasi karibu zaidi ya elfu mbili. Kitu ambacho nilichokuwa ninakiomba Mhe. Waziri kuna baadhi ya maeneo, kwa mfano katika Halmashauri zetu na maeneo mengine tayari kuna watu wanajitolea, hata katika vikosi vyetu vya SMZ ninafikiri Mhe. Waziri anayehusika na vikosi hayupo, lakini tayari kuna vijana ambao wanajitolea zaidi ya miaka mitano wengine na umri unakwenda.

Sasa ni vizuri pamoja na kwamba tumepitisha sheria kwamba kila ajira lazima ifanyiwe *interview*. Si vibaya na wao wakafanyiwa *interview* lakini kuzingatia nadhani na wao ni muhimu kuangaliwa.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, bado hapo hapo katika utumishi kuna malalamiko kidogo kwa baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Elimu, aidha ni walimu au wafanyakazi katika wizara ambapo katika nyongeza ya mwaka huu wao kulikuwa kuna fedha ambazo walitakiwa walipwe, lakini Wizara ya Elimu wao wakasema hawana uwezo wa kuzilipa fedha hizo karibu shilingi milioni 30.

Na wakasema fedha hizo zitalipwa moja kwa moja kupitia Utumishi wa Umma, sasa hapa nitakuja kutaka ufafanuzi kidogo. Kwa sababu Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora mimi ninajua kwamba wao hawalipi fedha, wao kazi yao ni kuagiza tu kwamba hawa walipwe hiki, lakini Wizara ya Elimu kule wao wanawaambia hivyo na kwa bahati nzuri mumekaa pamoja hapo mutajaribu kulizungumza hili ili kujua ufafanuzi wake utakuwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kulikuwa kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wamepewa dhamana katika taasisi mbali mbali na wamepata barua kutoka Utumishi wa Umma kukabidhiwa dhamana zote, aidha kwa lugha yetu munayoisema nyinyi wazungu ni kupewa *post.*

Hapa tunauliza mtu anapopewa dhamana hakuna nyongeza yoyote ya kukamata ile dhamana? kwa sababu hapa watu wamepewa dhamana wanahoji kuwa hawajapata yale marupurupu ya zile dhamana walizopewa.

Lakini vile vile kuna suala zima la vipaumbele vya mwaka ujao. Mhe. Naibu Spika, jana nilisema na nilijaribu kumwambia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba, bajeti ya mwakani ni vizuri yale malengo tukapatiwa mapema baadhi ya zile kamati au hasa kamati ya wenyeviti kuangalia vile vipaumbele.

Sasa hapa kuna kile kilio cha madiwani wetu. Mhe. Naibu Spika, katika suala zima la utawala bora, na wizara yako ndio iliyokabidhiwa huu utawala bora, bado Madiwani ni Wawakilishi wa wananchi kama sisi lakini mpaka leo wanaishi kwa kutegemea posho, na posho linakuwa halina hatma. Sasa tunaomba mwakani wizara yako basi ingeanza kuangalia madiwani wapo wangapi na watahitaji kiasi gani *at least* tuangalie katika vile vipaumbele, basi alau na wao tuanze kuwaangalia tunapokuja kumaliza na wao wapate kile cha kuondokea.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, *formular* munayoitumia katika ulipaji wa mishahara, kwa sababu tulijaribu kuwauliza watu wa Wizara ya Fedha wakasema aah! sisi tunaambiwa tu hawa walipwe hivi na wale vile. Kwa sababu Utumishi wa Umma nyinyi kazi yenu ni kutoa miongozo lakini walipaji ni Wizara ya Fedha. Sasa munakaa kushirikiana vipi katika kupanga hii mipango ya kutoa mishahara. Ninafikiri Mhe. Waziri wa Fedha hayupo lakini utamwambia ili muje mutujibu ili tupate ile jawabu ambayo itakayokuwa ya uhakika.Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, tumeangalia hapa fungu hapa la Mipango na Sera. Fungu hili lipo kubwa lakini maelezo yake ni finyu lakini kuna idara nyengine katika kazi za maendeleo fedha zake hatuzioni.

Sasa sijui ziko huko kwenye mipango na sera, lakini kama zipo kwenye mipango na sera, nani atakayewajibika katika usimamizi wa fedha hizo. Kwa sababu kama Fedha mfano wa Idara ya Nyaraka zikasimamiwa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango, sasa inapokuja kutokea matumizi mabaya, sijui nani hapo atakayekuwa anawajibika nani zaidi atakayeweza kuzisimamia vizuri.
Mhe. Naibu Spika, vile vile nilikuwa naomba kidogo uende kwenye buku fungu 14. Naomba uangalie ukurasa wa 16 katika *special allowance.*

Hapa tumejaribu kuangalia kwamba fungu hili katika bajeti iliyopita lilikuwa karibu shilingi milioni arobaini mia tatu na *something*, lakini mwaka huu limeongezeka karibu maradufu, limekuja karibu shilingi milioni mia moja na thalathini na mbili. Hili tu tutakuja kuhitaji maelezo.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, katika fungu hili hili fungu la 14 ukurasa wa 18, kuhusu ada ya malipo. Hii inakuja ada ya malipo kuna fungu hili linasema kwamba, “mwaka uliopita kulikuwa kuna bajeti ya shilingi milioni saba lakini bajeti ya mwaka huu lipo karibu shilingi milioni hamsini na tano. Sasa hili vile vile tutakuja kuhitaji maelezo.

Lakini vile vile kwenye ukurasa wa 18 kuna gharama za ukodishaji, sijui mambo ya mashamiana na vitu vyengine. Lakini hili fungu kwa kweli naona limeongezeka sana. Mwaka uliopita lilikuwa shilingi milioni moja lakini mwaka huu kuna karibu shilingi milioni mia moja na thamanini na sita. Sasa sijui kama ni *typing error* au vipi.

Lakini kama hiyo itakuwa ndio sahihi basi ninadhani hapa Mhe. Waziri kidogo nitakuja kuhitaji maelezo ya ziada. Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka ninakwenda na kurudi katika Afisi ya *Auditor General*.

Mhe. Naibu Spika, eneo hasa ndio kwenye utawala bora kwa sababu wao ndio wanaotakiwa kuichungulia na kuimurika serikali katika fedha ambazo tunazozipitisha hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Lakini Afisi hii sina taarifa kama na wao wanakaguliwa. Sasa sijui utaratibu wao upo vipi. Hapa tutakuja kuhitaji maelezo.

Lakini vile vile wameeleza hapa katika suala zima la ukaguzi tunaambiwa kuwa hivi sasa kuna ukaguzi wa mazingira, ukaguzi wa kitaalamu wa *electronics* na kompyuta. Vile vile Mhe. Naibu Spika, hapa hivi sasa kutokana na miradi mingi ambayo inayoekezwa kwa Zanzibar na fedha ndio sisi tunaoidhinisha, basi ninadhani hivi sasa imefika wakati wa kufanya na *technical auditing* vile vile.

Kwa sababu kwa Waheshimiwa Wajumbe kamati ya PAC wanapokwenda katika eneo wataangalia *value for money*, lakini hawana utaalamu wa *engineering*, hasa ule ubora au uimara hasa wa lile jengo ambalo litakalokuwa limejengwa. Sasa mimi ninadhani ni muhimu sana kuangalia.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, utakuja hapo mbele kuna baadhi ya Wizara zitakuja na bajeti zao, sisi tutahoji sana ile miradi iliyojengwa, fedha zilizotumika na hatua zilizofikia, na leo tunaombwa fedha nyengine kwa ajili ya maeneo yale yale wakati *impact* yake bado hatuioni.

Sasa hili ndio nikasema hivi sasa *Auditor general* anatakiwa aende *deep* zaidi. Lakini vile vile ninaomba afisi hii ya *Auditor General* ifanyiwe *audit* ya *human resources auditing* ya afisi yenyewe. Kuna malalamiko kidogo. Katika *human resources* naomba kidogo lifanyiwe kazi. Kwa kuwa Mhe. Naibu Spika, unacheka cheka ninajua umeshajua kwa sababu nikitaja hapa kidogo mambo mengine watoto wadogo watapata kujua, haya ni mambo ya kiofisi, naomba ufanye *human resources auditing*. Ninafikiri nikisema hivyo Mhe. Waziri ninadhani umenifahamu vizuri.

Sasa ninadhani…

Mhe. Naibu Spika: Umebakiwa na dakika 3.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hii. Mhe Naibu Spika, samahani sana kwa kuwa na wenzangu wanahitaji kuchangia na ninaamini na mengine watamalizia. Sasa baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nitakuja kuachia bajeti hii hasa nitakapopata hasa ule muhimili wa tatu ambao haujapata haki zake, Majaji wa Mahakama ya mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri anayehusika na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetujaalia leo kuwepo hapa wazima wa afya.

Ninachukua fursa hii adhimu vile vile kumpongeza sana Waziri pamoja na watendaji wake wote. Kwa kweli kazi nzuri ambayo wameianza, kwa sababu hii wizara tunafahamu ni mpya lakini imeanza kutupa matumaini makubwa hasa kwa wale watumishi wa umma. Kwa kweli ninampongeza sana pamoja na watendaji wake wote.

Lakini ninachukua fursa hii vile vile kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar. Kwa kweli maamuzi yake ya kuanzisha wizara hii tumeona alikuwa na muono wa mbali sana, na kwa kuwa na yeye alikuwa ni mtumishi wa umma, kwa hivyo ameona ipo haja ya kuwa na wizara hii ambayo itakuwa inaweka haki za watumishi wote pamoja na kuwa na utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza ukurasa wa 3 ambao unaelezea hasa majukumu ya wizara hii. Kwa kweli wizara imepewa majukumu makubwa sana. Haya majukumu yanasema wajibu wao kusimamia, kudhibiti, kuratibu, kutathmini, utekelezaji na uongozaji wa utumishi wa umma na utawala bora kwa kuzingatia misingi ya dira ya MKUZA, *vision* ya 2020 pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Hii ni kazi kubwa kwa sababu sote tunaelewa kuna changamoto gani katika wizara na idara zetu na utekelezaji wetu wa shughuli mbali mbali za kimaendeleo, hasa katika kutoa huduma. Mimi ninamuomba Mhe. Waziri kwa kweli kama ni kusimamia basi wanaohusika na kusimamia wasimamie vizuri, kwa sababu bado huduma sio nzuri. Wasimamizi bado ambao wengine wanateuliwa na Rais lakini kwa kweli usimamizi wao sio mzuri hata kidogo na wananchi wanalalamika. Kwa hivyo, namuambia Mhe. Waziri kwamba wananchi wanalalamika sana, kutokana na huduma mbovu ambazo zinatolewa katika maeneo yetu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 12 ambao unazungumzia suala la kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Mimi napenda kumpongeza sana Waziri kwa juhudi zake ambazo anachukua katika kuwapa elimu wafanyakazi wake, pamoja na wafanyakazi wa serikali katika idara mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, nina wasi wasi mkubwa ni kwenye haya mafunzo ambayo yanatolewa kweli yana tija, lazima Mhe. Waziri kuwepo na tathmini ili uweze kuwatathmini wale ambao wamepewa fursa ya kupata mafunzo, je uwezo wao wa kufanya kazi umeongezeka? Hilo ni muhimu sana, isijekuwa yanatolewa mafunzo watu wanakwenda kwa malengo ya kupata chochote, lakini baadae wanaporudi sehemu zao za kazi hali ni ile ile. Nasema hivyo kwa sababu Mhe. Waziri nimeangalia katika kitabu chako kikubwa ambacho kina kasma za mafunzo mbali mbali, zikiwemo semina na warsha, fedha nyingi zinakwenda katika maposho ya semina, ni fedha nyingi sana. Mhe. Waziri mimi nataka uje utuelezee hapa. Idara moja inaweza ikawa na kasma ya milioni 98,500,000 ya semina. Sasa Mhe. Waziri hebu uje utueleze hapa hizi semina zinakua ni ngapi, vikao vya kamati vinakuwa vingapi kwa mwaka na Wajumbe ni wangapi. Hapa ni lazima tufahamishwe Mhe. Waziri, kuna vikao vya idara ambao wana posho, *sitting allowance*, ambapo hiyo *sitting allowance* kwa mwaka mzima ni milioni 98,500,000.

Mhe. Waziri ukipiga mahesabu kwa kila kikao kimoja, kama unafanya kikao kimoja kwa mwezi basi haipungui milioni 5,000,000 kwa kikao kimoja, hivi hao Wajumbe wako wangapi. Hiyo ni *sitting allowance* tu, hapo bado kuna fedha bado zinatumika katika viburudishaji. Kwa hivyo, Mhe. Waziri sisi tunajua umuhimu wa kuwa na semina, tunajua umuhimu wa kuwa na vikao, lakini tunajua umuhimu wa wananchi wetu au watoto wetu kukalia ma-*desk*, umuhimu wake ni mkubwa. Kwa hivyo, hizi fedha tunataka utueleze na sio idara moja tu, ni idara nyingi sana zina fedha zinazotumika kwa *sitting allowance*, pamoja na viburudishaji. Uje utuambie Mhe. Waziri ni mara ngapi hawa watu wanakaa, kama ni kamati watu wanakaa tuambie ni mara ngapi, ili na sisi turidhike tujue kwamba kweli hizi pesa zinatumika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza sana Wizara kwa bidii yao ambayo sasa hivi wameifanya, nimeona wana mkakati mzima ambao utasaidia katika kusajili vijana wanaomaliza masomo ili waweze kujua ni vijana wangapi wanahitaji kazi. Mimi nafikiria hili ni la kupongeza sana.

Mhe. Spika, hii ikiambatana na e-*government* ambayo inakuja mimi nafikiria itasaidia sana. Kwanza Mhe. Naibu Spika, nimueleze Mhe. Waziri kuwa kuna umuhimu mkubwa sasa hivi wa kuanzisha kituo maalum, kituo ambacho vijana wetu watakuwa wanakwenda pale na ambacho kitakuwa ni bure kabisa, watakuwa wanakwenda pale ili waweze kupata *access* ya kujua kuna ajira ngapi, zikiwa za hapa nchini na za nje ambazo wao wanaweza kupata ajira. Hilo ni jambo muhimu sana Mhe. Naibu Spika, kwa sababu vijana wetu wengi bado hawajaweza kujua mbinu za kutafuta ajira, sasa tuwasaidie, sisi ndio waongozi wao tunaowaongoza, wizara ichukue hatua hiyo ya kuhakikisha tuwe na kitengo maalum ambacho kitakuwa kina ajira zote za ndani pamoja na za nchi za nje. Tukipata hiyo basi tutakuwa tumewasaidia sana vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nichukue fursa hii adhimu ya kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar kwa kumchagua mwanamke mwenzetu kuwa Mdhibiti Mkuu wa Matumizi ya Serikali ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mwanamke huyu ni mahiri sana, simsifu kwa sababu ni mwanamke mwenzangu hapana, namsifu kwa sababu anaweza, ameonesha anaweza. Kuna wadhibiti wengi Afrika Mashariki, lakini sehemu nyingi kumpata Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni vigumu, lakini huyu anaweza.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba kitu kimoja mpe nguvu, kwa kuwa anaweza basi mpe nyenzo, mpe uwezo wa kuweza kufanya kazi zake vizuri, kama hatapewa uwezo huyu mtu basi uwezo wake wa kufanya kazi hautoonekana, apewe uwezo ili afanye kazi, na ile kazi ambayo anaitoa, *report* ambazo anazitoa zifanyiwe kazi.

Mhe. Waziri, unajua Tanzania Bara hivi juzi tu *report* za Mdhibiti Mkuu wa Serikali ndizo zilizomsaidia Rais kujua maovu yanayofanywa na watendaji wake wakuu, ndio maana alibadilisha *cabinet* yake.

Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kuna siku mimi nilinunua karanga njiani, alikuwa muuza karanga yule miongoni mwa wanaopita na vigari, nikanunua karanga baada ya kununua zile karanga, nikafungua ile karatasi moja sijui ukurasa wa ngapi, lakini ni *report* ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali, aibu. Kwa hivyo, ile inachukuliwa wanafungia karanga, ndio kazi yake ikimalizika basi, lakini je *report* ile inafanyiwa kazi. Lengo hasa la kuwa na ofisi ile ni nini tujiulize, ikiwa kama hatuifanyii kazi ile *report* yake na ule ushauri ambao anautoa tuifunge ofisi haina maana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimalizie kwa kumwambia Mhe. Waziri kuwa, mimi nina swali moja ambalo huwa mara nyingi sana linanisikitisha, naomba hili litizamwe tena kuhusu mishahara ya walimu. Nasema hivyo kwa sababu Mhe. Waziri mimi nilikuwa mwalimu nimesomesha, najua kazi ya ualimu ilivyo ngumu, ingawa

tunaambiwa kazi ya ualimu ni ya kujitolea, lakini vile vile walimu wanataka maslahi. Inasikitisha sana kwamba walimu wanafanya kazi kubwa sana, na kitu ambacho kinavunja moyo, unajua watoto wetu siku hizi ukimwambia awe mwalimu, anakuambia mwalimu anakufa maskini. Yule mtu ambaye anawatayarisha wataalamu ndiye anayeumia na anakufa maskini. Kwa kweli mimi bado sijaridhika na mishahara ya walimu bado hairidhishi na ndio wenye kazi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, mwalimu mmoja anasomesha darasa moja lenye watoto 100, jamani tuwaonee huruma walimu. Mwalimu huyo huyo anapewa na majukumu mengine zaidi ya ualimu, lakini anafanya. Nakuomba Mhe. Waziri walimu wengi wanaanza kutukimbia na hasa walimu wa sayansi. Tuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi, inasikitisha sana kwamba watoto wetu ambao wanapasi vizuri *form four* kuingia *form five* na *form six* wanapasi vizuri sayansi, lakini wakifika *form six* hawafanyi vizuri kwa sababu hatuna walimu wa sayansi. Hebu toeni mishahara ya kutosha kwa walimu wa sayansi, ili tuwe na *incentive* maalum kwa walimu wa sayansi, ili vijana wetu wanaomaliza masomo ya sayansi wavutike kuingia katika fani ya ualimu.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho kabisa ambalo nataka kulizungumza ni jumla ya utendaji wa kazi katika wizara zetu mbali mbali. Mhe. Waziri wakati sisi tulipokuwa wadogo tulikuwa tunawaona wazee wetu wanafanya kazi, na kwa hakika kazi zilikuwa zinafanywa. Kulikuwa kuna ari ya kufanya kazi, kulikuwa kuna *commitment* ya kufanya kazi sasa hivi hakuna. Nakuambia Mhe. Waziri utasomesha mpaka utachoka, lakini *commitment* ya kazi haipo. Sijui nani kaja kaichukua akaondoka nayo. Wengine wanasema mishahara ni midogo na kila mmoja anasema lake.

Mhe. Waziri tufanye kitu kimoja, hebu tuanze kutathmini, tunaanza wizara tathmini za utendaji iwe *quarterly*, iwe ya wizara, idara, ikiwa kama ni *department* maalum, lakini mpaka kwa wafanyakazi mmoja mmoja, *individual*. Tufanye hiyo tathmini kila *quarter* aseme kafanya nini, kazalisha nini, kama kuzalisha katoa huduma gani na kwa watu wangapi, hiyo itasaidia sana Mhe. Waziri kwa sababu mara nyingi sana tukienda katika sehemu nyengine kwa kweli huduma hamna nzuri, halafu wizara zetu zote na idara zetu zote ziwe na sehemu maalum sasa hivi ya kusikiliza maoni ya watu.

Mhe. Naibu Spika, liwepo *desk* maalum la kuwasikiliza wale wateja ambao wamekuja pale, au watu ambao wanataka huduma pale, je wamepata huduma ya kuridhisha. Tukifanya hivyo Mhe. Waziri nakuhakikishia kazi zitafanyika, lakini sasa hii tabia tuliyonayo sasa hivi ya kwamba mtu unaondoka unakwenda kazini mradi umekwenda kazini, ukifika kazini huna unachokifanya, tunaanza kuirithisha kwa wengine ambao wao wanakuja maofisini wanakuta hali ndio ile, wanasema mbona wengine hawafanyi kwani mimi nani nifanye, ipo hiyo Mhe. Waziri.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri awakamate wafanyakazi wake sawa sawa sasa hivi, kama tunataka maendeleo, rasilimali watu ni muhimu sana, na hii rasilimali watu ni lazima iwekewe mikakati ili watumike vizuri, watoe huduma vizuri na hatimaye tutaona maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache, mimi nachukua nafasi hii tena adhimu kumpongeza Waziri. Najua kuwa Waziri uwezo anao na Mwenyezi Mungu atamjaalia uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake. Pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelezo mazuri sana ambayo yataturidhisha kuhusu matumizi yake hasa ya vikao vya kamati, pamoja na semina. Tunataka tu utuambie hesabu zako ulivyozipanga, kwa sababu tunajua kwamba kwa mwaka mna *plan* maalum, ambapo hiyo *plan* mna *activity* zenu ambazo mnazifanya, hiyo ni uhakika. Lakini turidhishe na sisi ili tujue kwamba hizi pesa kweli zinatumika kama ilivyopangwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Naunga mkono hoja nitakapopata majibu, ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu kwenye hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi yake kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, nikianza mchango wangu nitaanzia pale pale kwenye ukurasa wa 3 kwenye majukumu ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwenye fungu la 8 pale, Mhe. Waziri ameandika hapa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jukumu la kusimamia utendaji wa watumishi wa umma ili waweze kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu cha ufanisi na kuimarisha utawala bora nchini.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu hayo ofisi ina wajibu wa kusimamia, kudhibiti, kuratibu na kutathmini utekelezaji na uongozi wa utumishi wa umma na utawala bora. Mimi nianzie hapo Mhe. Naibu Spika, waswahili wanasema kabla ya kutoa kibanzi kwenye jicho la mwenzio, kwako wewe kuna boriti lakini unakwenda kutoa kibanzi kwenye jicho la mwenzio inakuwa kidogo ni tatizo, ina maana ushughulikie lile boriti lako lililokuwemo kwenye jicho kwanza ulitoe.

Mhe. Naibu Spika, kama utakumbuka sio muda mrefu sana hapa iliwasilishwa *report* ya Kamati teule, iliigusa wizara hii kwa sababu kulikuwa kuna matatizo ya utumishi, kuna watu waliajiriwa bila ya kuwa na sifa, kuna ajira nyengine ziliambiwa ni za upendeleo na zilionekana mule. Kwa hivyo, hili linamgusa Mhe. Waziri. Siwezi kusema kwamba yeye moja kwa moja ndiye aliyefanya kile kitu, lakini kwa sababu kimefanywa na wizara yake, ina maana watendaji wake yeye ndiye msimamizi mkuu wa ile wizara, na ndio maana leo katika bajeti hii inabidi nimchangie katika hilo kwamba hebu na yeye kwanza apaangalie hapa, aje atueleze katika hili yeye analionaje na nini amefanya. Kwa sababu inaonekana iko wazi kabisa kwamba taasisi yake inayoshughulikia mambo ya uajiri iko kwake pale.

Mhe. Naibu Spika, tatizo lile la uajiri katika *report* ya kamati teule limeonekana limekuwa pana kidogo. Sasa hebu Mhe. Waziri utakapokuja hapa tusaidie maelezo kidogo, hatua ambazo wewe kama Waziri umefanya nini katika wizara yako juu ya tatizo hili ambalo lilizungumzwa kwenye Kamati Teule, kabla ya kusubiri hiyo *report* kuu ya serikali ambayo sijui itawasilishwa lini, lakini wewe kama Waziri hebu tuambie hatua ambazo umefanya pale katika wizara yako, katika kuliona labda na wewe limekukereketa. Maana yake hii dhana ya utawala bora iko pana sana, na wewe ndio msimamizi wetu mkuu pale. Kwa hivyo, tungeona faraja au tungesikia fahari kama tungekuona wewe ndio umeanza zaidi pale, halafu ile *report* itakayowasilishwa hapa, ikawa imekuja kutilia nyama yale ambayo umeshatueleza sisi wenzako hapa. Maana yake dhana ya utawala bora ni nchi kuwa na utawala wa sheria, haki za binadamu, kuwa na demokrasia, uwajibikaji na vitu kama hivyo.

Kwa hivyo, hebu tusaidie Mhe. Waziri uje utupe kidogo, maana yake pale pameonekana pana ubadhirifu, uwajibikaji haukuwa mzuri. Inaonekana watu wanakwenda kibinafsi zaidi kuliko kwenda kuangalia ule utaratibu mzima wa sheria unavyosema. Sasa hili nimeona Mhe. Waziri ni doa kwako hebu njoo ulitie jiki ulisafishe, ili liondoke kabisa ili na sisi wenzako ambao sasa unakuja kutuomba hapa ili tuangalie ule uwezekano wa kusema usimamizi wako unaturidhisha, sasa tunaendelea kukupa mafungu ili uweze kuendeleza shughuli zako.

Nikiendelea mbele Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata marekebisho hapa yanaonekana ya kile kitabu kikubwa ambacho kimetoka cha makadirio na matumizi, kuna marekebisho yametoka ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kuna mabadiliko sio nyongeza zaidi, lakini hizo hizo bado nimeziona kidogo kuna matatizo. Sasa nilikuwa nataka nimuombe Mhe. Waziri ajiandae na hili kuja kutupa ufafanuzi mzuri. Kuna fungu moja nataka nitoe mfano hapa, kuna vote ya 01111 Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

Sasa hizi nimepata shaka sijui ziko mbili au vipi, kwa sababu mbele yake tena nimekuta kuna Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Hii vote yake ni 0301 aah hii ya Ofisi Kuu Pemba, hii ni ya kumalizia. Sasa hapa kuna mafungu hapa ya posho, vikao na kamati. Haya mafungu kwa kweli Mhe. Waziri yako manene mno, la Unguja na la Pemba. Hetu utakapokuja Mhe. Waziri uje utusaidie ufafanuzi katika mafungu haya kabla na haya mengine hatujaja kuyatia pingu. Maana moja kati ya jukumu letu katika chombo hiki ni kuangalia hayo matumizi yenyewe unayotaka, tukukubalie au tuyapunguze. Hatukuzidishii hapa, lakini tunakupunguzia. Kwa hivyo, nina hofu tusije tukakupunguzia halafu ikawa hivyo vikao vikawa havifanyiki. Kwa hivyo, uje utupe maelezo mazuri ili tuweze kukuridhia uweze kupata hayo matumzi yako kama ulivyoyaomba.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nisiende sana kwenye hii dhana ya utawala bora, Mhe. Mjumbe aliyetangulia ameizungumza sana na ameichambua vizuri namna ya utumishi na mambo mengine. Mimi hivi sasa niiwache na nirukie kwenye ukurasa wa 33, kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi niungane na wenzangu kuipongeza sana ofisi hii, hasa msimamizi mwenyewe wa ofisi hii huyo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ofisi hii mimi naweza kusema ni ya mfano, kwa namna ya utendaji wake. Kwanza inajitahidi katika kufanya kazi zake, ingawa naweza kusema inapata mashirikiano madogo na huko inakokwenda kufanya kazi, ndio maana tukaibuka kuna tatizo limejitokeza hapa ambalo Waheshimiwa Wajumbe hapa wamelizungumza, namna ambavyo kamati zinakwenda na ndio zinakuta yale mabomu, wakati mdhibiti amekwenda lakini hakuweza kuyaona. Mimi nasema sio kweli

kwamba hakuweza kuyaona. Mimi wasi wasi wangu ni kwamba ushirikiano anaoupata na wale watendaji kule unamsababishia asiweze kuona.

Kwa mfano, anaweza kutaka mikataba, mara nyingi sana watendaji wetu wanakataa kutoa mikataba kwa ajili ya mdhibiti kuikagua. Sasa kama hakupata huo mkataba ata- *comment* kitu gani na yeye hakuupata, hili ni tatizo. Lakini haya ni mapungufu mimi nafikiria vile vile kwenye sheria. Kwa sababu kwa vitu kama hivi ingekuwa imewekwa vizuri kwenye sheria za fedha, namna ambavyo kama mdhibiti anaweza kumuita Afisa, akamtaka kutoa vile vitu, kama hakutoa kukawa kuna adhabu zimewekwa. Nafikiri hii ingemsaidia kwake kwamba angekuwa mtu labda ana hofu kupata adhabu.

Mimi nafikiria Mhe. Naibu Spika, tuiangalie ile sheria yenyewe ya fedha, akiitwa yule mtu au afisa akiitwa na mdhibiti, hakwenda anapata adhabu gani. Nadhani tukiangalia kwenye sheria ya fedha hatuoni ile adhabu ambayo anaipata yule afisa, kwa hivyo hana hofu. Kwa hivyo, hapa katika kufanya wajibu wake kunakuwa kidogo kutatetereka kwa sababu kama yule mtu anamtaka jambo fulani na yeye hatoi, kwa hivyo hawezi kufanya kazi zake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ofisi hii inafanya kazi zake vizuri, huyu mama kwa kweli anajitahidi sana na hizi mbinde unazoziona za PAC, mimi naweza kusema ni mafanikio ya kazi yake. Anaisaidia sana Kamati hii kuiwezesha, kuipatia mafunzo ikaweza kujua haya mambo. Kwa hivyo, kama Wajumbe wanakiri kwamba PAC inakwenda na kukuta mabomu ni hizi nguvu za mdhibiti, ni jitihada zake maana PAC iko kwenye Baraza na mdhibiti yuko kwenye Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni wizara tofauti hizi. Sisi tuko chini ya Makamo wa Pili wa Rais. Lakini tukiulizwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais lini imeipatia mafunzo kamati hii, nafikiri itakuwa jawabu hamna. Lakini ukitizama kwenye ofisi hii ya mdhibiti, amejitahidi sana, kwa sababu anajua yeye ili kazi yake iwe ya mafanikio ni lazima kamati hii iwe na meno, iwe na uwezo, iwe na upeo. Ndio maana na yeye anafanya wajibu wa kuinoa, kwa hivyo makali haya unavyoyaona Mhe. Naibu Spika, ya kamati yako hii, ni tupa ya mdhibiti katika kuinoa kamati hii ikaweza kufanyakazi zake.

Kwa hivyo, mimi nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana mdhibiti kwa kazi hii na nimuombe aendelee kuinoa Kamati yako hii iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Leo hii mimi nafikiria Waheshimiwa Wajumbe wao wenyewe wanaona maajabu ya kamati hii. Katika bajeti iliyopita watu walikuwa wanaviacha vifungu vinatelezateleza tu, lakini mara hii semina ambazo zimewezeshwa kwa Baraza zima na kwa kamati hii, basi ni matokeo ambayo tunayaona kwamba bajeti sasa inachambuliwa vizuri. Hata wale maofisa wanaoshughulikia bajeti, wao wenyewe wanasema mara hii kama umeteleza basi utakiona.

Ndio maana jana tukaanza kupata marekebisho ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma, ameshagundua kwamba kuna vitu vimeteleza pale, wamefanya marekebisho. Lakini marekebisho haya vile vile mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu huu sijui kama tutakuwa ndio tunakwenda sawa, kwa sababu kitabu hiki kikubwa kilishapita kwenye Kamati ya uongozi kule, kikaridhiwa kwamba haya ndio yaliyokubaliwa. Lakini yanapofanyika katikati kama hivi tukaletewa sijui kama ndio yatakuwa yamefuata utaratibu sawa sawa ama vipi. Hii kama imeanzia kwenye Ofisi ya Rais utumishi wa umma, basi najua na hao wengine wanawezekana wakawa wanafanya marekebisho yakawa yanaletwa kama hivi. Sasa haya yanawezekana yakawa hayakupitiwa na Kamati ya Uongozi. Hilo labda nimi niliache atakapokuja Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma, anaweza kutusaidia zaidi katika kutoa ufafanuzi kwenye haya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 41 kuhusu Chuo cha Utawala wa Umma. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kitabu cha Mhe. Waziri cha mwaka jana alieleza Chuo hichi juu ya suala zima la ujenzi wa chuo hichi, kwamba umeshafikia asilimia 50 kwa kipindi kile cha mwaka 2010/2011, nafikiri ameomba tena fedha kwa ajili ya kuendeleza chuo hichi.

Lakini katika kitabu chake hichi tena cha mwaka huu 2012/2013, nacho pia Chuo kinaonekana bado hakijakamilika na sasa ndio anasema anakamilisha. Sasa mimi nimepata shaka kidogo kwa sababu ya fedha zile ambazo niliziona zimeingizwa katika kipindi kilichopita, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atusadie maelezo juu ya ujenzi mzima wa Chuo hichi.

Kwa mfano, nani mkandarasi pale, ile mikataba au makubaliano yenu kwamba ajenge nusu ndio sasa munatafuta mkandarasi mwengine amalize, yaani aje atusaidie ufafanuzi juu ya matumizi mazima ya fedha zile pale.

Mhe. Naibu Spika, kuanzia walivyoanza mpaka wakakubaliana, na ile hatua iliyofikiwa na sasa wanaomba fedha na kusema wanaanza kufanya utaratibu wa kuweka mkandarasi kwa ajili ya kumalizia pale paliposalia.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa najiuliza yule wa mwanzo walikubaliana ujenzi wa nusu, yaani ajenge tu kwa fedha zile alizonazo na halafu aondeke, nadhani ni vyema Mhe. Waziri wakati atakapokuja atusaidie maelezo kidogo.

Kwa kweli sikuridhika na maelezo ya matumizi ya fedha zile, hivyo nataka ufafanuzi, kwa maana hiyo aje atusaidie ufafanuzi wa kutosha katika hili, na shaka yangu hapa imekuwa kubwa kidogo juu ya matumizi mazima ya fedha hizi za ujenzi wa Chuo hichi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo naomba nimwambie Mhe. Waziri akae vizuri katika kuvipitia vifungu vya matumizi tutakuja kuwa na maswali mengine, kwa sababu haya mabadiliko ambayo yamefanyika kidogo inaonekana kuna sehemu fungu limeondoshwa na kuhamishiwa sehemu nyengine, hivyo tutataka sababu katika haya mabadiliko. Vile vile aangalie vizuri katika yale mabadiliko ambayo yamefanyika na maelezo yake yawe ya kujitosheleza kidogo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nafikiri nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hii. Pia nikushukuru Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa nafasi tunampa Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye ajiandae Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuniwezesha mimi pamoja na Waheshimiwa wengine wa Baraza hili, tukiongozwa na wewe Mhe. Naibu Spika asubuhi ya leo kuendelea na shughuli za Baraza letu tukiwa tunajadili Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii nami nitoe maoni yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nitumie fursa hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa hotuba yake nzuri, safi ambayo imepangika. Jana nilikuwa na dharura na nilitoka kidogo, lakini nilimsikia Mhe. Salmin Awadh Salmin akimpongeza, na mimi nakubaliana na yale aliyoyasema, kwamba hotuba hii imepangika vizuri na hata kitabu chake kimekaa vizuri. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Naibu Spika, hotuba hii imekuja vizuri kwa sababu kumeundwa Wizara hii. Vile vile nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana pamoja na kumshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa hatua yake ya kuunda wizara hii au kuweka sehemu hii katika ofisi yake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa Mjumbe kama mimi ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambapo tuna dhima kama ulivyo wewe Mhe. Naibu Spika ukiwa ni Mwenyekiti wetu, katika suala zima la kufuatilia shughuli za kila siku za wizara hii, na tunaona hali ilivyokuwa na wala si rahisi mtu aliyekuwa nje anayefuatilia kila siku akaiona hali ilivyokuwa na hali ilivyoanza kubadilika tokea kuundwa kwa wizara hii. Kwa hivyo, nataka nimpongeze sana Mhe. Rais kwa hatua yake hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sitaki nipoteze muda wako mwingi sana kwa kutoa ufafanuzi wa pongezi, lakini nataka niyataje maeneo machache, kwa sababu ni vizuri linapofanyika jambo zuri kulipongeza na tusionekane kila wakati tunakosoa tu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri katika maeneo haya. Kwanza wizara hii kwa jinsi inavyosimamia mageuzi katika Utumishi wa Umma (*Public Service Reform*). Lakini katika hili nataka niongezee kwenye hotuba yake pia amegusia katika mwaka huu sasa wanakusudia kufanya usimamizi wa mageuzi katika Serikali za Mitaa (*Local Government Reform*). *(Makofi)*

Sasa hotuba iliyopita ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tulilizungumza hili kwa urefu. Kwa hivyo, jambo la msingi ni kukaa pamoja kwa ajili ya kusaidiana, kwa sababu Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaonekana kidogo wamekuwa wazito.

Lakini kwa sababu Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora wamekuwa wepesi katika kusukuma baadhi ya mambo, basi naomba washirikiane, ili tuone kasi vile vile katika utekelezaji, sasa badala ya kuona maneno kila siku tuone utekelezaji wa mageuzi ya Sekta ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa ile miradi mipya ambayo wameibua waliyoitaja kwenye ukurasa wa 7 wa hotuba yake. Kwa kweli ikiwa miradi hii itasimamiwa na kuweza kupatikana wahisani wa kuweza kuisaidia, basi mimi naamini itatusaidia pakubwa katika kurekebisha mambo katika wizara hii.

Miradi yenyewe ni *Enhancing Democracy, Good Governance and Human Right, Digitalization of Zanzibar Archive, Comprehensive Capacity Building for Government Institutions and Anti Corruption Initiatives*. Mhe. Naibu Spika, miradi hii ukiangalia yote ni miradi muhimu sana kwa maendelo ya sekta hizi zinazosimamiwa na Wizara hii.

Vile vile nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuanzisha mtandao wa wizara kwamba wao wamepewa jukumu la kusimamia *E-Government*, na wameonesha mfano wa kuwa na mtandao wao, *website* hii na watu wakitaka taarifa waweze kuzipata pale.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie pongezi kwa Wizara pia kwa kuchukua hatua sasa za kutekeleza ile Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa mwaka huu kuwa na malengo ya kuianzisha mamlaka hiyo.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika wingi wa pongezi nitakuwa sitendi haki ikiwa sitowapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya tangu kikao hichi kimeanza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wananchi wengi hivi sasa wanatuambia kwamba sasa tunaliona Baraza la Wawakilishi likifanya kazi yake ya kuisimamia serikali. Vile vile wanasema na wala sitaki kumtaja hapa kuna Waziri mmoja juzi ameniambia hapa, Baraza hili sasa ndio linajadili bajeti na hivi ndivyo bajeti inavyojadiliwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nataka niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe, na niwaombe kwamba tuendelee na utaratibu huu, kwa sababu sidhani kama hapa tumekuja kushindana na Waheshimiwa Mawaziri, isipokuwa sote tunasaidiana kwa lengo la kuiendeleza nchi yetu, ili kuona kweli fedha za walipa kodi zinatumika ipasavyo. *(Makofi)*
Baada ya pongezi hizo Mhe. Naibu Spika, kuna mambo naomba Mhe. Waziri atusaidie. Kwanza pamoja na uzuri wa hotuba yake, lakini katika eneo moja kidogo nimeona upungufu, amefanya vizuri katika kutenga fedha ambazo zilizoidhinishwa katika kila Idara na kiasi ambacho kimepatikana katika miezi tisa ya kwanza.

Lakini wenzake walitupa na asilimia ya fedha zile, najua kwamba mwaka haujamalizika, angalau angetupa mwelekeo wa kuona wanaingiziwa kiasi gani na hili linatusaidia sisi kama wasimamizi baadae kujua na kuibana Wizara ya Fedha katika kusimamia fedha ambazo wanaziingiza. Mhe. Naibu Spika, naomba hili kwa miaka ijayo kuanzia mwaka huu ukimaliza tulione.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri fedha amezigawa katika kuomba idhini ya Baraza kati ya fedha za shughuli za kawaida na zile za maendeleo. Katika buku la *estimates* hili la makadirio kwenye Fungu la Maendeleo, utakuta fedha zote zimewekwa chini ya Idara moja tu ya Mipango Sera na Utafiti.

Lakini yeye Mhe. Waziri amezigawa, sasa hii kidogo inanipa mashaka kwamba utaratibu upi ni sahihi, kwa sababu mara nyingi tukiidhinisha inategemewa kila mmoja zikae kwenye Idara yake na haidhuru zinasimamiwa na Wizara moja.

Kwa hivyo, hilo naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja atusaidie kwa nini halikujitokeza hivyo, kwa sababu wao ndio wanaopeleka pale zikawekwa.

Mhe. Naibu Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo katika maeneo yafuatayo. Kwanza haya yanahusu mafungu Mhe. Naibu Spika. Kwanza kwenye Fungu la 11 la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, ukurasa wa 145 wa hili buku kubwa la *Draft Estimates of Recurrent and Capital Revenue and Expenditure for the year 2012/2013*.

Mhe. Naibu Spika, Fungu 221100 Gharama za Mafunzo kwa Ofisi ya *CAG* jumla yake kwa mwaka huu zinaombwa shilingi milioni 313,630,000/= na wala sitaki kupoteza muda kwa kwenda fungu moja moja kwa zile vote ndogo ndogo au *sub votes*. Lakini namuomba Mhe. Waziri akalitizame hili na halafu asaidiwe na watendaji wake, kwa ajili ya kutupatia maelezo, kwa nini kuna fungu kubwa kiasi hichi kwa matumizi haya.

Vile vile kwa nini kuna fedha za mafunzo ya nje shilingi milioni 47,000,000/= na pia kuna malipo ya ada *tuition fees* shilingi milioni 75,000,000/=. Sasa mafunzo ya nje ni yepi na malipo ya ada *tuition fees* ni yepi. Kwa hiyo, naomba hili wakati atakapokuja atusaidie. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo katika bajeti ya Fungu la 47 Kamisheni ya Utumishi, kuna maeneo kidogo yamenipa shida kuyakubali. Kwanza katika Fungu 220300 Gharama za Safari ambazo jumla yake safari za ndani, nje pamoja na gharama za hoteli ni shilingi milioni 95,120,000/= kwa mwaka mmoja. Hivyo na hili naomba wakati atakapokuja anisaidie maelezo kwa nini kuna safari nyingi katika Kamisheni ya Utumishi, ambayo kimsingi kazi zake zaidi ni za ndani.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anisaidie maelezo katika Fungu hili 47 la Kamisheni ya Utumishi katika kifungu au *vote* 220800 kuhusu Matengenezo ya Zana. Kwa kweli hapa kuna ununuzi wa *spares* na zana shilingi milioni 9,100,000/= na halafu kuna matengenezo ya magari shilingi milioni 9,400,000/=.

Sasa kwa uzoefu wangu mdogo tu, mara nyingi *service* ikifanywa inajumuisha na ununuzi wa vifaa, hivyo najiuliza ikiwa ununuzi wa vifaa una *sub vote* yake shilingi milioni 9,100,000/= na yale matengenezo yake tu pia ni shilingi milioni 9,400,000/= pamoja na kumlipa fundi au kuna kitu gani hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba hili Mhe. Waziri wakati atakapokuja basi anisadie.

Lakini nikiondoka katika mafungu hayo sasa niingie kwenye Fungu lenyewe la Wizara 45. Mhe. Naibu Spika, naomba maelezo katika Idara ya Utawala Bora katika ule waraka aliotugaia yeye ambao una marekebisho utakuwa ni ukurasa wa 2 *Vote* 311200 Ununuzi wa Mashine na Zana. Kwa mfano, kuna ununuzi wa friji pale shilingi milioni 10,000,000/= nilikuwa naomba hili anisaidie kwamba friji hili la shilingi milioni 10,000,000/= ni la aina gani.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba maelezo katika Fungu la Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi, *Vote* yake na hapa ninalo swali tu. Katika *Vote* 220400 Gharama za Mafuta na Vilainisho na wengine wote gharama za mafuta zinaongezeka, na huwa tunaambiwa kwamba sababu ya kuongezeka kule ni kupanda kwa bei ya mafuta.

Sasa hapa kidogo kuna maajabu, kwa sababu tulitegemea kama *trend* ndio hiyo basi iwe kwa Wizara pamoja na Idara zote. Lakini katika Idara hii kwenye gharama za *petrol* mwaka jana ilikuwa shilingi 610,000/= na mwaka huu 480,000/=. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kama utaratibu ndio huu basi kwa nini wizara nyengine zisije kujifunza hapa, ili tukaweza kupunguza gharama badala ya kuongeza gharama.
Mhe. Naibu Spika, naomba nisaidiwe kwamba kwa nini zinashuka, ili nipate uhalali na niamini kule kunakoongezwa kunakuwa na uhalali wa kuongezwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anisaidie maelezo katika Ofisi Kuu Pemba kwenye ukurasa wa 4 na 5 kuhusu maelezo yafuatayo. Kwanza kwenye *vote* 220200 Viburudishaji, imetoka mwaka jana shilingi milioni 3,900,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 26,645,000/= wakati huku mafungu haya kama ni ya *training* Idara inazosimamia tayari zinazo mafungu haya. Sasa kwa Ofisi Kuu Pemba peke yake kuna ongezeko hili kubwa sana.

Lakini jengine kama nilivyoeleza kule ukija kwenye Gharama za Mafuta na Vilainisho kwa Pemba hakujaongezeka sana mwaka jana na mwaka huu, na hili ni Fungu 220400, mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 5,570,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 5,556,000/= kwenye *petrol* na kwenye *diesel* mwaka jana shilingi milioni 5,000,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 5,280,000/=.

Sasa nikawa najiuliza hapa mafuta huku Pemba hayakupanda au ndio kama kawaida ya ofisi zetu nyingi kwamba kwa Pemba wanakuwa wanawekwa mkiani na wao hawapati manufaa ambayo ofisi nyengine inakuwa zinazo. Kwa kweli hiyo inaonekana katika fungu zima hilo Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Jengine ni katika vifaa na huduma katika Ofisi za Pemba, kwenye *stationary vote* 220501 fungu limepanda kutoka shilingi milioni 6,156,000/= mwaka jana hadi shilingi milioni 21,340,000/= mwaka huu linaloombewa. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja anipatie maelezo.

Vile vile niombe maelezo kwa ada ya ushauri ambayo imewekwa shilingi milioni 2,600,000/=. Mhe. Naibu Spika, ninavyofahamu mimi kwamba Ofisi ya Pemba inaratibu tu shughuli na mambo mengi haya yanayohusu kama vile mambo ya *consultant fees* yatakuwa yanafanywa kupitia ofisi zao zilizokuweko Unguja. Sasa fungu hili la shilingi milioni 2,600,000/= lilioko Pemba linashughulikia kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na Ofisi Kuu Pemba katika fungu lilioko kwenye ukurasa wa 6 kuhusu Ununuzi wa Mashine na Zana Fungu 311200 *vote* hiyo Mhe. Naibu Spika, katika *sub vote* ya ununuzi wa *computer* ambayo ni 311205 kumewekwa shilingi milioni 30,000,000/=. Kwa hivyo, hapa nataka kujua ni *computer* ngapi ambazo zimekusudiwa kununuliwa kwa ajili ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti ukurasa wa 7 wa waraka aliotupa Mhe. Waziri wa marekebisho kwenye vote 220100 Gharama za Vifaa na Huduma za Mawasiliano, kwenye Huduma za Mtandao wa Serikali *E-Government* kuna shilingi milioni 33,978,000/=. Kwa hivyo, hapa nataka kujua hizi zina shughuli gani, kwa sababu mwaka jana tuliidhinisha hapa shilingi bilioni 18 kwa ajili ya mradi huu, sasa mwaka huu ndio kwanza unaanza hizi shilingi milioni 33 za kazi gani? *(Makofi)*

Sasa naomba niende katika Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu ukurasa wa 11 wa marekebisho aliyotupa Mhe. Waziri *vote* 311200 kuna Ununuzi wa Television shilingi milioni 28,000,000/=. Hapa nilikuwa naomba nisaidiwe hii *television* ya shilingi milioni 28,000,000/= vipi na kama ni zaidi ya moja katika ofisi hii ya Nyumba ya Nyaraka kunahitajika *television* ngapi katika eneo lile hata iwe kuna fedha kubwa sana ambazo zimetajwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niende katika Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, idara hii iko kwenye ukurasa wa 17, kwa maana ya *Department of Administration and Human Resource* kwenye ukurasa wa 17 na 18 naomba nipatiwe maelezo. Kwanza Mhe. Naibu Spika, ni kwenye *vote* 220500 tena Vifaa na Huduma za Ofisi, kuna vifaa vidogo *sundry items*, na imetoka bajeti ya mwaka jana shilingi milioni 6,750,000/= na mwaka huu shilingi milioni 19,200,000/=.

Mhe. Naibu Spika, najiuliza *sundry items* gani hizi ambazo zina-*cost* kiwango kikubwa na hili limenipa mashaka, kwa sababu kabla ya kurekebishwa katika hili buku ambalo tulilonalo kabla ukiangalia ukurasa wa 662 Mhe. Naibu Spika Fungu la *Sundry Items* lilikuwa lina shilingi milioni 8,400,000/=, sasa katika marekebisho haya limeongezeka mpaka kufikia shilingi milioni 19,200,000/=. Kwa hivyo, najiuliza Mhe. Naibu Spika, kwamba kuna *sundry items* gani za gharama kiasi hicho.

Lakini fungu lililoniacha hoi katika Idara hii ya Utumishi liko kwenye ukurasa wa 18 *vote* 281400 Gharama za Kukodishwa, kuna gharama za ukodishwaji wa kumbi za mikutano mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 1,000,000/= na mwaka huu zimeombwa shilingi milioni 186,872,000/=.

Mhe. Naibu Spika, najiuliza he! Kuna shughuli gani, kwa sababu kama ni suala la semina na mafunzo ambazo ndio shughuli kubwa kwa wizara hii kwa ujumla, basi kila idara inalo fungu lake na fungu hilo linahusu gharama za ukodishwaji ukumbi unalikuta katika kila idara.

Sasa vipi katika idara hii ambayo inashughulikia *Administration* ya wizara pale kuna shilingi milioni 186,872,000/= kwa gharama za kukodi kumbi. Kwa hivyo, hili naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo kwa undani kabisa.

Mwisho kabisa katika vifungu na sio katika mchango wangu iko ukurasa wa 19, na hii nina maoni tofauti. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Mhe. Naibu Spika, mimi nimeipongeza Wizara kwa kuja na utekelezaji wa

kuanzisha taasisi hii, lakini nikiangalia bajeti yake ambayo kidogo imeongezwa na tofauti ilivyokuwa mwanzo ukitizama yale marekebisho yalivyokuwa.

Lakini hata marekebisho haya yananipa wasi wasi Mhe. Naibu Spika, tunapotaka kuunda Taasisi muhimu kama hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ituchunguze sote pamoja na sisi tuliomo katika Baraza hili la Wawakilishi. *(Makofi)*

Sasa Fungu la Mishahara ni shilingi milioni 8,988,000/=. Kwa hivyo, hivi tunataka kuwalipa mshahara wa kima kiasi gani Mhe. Naibu Spika hata waweze kuwa hawatovutika na vishawishi vya rushwa, mbona fungu hili ni dogo na hapo nilikuwa nikijiuliza.

Vile vile hata ukiangalia Fungu zima la Mafunzo, na wala sitaki kupoteza muda kwa jumla niseme tu fungu hili kwa ujumla wake ukilitizama, ambalo lina shilingi milioni 2,021,291,000/= mimi naona ni fungu dogo na pengine haya ambayo tumesema huku yamekaa siko yalipaswa yaongezewe ofisi hii, ili iweze kufanya kazi zake vizuri iliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba katika mafungu hayo Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maelezo ya kina, ili turidhike kwamba fedha za walipa kodi zitakwenda kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwenye mafungu naomba niende kwenye maudhui ya hotuba. Kwa kweli kuna maoni mengine tumetoa kupitia katika Hotuba ya Kamati, lakini nilikuwa naomba kuna maeneo machache niyazungumze.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, ni eneo linalohusu Utumishi wa Umma katika Taasisi za Muungano, ambalo Mhe. Waziri amelitaja katika hotuba yake ukurasa wa 49, na amesema wamekubaliana katika *formula* ile, kwamba Zanzibar itapata asilimia 21 na Tanganyika itapata asilimia 79 mgao wa Utumishi wa Umma.

Je, *formula* hii itaanza kutumika kwa ajira zinazoanza sasa au tutakwenda kuziangalia Taasisi zote za Serikali ya Muungano tujirekebishe na tuone *formula* hii inafuatwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba sana na zote kwa sababu Taasisi za Muungano ni nyingi kuna Jeshi la Polisi, Jeshi (JWTZ), Usalama wa Taifa, *TRA*, *BOT* na *BOT* tuligaiwa buku hapa Mhe. Naibu Spika na ikafika Wizara ya Fedha, basi ukilitizama muundo wake ule unatisha, yaani hakuna Mzanzibari zaidi ya Naibu *Governor* na wala hakuna mwengine katika *management*.

Vile vile kuna Taasisi kama Mamlaka ya Mawasiliano, Kampuni ya Simu na mengi sitaki kuyamaliza Mhe. Naibu Spika, kwa sababu nikitaja siyamalizi. Kwa hivyo, nasema je *formula* hii itaanza kurudi nyuma kwenda kuangalia hali ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu yeye Mhe. Waziri ndiye anayesimamia Utumishi wa Umma, na pia ndiye mwenye kuratibu Utumishi wa Umma wa Muungano, basi anisaidie. Kwa kweli ziko taarifa kwamba katika Kikosi cha JWTZ kilichopo Zanzibar kumekuwa na utaratibu kuwa askari wenye asili ya Kizanzibari mara zote hawazidi asilimia 7.

Kwa hivyo, nataka kujua *formula* hii imekubaliwa baina ya serikali mbili, kwamba vikosi vya Jeshi vinavyokuweko Zanzibar visiwe na *majority* ya wazanzibari kwa upande wa Zanzibar kuna kitu gani hapa. Mhe. Naibu Spika naomba hili atakapokuja Mhe. Waziri anisaidie, kwa sababu katika vikosi vyengine kama vile Polisi tunaona kwamba wazanzibari wengi ndio waliokuwepo katika jeshi la Polisi wanaotumika Zanzibar, kwa sababu ni taasisi ya Muungano wapo wanaotoka upande wa pili, na wala hatulipingi na hata kama lingekuwa katika jeshi nisingelipinga, lakini tunaelezwa kwamba kuna hilo suala.

Kwa hiyo naomba watusaidie, ili tuone kama ilivyokuwa katika taasisi nyengine kwa mfano, Idara ya Usalama tunawaona wazanzibari hapa, sasa kwa nini katika hili kuna hali tofauti.

Jengine naomba niende katika ukurasa wa 44 wa hotuba yake Mhe. Waziri, ambapo amezungumzia kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, kamati yetu utakumbuka ilipata nafasi ya kuitembelea.

Lakini kusema kweli ukitizama Tume hii unaikuta kwamba inashindwa hata kufanya kazi zake ipasavyo kwa upande wa Zanzibar kwa sababu ya ufinyu wa bajeti inayopewa.

Sasa nilikuwa najiuliza Mhe. Naibu Spika, kwamba chombo hichi si cha Muungano na tumekitungia Sheria katika Baraza la Wawakilishi, ili kukipa uhalali kifanye kazi Zanzibar. Lakini ikiwa halafu hakipewi bajeti kuweza kufanya kazi yake, sasa faida ya kukipa uhalali wa kufanya kazi hapa Zanzibar iko wapi Mhe. Naibu Spika?

Kutokana na hali hiyo, mimi napendekeza kwa sababu hivi sasa katika wizara hii kuna Idara ya Utawala Bora na pia tumeunda hii Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Kwa nini ipewe bajeti ndogo Tume hii ishindwe kufanya kazi zake Zanzibar na tusiiongezee na kuibadilisha Idara ya Utawala Bora na tukawa na Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu kwa Zanzibar, kwa sababu suala hili si la Muungano na ikawa tunajisimamia wenyewe kuzichunguza ofisi zetu na kuwapa nafasi wananchi ambapo wanaweza kutoa malalamiko yao yakashughulikiwa. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anisadie.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nataka nichangie ni suala hili la Taasisi mpya iliyoundwa ya *E-Government*. Katika maoni yetu ya kamati Mhe. Naibu Spika, tumetaka maelezo na tumesema kwamba tumetembelea na tumeona ofisi nzuri, mashine za kisasa, lakini bado tuna wasi wasi kwamba ile mitambo na muundo wake wote uliokuwepo pale kuwa unafikia thamani ulioombewa mwaka jana hapa ya shilingi takriban bilioni 18.

Sasa Mhe. Naibu Spika, sisi kama kamati tuliomba kwamba tupewe *break down* ya matumizi yote ya *E-Government* tangu ilipoanza mpaka ilipofika pale, na wale waliotusimamia pale na tulishangaa, kwa sababu waliokuwa wakitusimamia pale alikuwa ni Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa kweli mwaka jana nilihoji hapa kwamba hii mwenyewe nani? mbona kila mtu anaing'ang'ania kuna nini hapa, kuna shira hapa watu wanataka kuramba.

Mhe. Naibu Spika, tulipata wasi wasi zaidi pale tulipoomba *break down* ile hatukupewa, na tuliambiwa tuiombe Wizara ya Fedha na kamati imeandika Wizara ya Fedha na wala hatukupewa takriban ni miezi miwili na mpaka tumeingia katika kazi za bajeti.

Mhe. Naibu Spika, naomba tuambiwe hapa kuna nini na tunaomba *break down*. Kwa maana hiyo, Mhe. Naibu Spika, nafikiri tutafika pahala tutaomba *Special Audit* ya mradi huu kupitia *CAG* na *PAC* ya Baraza la Wawakilishi zikachunguze hasa fedha hizi zimetumika kweli? Kwa sababu kuna *serious doubt* juu ya mradi huu Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba Mhe. Waziri alitizame ni suala la posho na Mhe. Mgeni Hassan Juma amechangia vizuri sana hapa na wala sitaki kurejea maelezo yake. Lakini mimi naomba pia kuna eneo jengine mbali alilolisema yeye, kwamba kwa nini kumekuwa mazoea ya kujengeka posho za vikao na kamati ambayo inakuwa fungu kubwa sana na zinatumika fedha za walipa kodi.

Hata hivyo, kwenye mashirika Mhe. Naibu Spika, hatujazungumza, mashirika kwa sababu ni taasisi zinazojitegemea, basi kumejengwa utamaduni wa kila mmoja anajipangia posho anavyotaka yeye.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisadie kwamba hawaoni kwamba umefika wakati kuna haja ya kutoa muongozo unaoweka posho na malipo mengine katika mashirika haya, na ikawa zinafanana kwa mashirika yote, kwa sababu haya ni Mashirika ya Serikali kwa nini yasifanye hivi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kwenye dakika zako bado dakika tano kutimiza nusu saa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba Mhe. Waziri alitizame ni suala la posho. Mhe. Mgeni kachangia vizuri sana hapa sitaki kurudia maelezo yake. Lakini mimi naomba kwa vile alivyosema yeye kwamba kwa nini kumekuwa mazoea posho za vikao na kamati ambayo inakuwa fungu kubwa sana linalotumika fedha za walipa kodi.

Lakini si hapo tu, kwenye mashirika Mheshimiwa kwa sababu ni taasisi zinazojitegemea kumejengwa utamaduni kwamba kila mmoja anajipangia posho anavyotaka yeye. Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo anisaidie. Haoni kama

imefika wakati kwamba kuna haja ya kutoa muongozo unaoweka posho na malipo mengine katika mashirika haya ikawa zinafanana kwa mashirika yote, kwa sababu haya ni mashirika ya serikali. Kwa nini wasifanye hivyo.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine haraka haraka naomba nipatiwe maelezo ni katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Hii ndio Kamisheni inayozisimamia zile Tume za Utumishi nyengine zote katika sekta mbali mbali. Nilikuwa naomba nini mahusiano ya Kamisheni hii na Tume ya Utumishi Idara Maalum. Kwa sababu watu wa Idara maalum wana malalamiko yao mengi, lakini hawana pa kukimbilia. Sasa nikauliza hii ni kwa sababu ya nidhamu za kijeshi haiingii kule.

Hapo hapo nilikuwa naomba vile vile anisaidie katika Sheria ya Utumishi wa Umma tumepitisha hapa, tumeweka mamlaka za nidhamu katika mambo mbali mbali. Nataka kujua je, mfanyakazi wa Idara maalum askari anapokuwa anachukuliwa hatua katika kukata rufaa anaweza mwisho kuifikia Kamisheni ya Utumishi wa Umma au yeye kwa sababu ya nidhamu za kijeshi ndio anaishia kule kule katika utaratibu wao. Nilikuwa naomba hilo nipatiwe maelezo.

Mhe. Naibu Spika, niungane na aliyezungumza kuhusu Idara ya Utawala Bora. Hii Idara inapaswa ibadilike sasa. Hii si Idara ya Utawala Bora ya Wizara ya Utumishi wa Umma. Imepewa mamlaka ya kutambaa na kuenea kote (*Cross cutting).* Mimi maneno mengine niliyokuwa siyajui maana yake au siyapendi sitoyatumia, nitatumia *cross cutting*, linasema imejieneza na inapaswa iingie kila pahala. Nafikiri Kiswahili hichi kitafahamika zaidi kuliko haya maneno sijui 'Mtambuka' miye wala siyajui maana yake.

Nilikuwa nataka kujua imefanya kazi gani katika kusimamia Wizara kwa jumla. Katika haya Mhe. Naibu Spika, yapo malalamiko ya wananchi, mbali ya haki za binaadamu lakini ndani ya serikali yenyewe. Kwa mfano fedha za walipa kodi, unakuta magari ya serikali yanatembea mpaka saa 6 za usiku. Lakini tokea malalamiko ya wananchi kwamba magari, mengi ya wakubwa ambao tayari wana fungu lao la posho la mafuta. Lakini posho la mafuta anachukua mbali mfukoni halafu anakwenda kuchukua pesa za Idara au Wizara anataka atiliwe mafuta katika gari yake anayochumia kwa shughuli zake binafsi. Idara ya utawala Bora inafanya kazi gani katika suala hili.

Hilo Mhe. Naibu Spika, linasaidia kuongezeka kwa matumizi lakini pia kuyachakaza hayo magari yenyewe ambayo mwisho inakuwa ni mzigo kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mazungumzia matatu ya mwisho madogo madogo tu. Moja ni sare. Naipongeza kwamba Ofisi nyingi sasa hivi zina bajeti za sare. Nilikuwa naomba Wizara hili walisimamie. Ukienda katika Ofisi zetu ile sura ya kwamba unakwenda katika pahala pa Utumishi wa Umma haipo. Pahala pakiwa pana sare panapendeza. Tumezikuta Ofisi chache ambazo zinazo sare, zimefutiwa nafikiri hili walisimamie.

Jengine kuna wafanyakazi kama walivyosema wengi, sitaki kulirejea limeshasemwa na wengi ambao sio wenye utaalamu, hawana vyeti lakini wanafanya kazi ngumu na muhimu vile vile, katika yale masuala ya maslahi na nyongeza kwa mshahara na wamewafikiria kiasi gani, kuna madereva, wanakwenda katika shughuli madereva hawa wa viongozi wanashiriki katika mikutano na semina na wengine hata posho hawapewi. Tukila chakula wananyanyaswa wao hawakipati. Kwa nini wasihudumiwe vile vile watu kama hawa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu nafasi mpya za ajira. Hili Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nitoe indhari na nimuombe na Waziri akija anisaidie. Mhe. Naibu Spika, Waziri katwambia kwamba nafasi zilizokuwa zimeombwa ziidhinishwe zilikuwa ni 6817, wao wakaidhinisha 3356, lakini hatimaye zilizokubaliwa ni 2552. Mhe. Naibu Spika, tunajiuliza hata kwa hicho kiwango kidogo kilichokubaliwa 2552 tukiwa tunakwenda kwa wastani huu wa kila mwaka, hii *system* ya utumishi wa umma tutaweza kuihudumia hatimaye?

Hivi sasa tunaambiwa takriban tuna watumishi wa umma wasiopungua au wanaokaribia 39,000 Zanzibar. Sasa nasema kama hatukuzi sekta binafsi tukategemea kama kila siku tutaajiri watu katika Sekta ya Utumishi wa Umma kwa nchi ambayo ina watu ambao milioni moja na laki mbili, kiwango cha uwiano wa wafanyakazi na wanaohudumiwa ni kikubwa sana.
Nilikuwa naomba Mheshimiwa anisaidie katika hili, haoni kwamba tukiendelea kuajiri kwa mtindo huu tutafika pahala tutakwama. Kwa sababu idadi ya wanaoajiriwa na wanaostaafu hailingani. Kwa hiyo naomba maelezo katika hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme naiunga mkono hoja, lakini nitaomba ufafanuzi huu ni kuwepo na nimpongeze tena Mhe. Waziri na nimtakie kila la kheri na watendaji wake wote katika kufanikisha majukumu yao. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hotuba hii ya makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, nikupongeze kwa kukaa kwenye kiti chako hicho. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii aliyoisoma mbele yetu kwa ufasaha na vile vile niwapongeze watendaji wake kwa kumsaidia katika majukumu yake haya.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwenda na Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti.Kwa kweli idara hii ina majukumu mengi na ya msingi kabisa. Nimwambie Mhe. Waziri haya ni majukumu na ameomba pesa hizi na sisi kama Wawakilishi wa wananchi, na kwa sababu tunataka mafanikio ya nchi yetu basi ni kutizama bajeti hii na kuipitisha. Lakini likishakutoka hilo jukumu kwao kuyatimiza yale yote ambayo wameyataka na wameyaomba katika bajeti hii utekelezaji wake uwe na ufanisi. Sababu ikishakutoka kwetu sisi, sasa kuna mambo mengi ambayo wao itabidi wayatizame kwa upeo wake, na hasa kwamba hizi ni fedha za Umma na zinahitaji kutumiwa zile taratibu na sheria za fedha za Umma.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa Nam. 9 kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Tumeona kwamba Idara hii ina jukumu la kutoa huduma za utumishi na uendeshaji katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, zikiwemo ajira na maendeleo ya watumishi na kufanya takwimu za watumishi.

Idara hii majukumu yake ni hayo. Vile vile niseme kwenye idara hii kuna majukumu vile vile ya kujua maslahi ya wafanyakazi. Kwa kweli nimetizama maeneo mbali mbali ya kwenye buku hili la bajeti katika maslahi ya wafanyakazi bado ni madogo. Pia baada ya mtu kufanya kazi anatakiwa apumzike kwa kupata likizo ili aende aka *fresh* huko na baadaye arudi tena kuja kufanya kazi. Nikitizama katika buku hili la bajeti sijaona kuhusiana na hilo. Idara nyingi hazina fedha za likizo na pale ilipowekwa basi ni kidogo sana. Nimeona pahala kama Pemba nimetizama kuna fedha za likizo ni laki tatu. Mhe. Waziri akija labda aniambie kupitia huu *MTEF (Medium Term Expenditure Framework)* anambie laki tatu hizi zimegaiwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, nikienda ukurasa wa 12 kuna Idara ya Mafunzo na Maendeleo. Idara hii wenzangu wengi walilalamikia wafanyakazi wanaokwenda kusoma na baadae hawarudi. Naomba nitoe rai labda tufanye sheria ambayo tutasema ni *international*. Pale tutakapowachukua wafanyakazi wetu na tukawapa mafunzo na kwa bahati mbaya wakenda sehemu nyengine kufanya kazi basi ni lazima kuwe na fidia kwa yule aliyemchukua mtu yule, kuwe na vipingamizi ambavyo vitakuwepo kwenye sheria kwamba watu wale ni lazima yule aliyemchukua mfanyakazi yule kumtumia basi alipe fidia. Mhe. Waziri nikupongeze sana kwa majukumu ambayo unayoyatekeleza.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara yenyewe ya Utawala Bora. Kwa kweli hii Idara ina majukumu mengi, hasa tukitizama kwamba Utawala Bora wenyewe ni nyanja pana ambayo ina misingi yake ya Utawala Bora, ikiwemo *transparency* na *accountability*. Haya ni lazima kama Wizara nayo ina majukumu ya kuhakikisha yote haya uwazi unakuwepo na uwajibikaji wa kila sehemu.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa wa 26 ambao iko Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za Taifa. Ukweli kwamba Idara hii ina majukumu ya kuhifadhi nyaraka mbali mbali za taifa na mpaka kimataifa kwa taarifa nilizozipata pale zipo. Huja watu mbali mbali na kutoka nchi mbali mbali kuja kuzitafuta nyaraka za nchi mbali mbali. Ningeiomba Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla kwamba Idara hii itizame yale mafungu yake ambayo yameomba pesa iweze kuwatilia mia kwa mia kwani tumeona umuhimu wa nyaraka hizi.

Mhe. Naibu Spika, niende ukurasa nam. 33 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli na mimi niseme nampongeza mwana mama huyu kwa umahiri wake, kwa utekelezaji wake na anaifata ile misingi ya Utawala Bora. Ni mtu ambaye hana choyo, hana ubaguzi wa kijinsia wala wa aina yoyote. Anafanya kazi zake vizuri kwa ufanisi na kwa lengo lile lile la kuipenda serikali yake na kuitumikia.

Mhe. Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sisi kama Kamati ya PAC na mimi ninajinasib ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya PAC ambapo kila alipopata nafasi, basi ametuwezesha kwa ripoti

zile tunazozileta hapa ni kwa sababu ya kutuwezesha yeye. Tunakwenda sehemu mbali mbali kwenda kubadilishana mawazo na wenzetu wa PAC za nje. Ingawaje bado kuna matatizo ya hapa na pale ambayo bado hayajatambulika na hili mimi ndilo linalonitia mashaka.

Baraza la Wawakilishi pamoja na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini bado nikitizama sio *age* yetu kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu bado hajawa na uwezo wa kutambulikana. Kama yeye hatambulikani hata na sisi kama Kamati ya PAC tutakuwa hatuna uwezo wa kwenda Mataifa mbali mbali na kujitangaza. Lakini kwa ukakamavu wake anafanya jitihada mbali mbali, tumeweza kwenda kwenye PAC za *West Africa* ambazo ni WAPA. Tulikwenda PAC za SADCOPAC ambazo tumekwenda kubadilisha uzoefu mbali mbali wa kazi.

Niseme asionekane hatuwezeshi Kamati PAC. Kamati ya PAC kwenye Kanuni yetu ya Baraza la Wawakilishi imo. Kwa maana hiyo ndio anatuwezesha na anataka tujue kila kitu, kwa hivyo anatuwezesha kila anapopata nafasi ile. Hiyo niseme kwamba ndio misingi hasa ile ya Utawala Bora hafanyi kwa kujifichaficha, yeye anatupa sisi uwezo ili tuweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hichi kimekusanya mambo mengi. Sisi kama ni Wawakilishi wa wananchi niseme kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana hapa asubuhi hii. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia hii nafasi. Pia nichukue tena fursa hii kumshukuru Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri, hotuba yao nzuri ambayo wametuletea mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kusema msemo ufuatao ‘polepole ndio mwendo na mwenda pole hajikwai na akijikwaa huwa haanguki’. Haya Mhe. Naibu Spika, nayasema kutokana na upya wa hii Wizara ni mpya na ina majukumu mengi kabisa. Lakini kutokana na umahiri wa Mhe. Waziri na watendaji wake bado tunakwenda na hatuanguki na inshallah Mwenyezi Mungu atatufikisha pazuri.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze mchango wangu kwa kuzungumzia suala zima la rushwa ambalo limeelezwa katika kitabu hiki ambacho kitengo hichi kinakusudiwa kuanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa tunaambiwa tayari sheria hii tuliyoipitisha hapa na Mhe. Waziri ameshaisaini. Nilikuwa namuuliza tu Mhe. Waziri je, imeshaanza kutumika au inaanza lini kutumika kwa sababu ili tuwe na huo Utawala Bora basi ni lazima sheria hii ifanye kazi ipasavyo. Kukosekana kwa matumizi ya sheria hii basi ile dhana nzima ya Utawala Bora itakosekana. Hapa kuna kitabu cha Sera ambacho wametuletea nacho kina mpango mzuri iwapo kweli tutautumia na kuufata basi naamini tutaweza kufika mahali pazuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende katika ukurasa wa 47 hapa napenda niipongeze Wizara pale waliposema watahakikisha utaalamu uliokosekana na kusababisha kuajiriwa wageni unarithiwa na wataalamu wenyeji. Hatua hii naipongeza na nasema hatua hii ni nzuri na imetuonesha moyo, na tujitahidi ili tuweze kujinasua kutokana na wataalamu hawa wa kigeni ili tuweze kujitegemea na sisi wenyewe katika fani ya utaalamu huo.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu hautokuwa mkubwa lakini niende katika ukurasa 41 hapa kuna Chuo cha Utawala wa Umma. Wenzangu wamezungumzia sana juu ya Chuo hichi lakini mimi nilitaka kuzungumzia kuwaomba Wizara zote ambazo zimo humu ndani Mawaziri wake wapo. Hapa nilitaka kuziomba Wizara kuhusu kuwalipia wale wafanyakazi ambao tunawapeleka katika Chuo hiki cha Utawala wa Umma; ili Wizara ipate manufaa ya kuweza kuwa na wafanyakazi walioongezewa uwezo. Lakini pia na hichi Chuo nacho kiweze kupata mafanikio kuweza kujikimu katika elimu hiyo ambayo wanaitoa.

Mhe. Naibu Spika, pale tutakapokuwa hatulipii wafanyakazi wetu na hichi Chuo kinakwenda kutokana na ruzuku na hakina bajeti, Chuo hichi mwisho wake kitashindwa kujiendesha.
Mhe. Naibu Spika, ombi langu lilikuwa hilo katika Chuo chetu cha Utawala wa Umma. Lakini pia niende katika Idara hii muhimu ya nyaraka. Idara hii kweli ni muhimu, inahifadhi nyaraka za Taifa na za Kimataifa, nimuombe Mhe. Waziri kuwa makini katika kuona Wizara hii inapatiwa vile vifaa vinavyohitajika ili kazi yake pale iweze kuendelea.

Pia kutokana na kuonekana kuwa kumbukumbu zipo kila sehemu na wataalamu hawa anao yeye katika wizara yake. Nimuombe wataalamu hawa aweze kuwapeleka katika Wizara ili kuweza kuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhiwa kumbukumbu na zisiwe zinatupwa ovyo ovyo na hatimaye kunakosekana kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda mchango wangu tena niungane na Mhe. Mshimba pale jana alipowasemea madereva. Madereva wa viongozi kweli tuwaonee huruma ipasavyo. Wenzetu hawa wana majukumu makubwa na muda wao mwingi wanaupoteza wakiwa wamekaa wanasubiri viongozi wao watoke katika majukumu yao. Lakini bado hatujatilia maanani kuona wenzetu hawa wana kazi kubwa.

Mhe. Naibu Spika, niseme wenzetu hawa hawana kazi mbadala, akitoka asubuhi, atashinda hapo nje, hana kazi nyengine anayoifanya mpaka muda wa kazi hapa uishe aondoke na bosi wake na hatimaye jua limetua hawezi kujiingizia kipato kwa kazi nyengine.

Nimuombe Waziri kweli hawa madereva kuwaona wanaongezewa mshahara au maposho wanayoyapata wenzao na wao waweze kupewa maposho hayo. Madereva hawa pia ningependa niseme kwamba hata zile siku ambazo tunawatumia kwa Semina. Madereva hawa wanakuwa hawamo katika yale maposho kuweza kuona siku ile wao sio siku ya kazi lakini pia tumeweza kuwaleta pale kwa ajili ya kutuhudumia sisi, lakini utakuta tunawaacha hata lile posho dogo tunashindwa kuwajaalia. Nasema hilo kwa sababu kuna mfano ambao wametuonesha wenzetu wanaotoka Tanzania Bara.

Wenzetu wanapokuja hapa na semina zao wanawajali sana madereva na wanaingiza katika maposho. Hawa na wao ni watendaji kama watu wengine ni lazima na wao tuwafikirie, tuwajali na hata inapokuwa tuna semina zetu basi na wao tuwajali hata kwa kile chakula kinachokuwepo pale na wao tuwafikirie. Tunawaacha pale na njaa wao wapo nje, sisi tumo ndani, tukitoka pale unategemea dereva huyo huyo mwenye njaa aweze kukuendesha wewe. Hapo tunahatarisha hata ule usalama wetu. Nawaombea sana madereva tuwashughulikie ipasavyo, dereva hana Sikukuu, hata siku ya Sikukuu unaweza ukampangia awapeleke watoto Kariakoo. Mheshimiwa tuwajali sana hawa ni wenzetu.
Mhe. Naibu Spika, nimetaka nichangie kifungu kile cha mikataba kwa wafanyakazi wastaafu. Mhe. Naibu Spika, wenzetu wale wanaostaafu na wanakuwa wengine ni wataalamu, ndio inabidi saa nyengine wapewe mikataba hii ili inapoonekana amekosekana mtu wa kushika nafasi yake basi ndio maana tunamuweka yeye aendelee ili huku tukijiandaa.

Mhe. Naibu Spika, ni kwa nini mtu yule yupo Wizarani miaka yote anashindwa kupata mtu muandamizi ambaye anaweza akafatilia ujuzi ule baadaye anapostaafu mtu yule pakawa tayari tumemuandaa mtu mwengine. Kuendelea kuwaajiri wastaafu maana yake tunazuia wafanyakazi, vijana wetu wapo nje na wameshasoma na sifa wanazo lakini wanashindwa. Au hao walikwisha soma wasomi wetu huko nje wanasubiri, basi mtu si vibaya kuweza kumwita akajifunza ile kazi kama wanavyotumia wenzetu wa Mahakama.

Mahakama mwanafunzi akishakusoma sheria tu, unamuona anakwenda ku – *act* katika Mahakama mpaka muda unafika au anaajiriwa pale au anaajiriwa sehemu nyengine, lakini ule ujuzi anakuwa tayari ameshautumia.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu haukuwa mkubwa sana, lakini naweza nikapata dhambi kama sikumtaja humu mama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Wenzangu wengi waliotangulia wamesema kwamba mama huyu ni mahiri na anajitahidi kwa kazi. Mimi nasema hili naungana nao mkono kwa asilimia mia moja. Huyu mama anajitahidi na kweli anafanya kazi kwa kujituma na kwa ujuzi hasa ambao Mwenyezi Mungu kamjaalia.

Mimi nina wasi wasi kama huyu mama hatumtishi katika huo utendaji wake wa kazi. Kwa sababu ya kumuona pengine mwanamke ndio labda tunamtishiatishia. Ripoti anazitoa lakini kwa nini hatuzifanyii kazi. Anapoona ripoti hazifanyiwi kazi na yeye huwa anavunjika moyo kusema kweli kwa kutekeleza yale yanayomuhusu. Anaweza pengine akaona labda nilivyofanya sivyo na hali kumbe amekwenda vizuri tu. Huyu mama tumsaidie kwa hali yoyote ili aweze kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sikuwa na mengi, nilitaka tu niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia mawili matatu katika bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi sina mengi sana isipokuwa ni machache mno ambayo nimeomba kutaka kuchangia katika bajeti hii. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na timu yake yote ya wataalamu kwa kufanya kazi nzito sana ambayo tayari imewasilishwa hapa mbele yetu.

Mimi nilikuwa naomba kupata maelezo kidogo kutoka ukurasa nam. 646 mpaka 647 katika *vote* tofauti hapo. Lakini yale maeneo ambayo yatakuwa yanagusia ongezeko la matumizi kwa zaidi ya asilimia 300. Mhe. Waziri atakapokuja hapa ilikuwa tunaomba kupata maelekezo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tokea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipopandisha mishahara hadi hii leo ni kipindi cha mwaka mzima tayari. Haidhuru kwamba malipo yale ya mshahara yalipaswa kuanza kutumika katika mezi wa Oktoba, lakini jambo la kusikitisha sana kuona kwamba hadi hii leo kuna maeneo mengi bado kuna matatizo ya hapa na pale.
Labda tumuombe tu Mhe. Waziri atakapokuja hapa, kwa sababu mwaka mmoja tayari umepita na zoezi hili bado halijakamilika. Kuna *scheme of service* chungu nzima bado hazijalipwa, kuna maposho ya wafanyakazi chungu nzima bado hayajakaa sawa. Ni lini hasa taratibu hizi zitakuwa zimekamilika ili huu usumbufu ambao unaendelea na kesi za kila siku zinazokuja kwetu ziwe zimemalizika. Hilo nilitaka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri atakapokuja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kitabu chetu hichi Mhe. Waziri hapa alipokuwa akizungumzia katika ibara ya 49 kifungu Nam. 116 alizungumza maneno yafuatayo. Katika kuwatafutia ajira vijana wetu wanaomaliza mafunzo katika vyuo mbali mbali. Hapa amezungumzia vijana, ofisi yangu imefanya mazungumzo na kukubaliana na Afisi ya Rais, *Management* ya Utumishi wa Umma SMT juu ya mgao wa ajira wa pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wizara na Taasisi za Muungano kwa uwiano wa 21% kwa Zanzibar 79% kwa Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninapatwa na hofu na suala zima la uajiri katika vikosi vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Polisi pamoja na *Immigration*. Kwa sababu na hawa pia ni watumishi na wanafanyia shughuli zao na majukumu yao hapa hapa Zanzibar. Lakini si vikosi hivi tu hadi na maeneo mengine ambayo yanagusa sekta za muungano. Sasa sijui kuna *connection* ya aina gani baina ya Wizara husika na zile *sector* ambazo watumishi wake wapo Zanzibar lakini wapo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sijui takwimu zao watakuwa wanazo na uhalisia wao wanauweka katika utaratibu upi. Nilitaka kuelewa vile vile katika suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nilikuwa nataka kuja katika suala zima la Utawala Bora. Utawala Bora inagusa katika maeneo mapana sana ndani ya nchi yetu. Jana wakati tulipokuwa tunamsikiliza ndugu yetu upande wa pili wa Muungano ndugu Tundu Lissu alikuwa anazungumzia na alizama hasa katika sekta nzima ya utawala bora katika masuala hasa yanayohusu muungano.

Mhe. Naibu Spika, mimi niliomba kunukuu baadhi ya maeneo wenzetu walikuwa wanayazungumza katika maeneo yale kwa siku ya jana. Anasema kama hivi ifuatavyo:-

> "Katiba ya Muafaka au Katiba ya Uhuru Mhe. Spika, misukosuko ambayo imeukumba Muungano wetu tangu mwaka 1964 hailingani na hatari kubwa inayoikabili hivi sasa. Kama tulivyomueleza Rais Kikwete katika waraka wetu wa tarehe 27 Novemba 2011, muungano wetu upo katika hatari kubwa ya kuvunjika kwa sababu ya mabadiliko makubwa ya Kikatiba ambayo yamefanyika katika Katiba ya Zanzibar mwaka 1964 na kutokana na Mswada wa Sheria na mabadiliko ya Katiba hiyo."

Mhe. Naibu Spika, kusema kweli mambo haya ambayo yalikuwa yametokea hapa hapakuwepo na suala la uvunjwaji wa Katiba au suala la kupinga utawala bora, katika mabadiliko mazima ambayo yalikuwa yamefanyika au mambo ambayo yalikuwa yamepitikana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika Katiba yetu ya Zanzibar ambayo wenzetu tayari wanaikwiri. Kifungu cha kwanza cha Katiba ya Zanzibar kinasema Zanzibar ni nchi ambayo eneo la Mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na

Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo vinavyozunguka na bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Vile vile ibara ya pili inasema Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa mwenzetu anapokuja akaja akazungumza katika chombo kikubwa kama kile, kuzungumzia kwamba hapa tumekiuka utawala bora. Hebu Mhe. Naibu Spika, tunaomba katika mambo 10 ambayo mwenzetu alikuwa amekuja kuyazungumzia kwa siku ya jana tumpe nafasi hapa Mwanasheria Mkuu ili atakapokuja hapa aje atupe ufafanuzi kweli Zanzibar ilikiuka utawala bora katika masuala ya ubadilishaji wa mabadiliko ya kumi ya katika Katiba ya Zanzibar. Tunaomba maelekezo hayo.

Lakini pia katika katiba hiyo hiyo ambayo wenzetu labda walikuwa hawakuangalia vizuri katika kifungu cha 103 kinasema naomba kunukuu. Kutakuwa na kiongozi wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambaye ndiye atakuwa Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile atakuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kilichozungumza hivi au kilichotoa maelekezo haya ni Katiba za Serikali zote mbili. Zanzibar pamoja na Tanzania Bara au Tanganyika kwa wakati ule ndizo zilizounda serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelekezo haya machache tutaomba kwa heshima na taadhima Mhe. Mwanasheria Mkuu atakapokuja hapa atuelekeze kwa kina juu ya suala hili zima ambalo linaelekeza kwamba utawala bora umekiukwa katika nchi ya Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, mengi na mazuri yameshazungumzwa kwa kina, lakini kwa dhana ile ile ya Mhe. Rais ya kumteua mwenzetu, ndugu yetu, Haji Omar Kheri basi hatuna budi kumsaidia kwenye maeneo ambayo tuna michango ya kusaidia. Wizara ni mpya, watendaji mahiri alionao, sasa ni vyema kwa mle tunamomuona kunahitaji kuwekwa sawa tutafanya hivyo ili kumshauri waweze kufanya vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri atuelewe kwamba tuna nia moja tu ya kumsaidia na kushauri kwenye bajeti yake, bajeti ya Chuo imeomba bilioni moja, mia mbili sitini na saba milioni na laki tano. Ukenda kwenye mchanganuo ule mapato milioni sita na tisa, laki tano. Ruzuku mia sita hamsini na nane milioni, matumizi ya maendeleo milioni mia tatu, ukija ukijiuliza hapo kimahesabu tunaomba kidogo watuweke sawa kuna bakaa ya mia tatu na tisa. Hizi tunajiuliza zitaelekezwa wapi.

Lakini jengine kwenye kumalizia jengo matumizi mia tatu thamanini na saba milioni. Kule mwanzo kumetajwa milioni mia tatu. Hapa tatu na thamanini na saba kuna thamanini na saba za ziada. Thamanini na saba hizi zitatokea wapi na zitakuwa ni za ziada. Mia tatu zimeonekana lakini thamanini na saba zitatoka wapi? Hatujapaona, Mhe. Waziri humu tutahitaji kidogo utuwekee sawa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, limesemwa lakini kwa uzito wake naomba kulitilia mkazo ni GSO. Inalalamikiwa Mhe. Waziri pamoja na kazi nzuri aliyoifanya Mhe. Mwanasheria Mkuu ya ufafanuzi, sababu na madhumuni ya kuwepo kwake pale chombo hichi. Hatuna mjadala juu ya hilo lakini kazi inayofanya siyo iliyotajwa na Mwanasheria Mkuu. Hili ndilo lalamiko la walio wengi.

Mhe. Naibu Spika, ushahidi wa hilo ni mengi lakini na kukiukwa dhana hasa ya utawala bora ni vijana ambao wanamaliza masomo yao ya Sekondari ama vyuo. Wake ambao wazee wao kwa namna moja au nyengine wana nyadhifa. Hawa wanapewa ajira kama ni mpito si zaidi ya mwezi au miezi miwili tayari ana *scholarship* keshapewa nje ya nchi na serikali hii ndiyo inalipa. Majina hayo yapo ya hao na taasisi zilizofanya hivyo zipo. Sasa ni changamoto kwa Mhe. Waziri, tunakwambia majina tunayo na taasisi tunazo, tunazijua. Na walikokwenda tunakujua na vyuo vyao tunavijua, tunavyo. Sasa ile kazi aliyokupa Mhe. Rais ni hapo, utakwenda utaifanya iwe na pale utakapohitaji misaada yetu utakuja kutuona. Sisi hatutaki posho katika hilo, tutakushauri na kukusaidia.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ile ile utawala bora Mwalimu alisema uongozi bora, tumetumia neno zuri zaidi kwa wakati muafaka ni utawala bora sasa. Mhe. Waziri bado tuna tatizo kwenye mashirika na baadhi ya taasisi nyengine. Miundo ya bodi inadharauliwa kutoa mianya watu kufanya yasiyofaa. Sheria hizi tumezipitisha hapa, umuhimu wa vyombo hivi kwenye taasisi na huku kuna neno *ceiling* ya matumizi bila ya idhini ya bodi. Cha ajabu bodi inapewa

mgongo hata kama ilikuwepo kama vile inaanza kuzeeka. Inajitetea bodi Waziri anajibu ni kweli tunafanya kinyumenyume lakini ndio tunafanya.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyekiti wa bodi Shirika la Biashara (ZSTC) ametajwa, hivi muundo umekamilika wa bodi yenyewe ni swali. Mbona kuna tetesi kwamba bodi hii ndio iliyopata hiyo sakata nililolitaja. Baaada ya kutajwa huyu Mwenyekiti ikakomea hapo, msimu umeingia hadi sasa labda Mhe. Waziri atusaidie kuondoa wasi wasi uliowatinga Wazanzibari juu ya sehemu hiyo. Wazanzibari wanaumwa na fedha zao, kwa hiyo wakisikia harufu huwa wanatufuata kutulalamikia. Kwa hivyo naomba wizara yako iwaondolee wasi wasi huo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni vifungu vya matumizi Mhe. Waziri ndugu yangu, swahiba yangu kuna vituko na vichekesho. Naomba sana ukakae na watendaji wako na hapa kuna maeneo itabidi kwanza tukuzuie, lengo ni kupata ufafanuzi hatutaki kukunyima matumizi kabisa. Dhana ni ile ile ya Rais Mheshimiwa wetu ndiyo tuliyonayo, lakini tunataka tujiridhishe.

Mhe. Naibu Spika, unafika mahali unaambiwa chakula na vinywaji ni X lakini mimi nataja tu kwa mfano X shilingi, halafu kwenye sub vote hiyo hiyo inaandika *refreshment* ama vinywaji sasa peke yake. Sasa hapa utapata swali chakula na vinywaji iwe ni maji na chakula halafu huku vinaandikwa vibutudishaji labda vinywaji ndio vya moto ni wageni maalum. Sasa lugha zinatuchanganya, Mhe. Waziri tunataka utuwekee sawa kwenye maeneo kama haya. Wenzangu wengi wameyataja haya, inakuwa ni zaidi. Unakuta ununuzi wa vifaa vya kuandikia kama Afisi Kuu Pemba utakuja kujiuliza hivi ni kila chumba kompyuta ama wengine imekuwa ni vifaa vya kuandikia tu, kutoka milioni 6 mpaka 21, kumezidi nini na nini.

Mhe. Waziri hapa tatizo sikuona wingi wa pesa, lakini hakuna mchanganuo, tunashindwa kufuata. Mwaka jana imenunuliwa hii TV, haipo imeibiwa, mbovu, au vipi na vipi, mahitaji yameongezeka kiasi gani mpaka iwe tunahitaji fedha kiasi hichi. Hizi ni pesa za watu zinahitaji maelezo, sasa kuziidhinisha hivi hivi kidogo inatupa mashaka. Tunaomba tueleweke hivyo, tunataka tupate mashiko ili tutoe *go ahead* kuhusu haya, hatuna jengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima nataka na mimi niingie kwenye Afisi ya CAG. Niungane na wenzangu kumpongeza sana mama kwa jitihada yake. Lakini pia naomba niseme kwamba penye zuri na baya lipo. Hii Afisi ni koo ya serikali, tunahitaji tuone utendaji ni 100 + kuondoa mashaka, wasi wasi wa wananchi wa nchi hii. Lakini vitendea kazi navyo serikali ihakikishe kwamba kwa jitihada zote zimekidhi mahitaji. Rasilimali watu wanaofaa kwenye fani yenyewe. Afisi hii wanazo *human resources* ambao *qualified* wapo.

Mhe. Waziri kuna malalamiko wametelekezwa hawafanyi kazi zao kama walivyofundishwa. Nafasi zao ambazo ingestahiki wao wafanye wanafanya watu wengine ambao hawaku *qualify*. Mhe. Naibu Spika, mwenzangu Mhe. Hamza Hassan Juma, *human resources auditing* inahitajika kwenye Afisi hii. Tunahitaji *transparency* kuiona na tusione tu ambayo ina – *operate*.

Mhe. Naibu Spika, mgawanyo uliokuwepo hapo Kamati ya Baraza hili tukufu iliyosomwa jana, ilithibitisha kwamba ripoti za Afisi hii zinajirudia kwa nini na yawaje Kamati ya Baraza iingie kwenye taasisi za serikali ikakute madudu kwenye ripoti ya CAG haipo, *question mark*. Hii ndiyo dhana kwamba wale *qualified human resources* haifanyishwi kazi yake badala yake wametelekezwa kuna watu wengine wanafanya hayo.

Mhe. Waziri hiyo ni kazi ipo, inahitaji kufanywa, kusudi wewe ni Alhajj na Mhe. Rais kakupa hiyo kwa makusudi, Utumishi na Utawala Bora, jicho linakutizama, Wazanzibari wanakutizama, wakulima wanakutizama, na Baraza hili tunakutizama kwa macho yote. Tutakusaidia pale pa kukusaidia lakini ukija ukitutafunia maneno tutakubinya, hatutaki kutafuniwa maneno kwenye maslahi ya watu na mali zao.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Pia nikupongeze wewe kunipa nafasi hii adhimu ili na mimi niweze kutoa mchango wangu japo mdogo juu ya hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia nimpongeze Mhe. Waziri na

watendaji wake kutuandalia hotuba hii ambayo ni dira ya maendeleo ya nchi yetu katika masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Baada ya hapo niende moja kwa moja katika kitabu. Nitazungumza kwa uchache kiasi ukurasa wa 3 kuhusiana na majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametwambia hapa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jukumu la kusimamia utendaji wa Utumishi wa Umma ili waweze kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu cha ufanisi na kuimarisha Utawala Bora nchini. Hii sentensi ina maana kubwa na ina maana pana sana, masuala mengi ya Utawala Bora wameyazungumza Wajumbe wengi ambao wamesimama hapa kutoa michango yao. Mimi nitazungumza japo kwa muhtasari.

Mhe. Naibu Spika, utoaji wa huduma unahitaji uzalendo wa hali ya juu kabisa. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri ajue kwamba ana jukumu kubwa la kusimamia watumishi wa umma, pamoja na utawala bora katika nchi ili nchi yetu iondokane na mashaka na malalamiko mengi ambayo yapo hivi sasa, katika masuala mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha sana katika utendaji wa baadhi ya watendaji wetu kuchelewa kufika hapa katika majukumu yao ya kazi. Inasikitisha kwamba katika kazi inawezekana siku nyengine kiongozi Mkuu amefika lakini viongozi wengine baada ya yule kiongozi mkuu wanachelewa kufika bila ya sababu zozote za msingi. Sijui Mhe. Waziri atatwambia nini juu ya kuirekebisha hali hii, ili kila mmoja ajue wajibu wake na utekelezaji wa majukumu yake katika kazi ile ambayo amepangiwa. Mimi niseme tu inawezekana hata katika wizara mbali ya afisi ndogo ndogo basi inawezekana Waziri anaweza akafika mwanzo katika afisi yake kuliko hata Katibu Mkuu, Mkurugenzi au Mtumishi mwengine. Mbali katika masuala ya huduma kama hospitali, wanaweza wakafika wagonjwa madaktari hawapo. Hili ni suala ambalo Mhe. Waziri uliangalie kwa upana na ulitolee taaluma ya kutosha ili kila mmoja ajue wajibu wake na ajue nini maana ya utawala bora na nini afanye katika jukumu lile ambalo amepangiwa.

Nikiacha hapo Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa sababu wachangiaji wengi walieleza juu ya umuhimu wa ofisi hii, kwa hivyo na mimi nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuitaja ofisi hii japo kwa muhutasari.

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii ni muhimu kama alivyosema Mhe. Asaa Othman Said kwamba hii ndio koo ya serikali, kwa nini ikawa ndio koo ya serikali? Mhe. Naibu Spika, mapato yake ambayo yanakusanywa katika nchi lazima yadhibitiwe na yakaguliwe na huyu ndiye mkaguzi na mdhibiti wa hesabu za serikali, mwanadamu koo yake hii hapa ina maana akikatwa hapa hana uhai. Ofisi hii inahitaji au inahitajika serikali iiangalie vizuri kuiwezesha.

Mhe Naibu Spika, mimi nataka nizungumze kwa uchache tu kuna ripoti ya mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za serikali za mwaka 2009/2010, kitabu hiki nataka nifungue ukurasa wa tatu (3) kuna neno limeandikwa ‘matatizo’ *point* ya sita hii nataka niinukuu.

> “Ofisi inaendelea kukabiliwa na tatizo la upungufu wa wataalamu katika fani mbali mbali zitakazosaidia kukabiliana na mbinu na aina mpya za ukaguzi, wataalamu wanaohitajika ni katika fani tofauti zikiwemo fani za uhandisi, ufamasia, uchumi, mazingira na kadhalika. Ofisi inajitahidi kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya kwa kushirikiana na vyombo husika”.

Swali, je Mhe. Waziri, vyombo husika vya kuiwezesha taasisi hii kuendelea na kazi zake vyema ni zipi, na kutokana na masuala haya ambayo ni kero au ni tatizo katika ofisi hii toka kiwasili kitabu hiki ikiwa leo tupo mwaka 2012/2013 ni tatizo gani ambalo limetatuliwa kutokana na haya ambayo wameyaeleza hawa ofisi ya mdhibiti ili kukamilisha shughuli zao na utendaji wao vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niseme kwamba ofisi hii kama hatukuipangia, hatukuiwezesha, hatukuwapa wataalamu ambao wanajitosheleza, basi mapato yote tutakayoyakusanya yataingilia mkono wa kulia yatoke mkono wa kushoto; wananchi wetu wabakie katika hali duni na malalamiko yasiyokwisha katika nchi hii.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, niangalie kidogo katika ripoti ya mdhibiti huyu huyu katika kipindi cha mwaka 2008/2009. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tuna tatizo kubwa mno la upoteaji wa fedha za serikali na mali za serikali kiholela. Kwa mfano, niangalie ukurasa wa 21 wa ripoti ya mwaka 2008/2009, malipo yasiokuwa na stakabadhi ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika lakini stakabadhi husika hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika. Kutoambatanisha stakabadhi katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kanuni ya 95(4) ya kanuni za fedha za Zanzibar ya mwaka 2005.

Hii ni *sampling* tu niliyopenda kuieleza Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki kama utakiangalia kuanzia *page* ya kwanza mpaka ya mwisho kuna malalamiko ya namna hii na mfano wa haya mengi sana. Kwa hivyo nimuulize Mhe. Waziri, nani ambaye anahusika na kutoa maelezo au maelekezo baada ya ripoti ya mdhibiti na baada ya uchunguzi wa Kamati ya *PAC*. Hili nazungumza kwa sababu, ripoti hizi zinakuwa zinaletwa kila kipindi lakini hakuna chengine ambacho kinaendelea baada ya kusomwa ripoti hii. Je, Mhe. Waziri hizi ziwe ni ndogo tu, ili kuzidhibiti fedha, huduma za wavuja jasho wa nchi hii inapaswa kuwe na chombo maalum baada ya ripoti ya mdhibiti na baada ya ukaguzi wa Kamati ya *PAC* kuwe na jawabu maalum kwa wale ambao wanahusika. Kitabu hiki kina mamilioni ya shilingi.

Lakini tukiondoka hapo kuna vitabu vitatu hivi ambavyo tayari wameshavitoa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali nako kuna mashaka kama hayo. Je, tunakwenda wapi? Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba tubadilike, watendaji wa nchi ya Zanzibar wabadilike hatuwezi kuwa na maendeleo ya aina yoyote bila ya kubadilika katika matendo yetu na moja katika kubadilika Mhe. Naibu Spika, si vyengine ni kufanya wajibu wako na ukatekeleza yale majukumu ambayo umepangiwa kiuadilifu. Hapa panahitaji uzalendo wa hali ya juu. Mhe. Waziri bila ya kuwa wazalendo hatuwezi kuendelea.

Mwalimu Nyerere alisema yeye kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne; ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Mimi nasema kwamba na la tano uzalendo uwepo, kabla ya kuwepo uzalendo hayo manne sisi tunayo Zanzibar kwa sababu watu tunao, ardhi tunayo, sijui siasa safi na uongozi bora, lakini pamoja na hayo uzalendo, kwa sababu siasa safi na uongozi bora uwepo uzalendo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awaelimishe watendaji wa nchi ya Zanzibar kuwa na uzalendo ili rasilimali zinazopatikana katika nchi hii ziwaenee wavuja jasho ambao kila siku ni malalamiko juu ya maisha magumu ambayo yanawakabili hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali niende kidogo katika Chuo cha Utawala wa Umma. Mhe. Naibu Spika hiki Chuo ni muhimu mno, chuo hiki ni muhimu kwa sababu kinatoa taaluma mbali mbali kwa watendaji wetu kwa maana hiyo hiki chuo kinakabiliwa na changamoto nyingi, miongoni mwa changamoto zinazokikabili chuo hiki kwanza ni uhaba wa mahali pa kusomea. Wanafunzi wanapata tabu wanasoma katika maeneo mbali mbali. Kwa hivyo, pamoja na bajeti ambayo imepangwa kwa ajili ya kukimaliza chuo cha Tunguu mimi naomba chuo kile kimalizike haraka haraka ili wanafunzi hawa wapate kujisomea kwa vizuri na kujitanafasi katika shughuli zao za masomo.

Lakini miongoni mwa changamoto ambazo zinakikabili Chuo hiki inasemekana tu kwamba, kuna baadhi ya wizara zinapeleka wanafunzi pale kwa ajili ya kusoma lakini hawalipi, wanachelewa kulipa malipo ya chuo kile kwa hivyo ina maana chuo kile kinapata kudhorota, kinadhoofika katika baadhi ya mambo yao ambayo yangewafanya kwamba waendelee zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niende katika ajira, ajira ni kitu muhimu mno lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba ajira hivi sasa zinalalamikiwa sana kutokana na suala zima la upendeleo wa ajira. Tunamuomba Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndiye mwenye bendera ya utumishi wa umma atueleze ni vigezo gani anavyotumia ambavyo vinamfanya kila mwenye haki kupata haki hii, na vigezo gani anavyotumia mpaka ikabidi kuweko malalamiko. Inasemekana kwamba kuna watu mbali mbali waliajiriwa lakini hawakutimiza viwango vile vinavyotakiwa, hii lazima malalamiko yaweko kwa sababu kuna vijana wetu wengi wamesoma, wana sifa za kufikia ajira ile inayostahiki hawaajiriwi watu wanapita kwa mkono wa kulia wanatokea mkono wa kushoto, wengine wanapitishwa katika mlango wa nyuma.

Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri awe muangalifu juu ya hili, kwa sababu haki na wajibu ni watoto pacha lazima mwenye haki apewe haki yake na mwenye wajibu atekeleze wajibu wake.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, niende tena katika suala la mishahara. Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko makubwa kutokana na marekebisho ya mishahara ambayo yamefanywa na serikali katika kipindi kilichopita bajeti ya mwaka jana. Kwa kweli mimi niipongeze serikali kufanya hivyo, lakini malalamiko yaliopo ni kwamba ni hivi juzi tu wafanyakazi wengi ikiwemo kada ya ualimu wamepunguziwa mishahara yao kwa kiwango kikubwa, kiwango ambacho kabla ya marekebisho ya mshahara basi mkato wa kipindi hiki baada ya mkato huu kile kiwango walichokuwa wakipokea mwanzo kabla ya marekebisho hawakufikia.

Je, ni kigezo gani ambacho kilitumika mpaka wafanyakazi hawa kupunguziwa mshahara ambao kabla ya marekebisho hawafiki hivi sasa? Mhe. Waziri hili ni tatizo na kwa kweli niseme kwamba kinyume na kufanya utafiti wa hali ya juu kutakuwa na manung'uniko makubwa ambayo yatazifanya taasisi zetu zichelewe kwenda mbele kiutendaji kwa kuvunjika moyo wafanyakazi.

Mwisho nauliza swali tu, katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu baada ya kumpongeza, majengo yale ambayo wameyajenga pale amejenga majengo mazuri kwa gharama ndogo kiasi fulani lakini je, kuna jengo gani la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Pemba? Na je, watajitegemea lini kama jengo hili halijakuwepo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kupata fursa ya kuchangia hotuba hii, na mimi ningependa nimpongeze Waziri kwamba na yeye kaona mengi na kafika kutuletea hapa ili apate baraka zetu, na nafikiri na yeye anaungana na mawaziri wenzake katika zile mbio ambazo mawaziri siku zote wanazipiga ili kuhakikisha kwamba malengo aliyoyapanga atayafikia na atayatekeleza.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni mpya na kusema kweli majukumu iliyopewa ni makubwa mno, na mimi Mhe. Waziri niko karibu naye sana, sasa labda kwanza ningependa tu kumpa mambo ambayo na mimi niliyapata kutokana na kusomasoma kwingi.

Mhe. Waziri kule Amerika ya Kusini katika miaka ya sitini mchezo wa mpira ulikuwa una rafu nyingi, fujo nyingi na dhulma nyingi. Mara tu kuna Rais mmoja alipoingia madarakani nafikiri wengi tunamkumbuka anaitwa Pinochet yeye alikuwa ni Rais wa Chile. Wakati anaingia madarakani waandishi wa habari walimuuliza wakamwambia vipi unaonaje hali ya nchi yako? Yeye alijibu na kusema kwamba, naomba ninukuu kwa Kiingereza alisema kwamba, "*Things are hardly more dangerous than a game of football in Latin America*", tafsiri ya Kiswahili nikitafsiri mimi nitasema nitakavyo lakini nawaachia kila mmoja aseme anavyotaka mwenyewe kwa tafsiri hiyo. Na naomba nimkumbushe tu kwamba na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa jina anaitwa **Kurt Waldheim** na yeye alihudhuria mkutano mmoja nchi Ivory Coast, hivi sasa tunaita *Cote d'ivore.* Pia na yeye aliwahusia viongozi wa Jumuia ya Uchumi wa nchi za Afrika ya Magharibi *ECOWAS* akawambia, *the missing element is not a technical knowledge, what has leaken is a political will*. Hivyo ndivyo alivyowaambia.

Na mara tu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipoingia madarakani na yeye kuna jambo aliligundua akasema sisi tuko siku zote na *business as usual*. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu nchi nyingi za Kiafrika haya ndio tuliyonayo, na namuona Mhe. Waziri ana kazi kubwa sana ya kujenga utawala bora katika nchi zetu za Afrika hasa kusini mwa jangwa la sahara. Kazi aliyopewa ni kama vile ya kumtia ngamia katika tundu ya sindano. Mimi namuombea dua tu lakini kazi aliyopewa ni kubwa, na pia Waingereza wamesema kwamba, *where there is a will there is a way*, namtakia kila la kheri.

Mhe. Naibu Spika, kazi hii si ndogo ya kujenga utawala bora katika nchi ambazo misingi yake inayotokana nayo ni mibovu tena mibovu sana. Juzi tu Waheshimiwa wengi hapa walikuwa wakilalamikia na walisema sana kuhusu vitambulisho. Nafikiri ujumbe umefika, hii ni dalili kwamba nchi haiko katika misingi ya utawala bora bado. Kwa hivyo, kazi kubwa aliyonayo Waziri hivi sasa ni kuhakikisha kwamba haya madogo na haya yaliyo nje basi anayatekeleza kwa haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo nataka niende katika mambo ya uchumi. Sisi au mimi ni mtu hapa katika Baraza hili na najifunza mengi sana, na baada ya kupitia kitabu hiki nimeona mengi sana, na nimeona haya huwa najiuliza hivyo haya ndio kweli tuliyosema kuwa ni vipaumbele, hivyo haya kweli ndio tuliyosema tunataka tuyafanye tukiacha yale mengine ambayo nahisi mimi yana umuhimu mkubwa zaidi? Wengi wamesema hapa kwamba matumizi yamekuwa mengine ni ya kiholela, kwamba unakuta idara zote saba au pengine nane zilizomo katika wizara hii basi zimeingiziwa au zimepewa posho kwa ajili ya vikao, posho kwa ajili ya kamati na tena pesa hizo sio

kidogo, nyengine utasikia shilingi milioni 38, nyengine 21, ukipiga hesabu kwa wizara hii tu basi unaweza kukuta shilingi milioni mia moja *plus*, basi pia zinaingia katika posho na vikao. Sasa je, sijui vikao hivi vinafanyika wakati gani, wakati ule ambao tupo kazini, wakati ambao tushaondoka kazini au vipi na zinalipwa katika misingi gani.

Lakini jengine ni kwamba katika hilo hilo nimegundua kwamba kuna idara ambayo imetajwa humu mara mbili, Idara ya Miundo ya Taasisi. Kuna fungu limeingiziwa 21 kuna sehemu nyengine idara hiyo hiyo imeingiziwa 38. Sasa mimi najiuliza, ingelikuwa fungu hili kweli limekosewa katika ukurasa mmoja *amount* isingelikuwa ni ile ile, kwa nini sasa hapa katika ukurasa mmoja iko 21 ukurasa mwengine iko 38. Sasa hapo napata mawazo kwamba hizi pesa ambazo huwa zinaingizwa labda huwa zinaingizwa tu, lakini ule utumiaji wake haupo sahihi kwamba hapa tunataka kufanya hiki, kwa nini hapa iwe 21 na hapa iwe 38.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anieleze hii imekuja kimakosa kwamba imekuja mara mbili Idara ya Miundo ya Taasisi kwamba hapa wamepata posho la vikao 38 lakini sehemu nyengine imekuja tena wamepata 21 ni makosa au ni vipi.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamezungumza hapa kuhusu Idara ya Udhibiti na kama walivyosema kwamba hapa ndio roho ya nchi kwa sababu wao ndio wanaotupa dira ya kuuona huo utawala bora ukoje. Wanatwambia kwamba idara fulani kuna moja na idara fulani kuna mbili. Lakini katika hili bado tunaendelea kuwa tuko pale pale kwamba hata tukitoa ripoti basi ripoti zetu zinabakia kuwa hazitekelezwi, ni kama vile na sisi kama ni muhimili tulio peke yetu wa Baraza, unapofika wakati wa kutoa ripoti lakini utekelezaji tunaona tumsubiri mwengine sasa hii mihimili sijui hapa tunafanya kazi vipi.

Mheshimiwa aliyenitangulia alizungumza mengi kuhusu ukosefu, lakini ukosefu ule hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Katika ripoti hii ya Mkaguzi Mhe. Naibu Spika, imeeleza kwamba kuna baadhi ya mashirika hakuna hawakupata ripoti hao *CAG*, lakini hakuna ripoti yoyote na mashirika hayo ndio mashirika makuu ya ukusanyaji kodi. *ZRB*, Benki, Shirika la Meli, wao wametupa ripoti tu kwamba hawa, lakini hawakukabidhi ripoti zao za mwaka. Nini lilifanyika baada ya hilo Mhe. Waziri, je kuna utaratibu wa mtu ambaye hakupeleka ripoti yake ya mwaka kuwa na adhabu fulani au utaratibu wowote uliowekwa kuwa huyu ambaye hakuweza kukamilisha ripoti yake anatakiwa afanye moja, mbili, tatu au hakupeleka ripoti basi. Sasa sisi tutapata vipi ripoti mfano *ZRB* wamefanya nini hamna yaani tunakwenda tu *business as usual* hakuna jengine linalofanyika.

Mhe. Naibu Spika, naingia kidogo katika zoezi la wafanyakazi, sijui niseme kwa lugha gani. Lakini mimi nashangaa mpaka hivi sasa ikawa hakuna takwimu, na tuna mtakwimu mkuu ambaye anatupatia ripoti tunazozitaka ya kuweza kujua kwamba hivi sasa tuna wafanyakazi fulani katika idara fulani na wana sifa fulani, kiasi kwamba ifike kuwa muajiriwa anafika wakati wa kustaafu lakini hatujui kwamba *replacement* yake atakuja nani, hatuna mipango kama hiyo. Nina imani mimi kwamba ipo lakini sasa utumiaji wake sijui ni vipi, tunakwenda kumchukua mtu ambaye muda wake umemalizika tunamuongezea muda, yule ambaye tumemsomesha tunamwambia wewe subiri na tumemsomesha kwa gharama kubwa kwa sababu sisi wengine tuliokwishazeeka tumesoma huko wakati tukisema kwamba ile sera ya elimu bila ya malipo au elimu bure ilikuwa ipo, sisi wengine tumesoma bure. Lakini sasa hawa wametumia pesa zao nyingi lakini tunawaambia bado nyinyi subirini tunakwenda kumchukua mtu ambaye tayari muda wake umeshafika tunamuweka pale, sijui tutaendelea na sera hii mpaka lini, wakati sisi tunataka kuwajengea ajira na tunasema tunataka tufanye utawala bora. Lini tutafikia hatua kama hiyo.

Mimi nahisi serikali ingeacha mara moja hili zoezi la kusema hawa tuwaongezee muda. Tuna vijana ambao wameenea ulimwenguni kutafuta elimu, na leo wamerejea kwao kwa nia nzuri ya kuja kulitumikia taifa lao, lakini tunakuta bado wale ambao wameshamaliza muda wao tunawaongezea muda. Hili zoezi ningependa Mhe. Waziri akaliangalia kwa makini na muda mfupi likaondoka ili kutoa fursa kwa vijana wetu, na ili kuwapa vijana wetu moyo wa kuona kwamba tunasomeshwa na baadae tunapatiwa ajira.

Mhe. Naibu Spika, katika hilo wizara hivi karibuni ilikuwa na zoezi moja kubwa sana, na zoezi hili ilikuwa ni kuwatambua wale ambao ni wafanyakazi labda sijui waliokamilika au waliopo kazini au sijui vipi. Zoezi hili kuna baadhi ya wizara zilikuwa na kasoro nyingi sana, Wizara ya Elimu kuna mwezi wa Aprili zilibakia fedha kwa ajili ya mishahara karibu ya shilingi 60 milioni, lakini ilipokuja tena katika mwezi wa Mei zoezi hili liligundua fedha nyingi zaidi ya zile za mwezi wa Aprili. Sasa sijui hili zoezi lao likoje na je, wamepata picha gani serikali baada ya zoezi lao hili, na kama wamegundua watu ambao hawakuwemo katika orodha au walikuwa kama ni hewa sijui hatua gani zitachukuliwa baada ya kuona kwamba kumetokea ubadhirifu huo.

Lakini katika hilo hilo labda tumejifunza mengi kwamba ukiulizia unaweza kuambiwa aa wafanyakazi tu wengine tunataka wathibitishe, idara hiyo hiyo moja inakwambia aa huyu mfanyakazi wetu hayupo yuko nje. Ah! Sasa kama alikuwa mfanyakazi anakwenda nje kusoma alipewa ruhusa na nani, si kapewa na wizara. Sasa wizara inafika hadi kusema kwamba tumempelekea ajieleze atuletee maelezo kwamba yeye ni mfanyakazi, aliajiriwa na nani si Wizara yako. Sasa haya Mhe. Waziri yanatupa wasi wasi, kwa hivyo ningeomba zoezi hili kama linafanyika basi na Wizara ya Fedha wakahusishwa moja kwa moja ili kuepuka kumlipa mtu ambaye pengine hana kiwango kama kile, na pengine hayupo. Kwa sababu waliofanya hayo ilikuwa ni Wizara ile ile sasa leo wanakuja kukwambia ngoja tusubiri yuko Malaysia anasoma si ulimruhusu wewe kwenda kusoma, sasa leo vipi usijue *particular* zake na kwa nini usimpe muda maalum. Zoezi hili linamsubiri zaidi ya miezi mitatu au minne.

Mhe. Naibu Spika, najua utaniambia kwamba muda unataka kwenda mbele, naomba nimalizie labda kwa kuona hawa madiwani ambao wamechaguliwa kwa kura za wananchi. Hadi hivi sasa serikali haijafikiria lolote kuhusu watumishi hawa wa umma. Sasa mimi ningemuomba Waziri kwamba hawa walitumia fedha nyingi sana katika kupatikana kwao kwa sababu uchaguzi ni gharama. Na wao ni watendaji wakuu; hivyo mwaka unaofuata utuoneshe kwamba na wao ni watumishi wa umma au ni viongozi wa kisiasa na wao wakae upande mmoja wapo ili wafaidike na kule kuteuliwa kwao kama ni viongozi.

Lakini hivi sasa kimtazamo kwamba kuna watendaji; sheha na diwani, watendaji hawa wote mimi mpaka hivi sasa sifahamu kazi zao wanazifanya vipi. Kwa hivyo, hebu atueleze Mhe. Waziri nini hasa wajibu wake huyu diwani, na mpango unaonesha kuwa Diwani yuko juu au *seniority* yake iko kubwa kuliko Sheha. Lakini je, wao hawa watendaji wawili hawa wanajua yupi ana dhamana kubwa zaidi kuliko mwengine, na dhamana zao wanazitekeleza vipi. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa mchana huu kuwa ni mchangiaji wa mwisho katika mjadala huu tunaokwenda nao. Nikupongeze tu kwa kuniweka mwisho.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kufika hapa katika kazi yetu, na nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuleta kitabu hiki. Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja na Idara ya Utawala Bora ukurasa wa 23 katika sentensi moja ndogo inayosema, jukumu jengine la Idara hii ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili waweze kuelewa haki na wajibu wao kwa taifa.

Mhe. Naibu Spika, hapa kuna mambo mawili yaliyotajwa pamoja, haki na wajibu ni mambo ambayo yanakwenda sambamba. Mwanadamu anatakiwa atekeleze wajibu wake na hatimaye apate haki yake. Kuna baadhi ya wakati unapata haki pamoja na kutenda wajibu wako, sasa haki kwa watu ni neno pana sana; ni pamoja na kupatiwa mahitaji yote ya lazima, kupatiwa ajira kama ipo, kupata kila kitu ambacho ni cha lazima mtu apate hivyo ni haki ya mtu kupatiwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, upatikanaji wa baadhi ya haki kuna matatizo, na sijui kwa nini kuwa tumetandika Wizara hii ya Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, ningeomba hili jina libakie kama lilivyo ili mimi nisijelifanya vyengine, kwa sababu hii inaitwa Utumishi na Utawala bora, isijekuwa bora utawala ibakie utawala bora, hii idara ibakie na jina hili hili la utawala bora. Utawala bora ni kujitahidi kutekeleza yale yote ambao yamepangwa na kuziacha dosari zote ambazo zinajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, mimi huko nyuma nilikuwa mwalimu, na walimu walionisomesha wengi walikuwa wageni ama walikuwa ni Warusi na Wajerumani, mimi na wenzangu wachache tuliomo humu. Kwa wakati huo serikali ilikuwa ni sahihi kuagiza walimu wa kigeni kutusomesha, lakini je, baada ya miaka 48 tushukuru kuingia wa 49 kuna tetesi kuwa Zanzibar inataka kuagizia walimu wa kigeni wa sayansi, kipindi chote hicho sisi hatujapata walimu wa kuweza kujitosheleza? Nasema hatujapata, kwa nini, kwa sababu hii dhana ya utawala bora haijapewa haki yake. Kwa sababu tumesomesha wengi lakini kila anayehitimu anatafuta pahala anakwenda, kwa nini, kwa sababu bado haki yake ya kimsingi haitekelezwi.

Tuache hao wasomi wakubwa, tuchukue hawa wasomi wadogo walimu ambao tunao wa vyeti. Mhe. Naibu Spika, ni jambo ambalo mimi silielewi hata kidogo kuwa serikali imetoa asilimia 25 ya nyongeza ya mishahara kipindi kilichopita na wakapata takriban wote isipokuwa kwenye matatizo ndio yametokezea. Lakini hivi sasa kuna walimu

mishahara yao imepunguzwa kufikia pahala ambapo hata ule waliokuwa nao kabla ya nyongeza hii hawakuufikia tena. Hapa pamechukuliwa kigezo gani.

Nitoe mfano kulikuwa kuna walimu wanapata zogo lote hilo kwenye *scale* yao ilikuwa ni shilingi 167,000/- kabla ya nyongeza wakavutwa katika shilingi 230,000. Mwezi wa Juni walimu hawa wamepokea shilingi 161,000/- hata ile ya msingi waliyokuwanayo mwanzo haikufika tena kuna nini hapa. Tokea hapo walimu hawana mshahara isipokuwa kundi la watoto, mnachokuwanacho chote unakiramba wewe, na mwalimu huyu ka-*suffer* katika ajira hii takriban kwa miaka 33 au 34, ile *13 point* ambayo imo katika toleo la serikali hakuifika. Kwa sababu kama ataajiriwa mwalimu wa cheti leo wa *Form IV* ataanza kwa mshahara wa shilingi laki moja na sabini na mbili, mwalimu huyo akishafanya kazi kwa miaka 30 hapo hajafika. Hivyo tuna utawala bora au bora utawala tu, utakavyo wenyewe kwa kuwa serikali yetu ifanye itakavyo yenyewe.

Ningeomba Mhe. Naibu Spika, wizara iandae *scheme of service* ya watumishi. Mimi kama leo ingekuwa bado ni mwalimu ingelikuwa mjukuu wangu wa kielimu namchungulia vile, pengine ningekuwa nimetumia miaka 30 au 35 lakini nyuu kama aliyekuja leo mwenye elimu kama yangu ama mtalipwa sawa au atanipita, aka! Utaalamu hapa ndipo ulipotufikisha? Tunafanya nini, tunatoka wapi tunakwenda wapi. Mhe. Naibu Spika, hii dhana tuione kuna nini hapa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hapa pameelezwa kuwa kulibuniwa maombi ya ajira, na kuna ajira kama 3,356 ziliidhinishwa, hapa limetumika neno 'ziliidhinishwa'. Lakini limetumika neno jengine kuwa, ajira 2,552 zilikubaliwa. Sasa hii zilizoidhinishwa na zilizokubaliwa je, hizi zilizoidhinishwa 3,356 kama ziliidhinishwa si ndo zimekwishakubaliwa? Lakini hapa sasa kuna lugha nyengine zilizokubaliwa ni 2,552 ina maana kuna jengine ambalo ziliidhinishwa itakuwa hazikuajiriwa watu, kwa nini na zilikuwa zishaidhinishwa au ndio kauli hizo za mjomba na shangazi ndio itakuwa pembeni akiwa mtoto wa mjomba yake ipo. Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo napo nipate maelezo kwa sababu Idara hii au Wizara hii lengo lake ni kuratibu mambo yaende vyema.

Mhe. Naibu Spika, kuna pahala pameelezwa humu kuwa idara hii ilitoa mafunzo kwa Makatibu Wakuu sawa na wengineo, na ikatoa mafunzo mengine bure ya uraia kwa shehia sita za Unguja na shehia sita za Pemba, *well done* hapa. Lakini baadae ikatoa mafunzo kama hayo kwa wilaya nne za Unguja, lakini mafunzo kama hayo hayakwenda kwa wilaya hata moja ya Pemba, kwa nini. Mhe. Naibu Spika, huu utawala bora uwe ni bora kweli usiache mwanya baina ya visiwa viwili hivi, hivi ni visiwa vimoja bahari imetenganisha sasa na mwanadamu asitenganishwe aiache bahari tu, lakini mtenganisho wa bahari hautufanyi sisi kuwa ni watu tofauti, kinachofanywa upande mmoja wa visiwa hivi kwa sababu ni haki na wajibu pia kitendeke na upande wa pili.

Mhe. Naibu Spika, katika miaka ya mwisho mwisho ya 1960 Nigeria kulikuwa kuna utawala wa majimbo; kwa wakati huo ilikuwa ina majimbo 12, Jimbo la Mashariki lilikuwa likizalisha mafuta kwa wingi kuliko sehemu nyengine zozote, na kwa kuwa nchi hii imekutwa na utawala wa kijeshi mara nyingi, wakati huo ilikuwa iko chini ya utawala wa kijeshi na mtawala wa kijeshi wa jimbo hilo kwa wakati huo alikuwa *some body* akiitwa nadhani Kanal Ojukwu. Mwanajeshi huyu kwa kuwa jimbo lake lilikuwa lina uzalishaji mkubwa wa mafuta lakini kwa mtazamo wake yeye ikawa ile rasilimali inayopatikana kurudi katika jimbo lake ni ndogo, akahisi kuwa jimbo langu linaonewa na baadae kwa maana hiyo sijui kulikuwa sahihi au laa, aliamua kuliengua jimbo lake katika shirikisho la Nigeria, hatimaye akasababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe ingawa halafu alishindwa.

Mhe. Naibu Spika, sitaki nitoe ufafanuzi wa maelezo yangu hayo, lakini ni mambo ambayo yanaweza yakatokea popote duniani pale ambapo mwanadamu anapohisi mwenzake anamuonea, anamhujumu au anamnyima haki yake ya msingi.

Mhe. Naibu Spika, katika hali hii ningeomba wizara hii ikae, ipange, itathmini ili hatimaye ilete mwelekeo mzuri wa kuendesha wizara hii kama vile ambavyo imekubaliwa.

Zanzibar kama nilivyosema na kama walivyosema wengi tuna tatizo la ajira; na wenzangu wametaja upendeleo wa ajira. Mimi kwa kutumia kile kigezo upande mmoja kwa matukio ya aina fulani, upande wa pili kama matukio kama yale hayakupatikana pengine nifanye hii kama ni *question,* inaweza kuwa ni kweli huu upendeleo uko. Kwa sababu jambo dogo kama hili ambalo ni la mpito la mafunzo tu, upande mmoja ukakoseshwa, je ajira ambayo hatimaye itamuongoza na kumuendesha mtu inawezekana kweli ikawa upendeleo huo uko.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba tatizo hili litizamwe kwa undani wake ili twende vizuri ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu ya tangu asubuhi hadi hivi sasa, na wachangiaji *backbencher* tumemaliza tumebakia na wachangiaji wawili ambao watamsaidia Mhe. Waziri kujibu hoja jioni. Wa kwanza Mhe. Naibu Waziri wa Afya na wa pili Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ninachokiomba kwa Wajumbe kwamba jioni tuna kawaida ya kuchelewa sana, muda mwingi tunaanza kikao cha jioni mna watu 12 mpaka 15, sasa leo kuna hoja za msingi zimeulizwa kama patajibiwa hoja Mheshimiwa hayupo akipiga buti hatumnyanyui. Kwa sababu ukipewa maneno na mwenzio pengine ataongeza ama atapunguza, kwa hivyo ni haki mtu awepo mwenyewe asikilize hoja zake, hakuridhika ndio apige buti kutaka maelezo zaidi. Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao mpaka saa kumi na moja za jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nishukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa kile kilichoelekezwa kwetu Wizara ya Afya, ili kusaidiana na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kuweza kutoa ufafanuzi kwa upande wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Rais kwa kutengeneza Wizara hii ambayo kwetu sisi Wizara ya Afya imetupa afuwa kubwa. Mimi ni mfanyakazi wa Wizara ya Afya tangu hapo nyuma, lakini sikuwa nikijua kama tulikuwa na matatizo kiasi hicho mpaka baada ya kuundwa hii Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Lakini hivi sasa imetusaidia, imetuongoza, na tunaanza kutatua matatizo yetu tukishirikiana na Mhe. Waziri pale.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa msaada mkubwa ambao wanaotupa sisi Wizara ya Afya, tunapokuwa na matatizo, tunakaa kwa pamoja, tunashirikiana kutatua changamoto tulizokuwa nazo.

Katika majadiliano hapa, kubwa lililosemwa kwamba wafanyakazi wa Wizara ya Afya tuna matatizo ya *allowances* kwa watu wetu. Ninakubaliana na hilo lilikuwepo. Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa juhudi za pamoja na Mhe. Waziri wetu na Waziri huyu, tuliweza kulitatua tatizo hilo na sasa hivi kwa kipindi cha miezi kuanzia mwezi wa Oktoba madaktari wetu wameanza kulipwa *call allowances* hizo, na zilizobakia tutaendelea kuzilipa katika mwaka ujao wa fedha.

Lakini pia sio hilo tu, mambo mengine ambayo yaliyokuwa yametajwa ni suala la likizo. Kwa upande wa Pemba wameweza kulitatua hilo, na wote wanaokwenda likizo wanapewa, na kwa Unguja pia tumeanza, kwa sababu Unguja wafanyakazi ni wengi, kwa hivyo tumeanza kutoa na tunategemea miezi miwili mitatu ijayo tunaweza tukamaliza wale waliokwenda likizo.

Lakini pia tunasaidiana naye katika suala la *increment* kwa ajili ya wafanyakazi. Wafanyakazi tunatakiwa waanze kupewa *increment* zao, na hatua za kutayarisha hayo pamoja na wizara yake zinafanyika. Kwa hivyo tunategemea kwamba wafanyakazi wetu kuanzia mwaka ujao wa fedha masuala ya *increment* nayo yatakaa sawa.

Lakini kama hayo hayatoshi, tumesema kuna *call allowances*, lakini kuna *allowance* nyingi kwa wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Hayo yapo katika mchakato tunaoendelea nao kwa ajili ya wafanyakazi wengine wa Afya nao waweze kupata stahiki zao zile wanazopaswa kupata.

Suala ambalo limejitokeza la watu kulalalamikia mishahara wanaolingana kada. Katika kutembelea vituo watu wenyewe wamepata fursa kila mmoja kueleza shida zake, na tuliwapa fursa makusudi, kila mwenye shida zake aseme.

Wapo waliolalamikia mishahara, tukawaambia warudi kwa Mkurugenzi wa Kinga. Kwa hivyo wote wakaja wakapelekwa kwa mtu wa mishahara wakaleta vyeti vyao na kuhakikiwa mishahara yao. Na si hivyo tu, pia tumehakikiwa ninakumbuka mara mbili, matatizo madogo madogo mengi yametatuliwa. Lakini hata hivyo

tunawaambia wafanyakazi wetu, kwa yule ambaye bado hajaridhika na anahisi bado kapunjwa, aje wakati wowote na sisi tutamsaidia.

Kwa hivyo masuala haya kwa kiasi fulani tatizo limepunguka kwa kiasi kikubwa. Wizara ya Afya ni Wizara kubwa katika Wizara za serikali kama vile Wizara ya Elimu. Kwa hivyo na matatizo tunayo mengi. Lakini kutokana na wizara hii na miongozo na sera tuliyopewa, ni matumaini yangu kwamba matatizo hayo yatatatuka kwa kushirikiana pamoja, na itafika siku watu wa Wizara ya Afya tunaweza tukafanikiwa na tukaweza kupata stahiki na haki na posho ambalo tunalolitaka.

Hili limetusaidia sana sasa kuweza kuwajibisha wafanyakazi wetu. Maana wajibu siku zote uende na haki, utashindwa mtu kumwambia njoo ulale *on call* wakati humlipi. Lakini sasa tutakuwa na nguvu kurekebisha na kuhakikisha kwamba huduma zetu zitakuwa sawa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, na kutufikisha wakati huu kuendelea kujadili hoja hii, napenda na mimi nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa uendeshaji kwanza wa wizara, lakini na pia maandalizi ya hotuba na yeye mwenyewe jinsi alivyoisoma.

Lakini pili, mimi sifa ambazo ninampa Mhe. Waziri ni kwa sababu Mhe. Naibu Spika, moja katika bahati ambayo niliipata, na heshima ambayo nimeipata katika utumishi wa serikalini katika nchi yangu hii, ni kuanzisha Wizara ya Katiba na Utawala Bora wakati ule. Wakati ule ikiwa dhana bado ni mpya, na ninashukuru ilipoanzishwa hii Wizara mwaka 2000 nilipata heshima ya kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Leo ninapoona wenzetu wamefanya haya waliyofanya katika kipindi kifupi kuhusiana na utawala bora, kwa kweli ninawasifu kwa dhati kwamba wamefanya kazi kubwa sana.

Mimi niseme michango sehemu tatu tu. Najua Mhe. Waziri amejiandaa vizuri katika kujibu hoja. Lakini kwanza nitangulie kusema kwamba na mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, na niwaombe wenzangu tuiunge mkono ili tumuwezeshe Mhe. Waziri afanye kazi kubwa zaidi, kwa sababu kujenga utawala bora wanasema si jambo la mara moja, isipokuwa ni mchakato, yaani sio *event* lakini ni *process.*

Mchango wangu Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu suali liliulizwa sana uhusiano baina ya Tume za utumishi na Kamisheni ya utumishi. Siku zote mimi mawazo yangu yamekuwa kwamba ukitaka kuliangalia jambo hili, lazima uliangalie katika msingi wa mageuzi, kwamba msingi huu uliowekwa wa kuwa na kamisheni ya utumishi na tume za utumishi, ni sehemu ya mageuzi ya utumishi wa umma.

Moja katika maeneo ambayo yaliyohitajika kufanyiwa marekebisho, ni usimamizi wa utumishi wenyewe wa umma. Miongoni mwa matatizo yenyewe yaliyokuwepo ni kwamba hizi tume zilikuwepo, lakini zilikuwa na ushindani, lakini ushindani wao zaidi katika usimamizi wa maslahi ya watu hawa ambao wapo chini yao.

Lakini hakukuwa na utaratibu mzuri wa usimamizi mzuri kwanza wa maadili, utendaji wa ajira, na hata kuweka vigezo vya utendaji katika utumishi. Kwa hivyo wengi tunadhani kama kwamba hizi tume bado mawazo yanakuwa yale yale kuwa tume hizi zina kazi ile ile ya kuweka maslahi au kushughulikia suala la maslahi.

Lakini hilo Mhe. Naibu Spika, ndilo lililokuwa tatizo, kwamba hizi Tume zenyewe zilikuwa zinashindana kuweka maslahi kwa hawa watumishi wao, mpaka unafika wakati wote wanatumikia walipa kodi hawa hawa. Maana mwisho wa siku pesa ile inatoka kwa mlipa kodi, na pesa ile inakwenda katika mfuko mkuu wa serikali, *consolidated fund*.

Sasa matumizi ya *consolidated fund* moja katika matumizi yake ya msingi na ya mwanzo, ni ulipaji wa mishahara na maslahi kwa watumishi wa umma. Sasa lazima uwe na kigezo, ufike pahala hii kupishana kwao iwe kwa misingi ambayo imekubalika pahala pamoja, isiwe ni kwa ushindani wa kwamba kila mtu anasema aah! mimi wa kwangu ni bora kila mtu anavutia upande wake.

Sasa mageuzi ya Utumishi wa Umma yamekuja kuondoa huo ushindani, na kwa kweli Mhe. Naibu Spika hilo ndio limekuwa tatizo kubwa katika nchi zote ambazo zimefanya mageuzi ya utumishi wa umma, kwamba kumekuwa na ushindani wa hizi taasisi zinazosimamia watumishi. Kwa hivyo sasa kilichowekwa ni kwamba wote hawa wanachofanya wanapendekeza, na baada ya kupendekeza, *central establishment* kwa ushauri wa *public service commission* au wa hii kamisheni ya utumishi ndio wanaweka sasa vigezo.

Kwa hivyo kuna chombo, hizi Tume kazi yake ni kusimamia kwanza uajiri, maadili na taratibu za utumishi. Kamisheni kazi yake ni kuhakikisha kwamba hayo maadili ni kama *regulator,* kwa sababu hawa watu ukiwaachia wanakuwa kama na ushindani fulani. Sasa kazi ya kamisheni kubwa ni *regulator* wa hizi tume nyengine. Nadhani hili tumelizungumza kwa muda mrefu. Kwa hivyo ni suala ambalo kama tutaondoka hapo, tuache sasa turudi kila tume iweke mishahara kwa watumishi wake, tutakuwa tunarudi kule kule, hatimae tutarudi katika mizozo ile ile ambayo mageuzi haya yamekusudia kuyafanya.

Mimi rai aliyotoa Mhe. Mtando pale kwamba kwa nini hii Tume ya Baraza la Wawakilishi inapokuja suala la uteuzi wa Katibu, kwa nini na wao wasifanye kazi kama ile wanayofanya Tume ya Utumishi ya Mahakama ya kumshauri Mhe. Rais unapokuja uteuzi wa Majaji. Mimi ninadhani hiyo ndio katika dhana nzuri za kujenga kwamba, hizi tume tutizame wapi kuna mapungufu ili tuweze kuziimarisha, lakini tukisema kwamba turudi tena katika ule mchezo wa operesheni huria, tutarudi katika tatizo. Kwa hivyo mimi naomba tuliangalie hilo, kwamba madhumuni ya kamisheni ya utumishi wa umma ni kuchunga maadili.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikumbushe jambo moja tu kwamba hii kamisheni ya utumishi wa umma ina kazi mbili kubwa. Kwanza kama ni *regulator,* kwa maana ya kusimamia hizi tume nyengine, lakini la pili wenzetu wanasema hii *meritocracy commission.* Katika baadhi ya nchi kwa sababu misingi mikubwa ya utumishi wa umma ni kupata watu kuajiriwa kwa sifa, na tunaposema sifa wengi wamelizungumza hapa haina cheti tu. Ukisema unatumia sifa kwamba kwa cheti tu, hiyo siyo *qualification*, hiyo ni *credentialism*, yaani mtu mwenye cheti sasa huyo ndio unasema mtu mwenye sifa, lakini sifa zina maana nyingi pamoja na *aptitudeness*. Ile *aptitude* ya mtu katika kufanya kazi basi pia ule uwezo wake, maadili na mwenendo wake ni sehemu ya sifa.

Kwa hivyo, moja katika kazi ya kamisheni ya utumishi kuhakikisha sifa zinafuatwa hizi tume zinapoajiri watumishi katika utumishi wa umma. Kwa hivyo mimi ninadhani ni jambo la msingi la kulizingatia.

Lakini suala jengine ambalo nimeona labda na mimi nijaribu kulichangia ni suala la migomo. Mhe. Naibu Spika, kwanza nitangulie kusema kwamba sheria yetu ya mahusiano kazini, yaani *labour relation* Na. 1 ya mwaka 2005 inaruhusu migomo kama ni haki ya wafanyakazi.

Lakini naomba Mhe. Hamza bahati mbaya hayupo asiondoke baada ya mimi nikisha kusema hivyo, kwa sababu mgomo una masharti yake. Mgomo una masharti matatu makubwa. Sharti la kwanza ni kwamba iwe ni mgomo kwa ajili ya fursa na sio kwa haki. Yaani unatangulia na kitu gani. Mgomo unatangulia mapatano baina ya muajiri na muajiriwa, wanasema *collective bargaining* kuhusiana na fursa fulani zitolewe zaidi. Labda kuwe na nyongeza lakini huwezi kugoma kwa sababu hukupewa likizo au *maternity leave*, kwa sababu ile ni haki yako au hukulipwa mshahara, ule mshahara ni haki yako kuna njia yake ya kudai.

Lakini pia kuna na *procedures* ambazo sheria imeweka kwamba bwana ukitaka kugoma, basi utaratibu upige kura kwa hawa wahusika, na kura yenyewe iwe ya wazi. Lakini sharti kubwa la mgomo ni kwamba kuna watu hawaruhusiwi kugoma. Sheria yenyewe imesema kwamba baadhi ya watu hawaruhusiwi kugoma.

Na miongoni mwa wasioruhusiwa kugoma ni watu wanaotumikia katika sekta ya afya na huduma zake, ndio sheria inavyosema. Sheria Na. 1 ya mwaka 2005 inasema hivyo, imetaja wote, watu wanaohusika na usafi na masuala ya maji hawaruhusiwi kugoma, watu wanaohusika na afya na huduma zake nyenginezo zinazoendana na huduma ya afya hawaruhusiwi kugoma, na wengine wametajwa wanaohusika na masuala ya uzimaji wa moto, wanaohusika na masuala ya *navigation*, sheria yenyewe imeeleza mtu anaweza akasoma, kama mtu hana ninaweza nikamuazima hii ya kwangu, lakini imeeleza vizuri sana, na imetoa haki kwamba serikali inapokuwa mtu kagoma, wakati sheria haimruhusu mtu kugoma ichukue hatua zozote kuhakikisha mgomo huu haufanyiki.

Lakini na jengine imempa haki naye muajiri kumfungia nje huyo mfanyakazi. Maana yake ni mbili hizi; kuna *strike* na *lock out*. Kwa hivyo hizo ni katika haki za mtumishi. Ningeomba sana wafanyakazi hasa hasa hivi vyama vya

wafanyakazi, vijielimishe kuhusiana na hii sheria. Maana inaonekana kama kugoma si shangwe ni utaratibu wa kisheria ambao umeekwa na masharti yake mbali mbali.

Lakini la mwisho na mimi naomba nichangie lile alilolizungumza Mhe. Mahmoud ambaye ni Mwenyekiti wetu hapa kuhusiana kwamba marekebisho ya 10, anavyosema tumeambiwa kule Bungeni na mmoja katika Waheshimiwa Wabunge kwamba marekebisho ya 10 yanakwenda kinyume na utawala bora, kwa sababu Zanzibar tumevunja Katiba.

Mimi nimepata pia kusoma na kuangalia hiyo hotuba ambayo anayoisema Mhe. Mahmoud. Lakini pia nimeona na majibu ambayo yalitolewa, na hasa majibu aliyotoa Mhe. Shamshi Vuai Nahodha.

Moja amesema kwamba yale maelezo yaliyotolewa na Mhe. Tundu Lissu yamejaa hadaa, yamejaa na upotoshaji. Na mimi ninakubaliana naye kwamba niseme kwamba zaidi yamejaa upotoshaji, tena upotoshaji ambao umepindukia mipaka kwa kweli.

Kwa sababu la mwanzo ambalo linazungumzwa, hasa alilozungumza Mhe. Mahmoud kwamba Zanzibar kwa kusema kuwa ni nchi, anasema hiyo imejitangazia uhuru. Sasa Waheshimiwa jamaa zetu Wakojani wana msemo wanasema, "*Mungu lete baa iondoe balaa".*

Maana ya baa ni kitu kidogo, ni mtafaruku unaweza ukapita, lakini ukija huo uweze kuondoa balaa. Balaa ni jambo kubwa zaidi. Sasa wanao msemo huo *"Mungu lete baa iondoe balaa".*

Sasa kuja kwa haya yaliyokuja, yametuonesha kwamba kuna wenzetu kumbe wana fikra kwamba Zanzibar iliwahi kutawaliwa. Maana mtu anaposema marekebisho ya 10 Zanzibar imejitangazia Uhuru, maana yake ana fikra, na huyu ni mwanasheria, mtu ambaye kafika mpaka kuwa Mbunge, na anayeaminiwa na chama chake, lakini anasema kwa kufanya hivyo Zanzibar imejitangazia Uhuru. Kwani tulitawaliwa lini? Sasa hili mimi ninadhani limetusaidia kujua baadhi ya mawazo na fikra za wenzetu.

Lakini marekebisho ya 10 mimi ninadhani yamekuja kuimarisha Utawala bora. Kwa sababu gani? Niseme kwanza kwa sababu tatu muhimu.

Kwanza tunaposema kwamba Zanzibar imeseme, au marekebisho ya 10 yamesema kuwa Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizounda Jamhuri ya Muungano, ni kwa sababu kama mimi binafsi nilivyowahi kusema kwamba, bahati mbaya Katiba ya Muungano ina maswali mengi ambayo hayana majibu.

Moja katika maswali ambayo hayana majibu, lilikuwa ni hili kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, lakini kama nini? Kama Mkoa, kama Shehia, Kijiji au Kata, ndio lilikuwa swali. Sasa hilo halikuwa na jibu katika Katiba ya Muungano.

Katiba ya Muungano ilitakiwa iwe na jibu hilo, na ndio wenzetu ndio walivyofanya. Ukisoma Katiba ya *Waswiss.* Katiba ya *Waswiss* wala haikuja juzi juzi tukasema haya ni mambo ya kileo. Hii ni Katiba ya mwaka 1874. Lakini wao walielezana vizuri kwamba *federation* ya *Waswiss* imeundwa na Cantons na watu wa Uswiss.

Hawakuonea haya kusema kwamba, maana unaposema una *federation* lakini iliyounda hao *federation*, *constituency members* ni nani. Ndio nikasema hizi Cantons Ndizo zilizounda. Hata kwenye *preamble* au kwenye utangulizi wa Katiba yao, imesema kwamba sisi Cantons pamoja na watu wa *Swiss* tunatunga Katiba hii.

Kwa hivyo, tunatakiwa sisi kama tuna *constituency members* kwenye Muungano, Katiba yenyewe ilitakiwa iseme kwamba hawa *constituency members* ni wepi. Ndio utaratibu unavyotakiwa. Ndio maana ninasema hawa *Waswiss* wametunga hii Katiba yao 1874, kabla hatujajua kama kutakuja Tanganyika, maana 1874 Zanzibar ilishakuwepo. Lakini kabla ya kujua kama kwamba kutakuja Muungano.

Hawa wenzetu walivyotunga Katiba wakasema hivyo. *Warusi* ambao tunawaona kama ni ujamaa au *communist*, lakini kwenye Katiba yao nao wanasema hivyo hivyo, kwamba muungano wa Urusi umeundwa, tena wao wamezitaja kwa hadhi zao. Umeundwa *republic*, halafu wakazitaja hizo *republic* ndani ya muungano wao ni zipi.

Umeundwa na *regions*, *territories*, *special zones*. Kwa hivyo unakuta kwenye Katiba yenyewe imetaja. Sasa sisi Katiba yetu ya Muungano imekuja ikarukia tu, ikasema Tanzania ni nchi moja na Jamhuri ya Muungano. Ilitokea wapi na imeundwa na nani?

Sasa hilo ni swali ambalo lazima liwe na majibu katika Katiba. Ukijiuliza katika Muungano wa Urusi kwani umeundwa na nani, utapata majibu ndani ya Katiba yao, ya Waswiss utapata majibu ndani ya Katiba yao, na ya Wamarekani nao ambayo ni ya mapema zaidi utapata majibu ndani ya Katiba yao.

Sisi ya kwetu haikuwa na majibu. Sasa mtu anapokuwa wewe hakutambui, basi ni dhambi kubwa zaidi kuwa hata wewe mwenyewe basi hujitambui?

Marekebisho ya 10 ilichofanya ni kusema kwamba ikiwa mtu hatambui, maana ilikuwa imeshaonesha dalili kwamba kuna wengine hawatambui hilo, tena wakubwa. Sasa marekebisho ya 10 yalipokuja ni kufafanua tu, kama kuna mtu hatambui sisi wenyewe tunajijua *position* yetu. (*Makofi*).

M+he. Naibu Spika, na mengine niseme ukisoma kwenye Katiba za wenzetu ambao waliokubali kuwa na misingi imara, na ndio maana miungano ya ikaimarika, ni kwa sababu wameweka misingi. Lakini ukirudi kwenye hiyo Katiba ya *Uswiss*, hata raia jambo ambalo sisi lingeonekana pengine ni la kituko. Lakini Katiba ya Uswiss inasema raia wa *Uswiss* ni yule raia wa Canton Ukishapata raia wa Canton basi wewe moja kwa moja ndio unakuwa raia wa *Uswiss*. Ndio Katiba yao inavyosema, kwamba uraia huupati kutoka juu unaupata kutoka chini.

Pale ulipozaliwa ndio panapokupa uraia, na kuna mengi ambayo nadhani tatizo liliopo kwa wenzetu ni kwamba hawajifunzi kwamba Katiba, Muungano ni kitu gani. Muungano ni suala ambalo nchi mbili munapoungana, nchi mbili zilizokuwa huru ni suala la makubaliano. Mutakachokubaliana ndicho hicho ambacho kitakuja kwenye Katiba yenu.

Hakuna mtu ambaye atawazuiwa kusema aah! Katiba yenu isiwe namna gani au isiwe hivi. Ndio maana unakuta Katiba za muungano zipo nyingi, lakini kila moja ina *structure* yake kwa mujibu mulivyokubaliana nyinyi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, labda hapa nadhani Mhe. Mahmoud sijui swali lake nitakuwa nimemjibu, lakini mimi nadhani wa kusifiwa tumekuja kuimarisha Utawala bora. Maana moja ya msingi wa utawala bora ni uwazi.

Sasa marekebisho ya 10 yanaweka uwazi. Na nimeona jengine analalamikia kwamba aah! Tumeliimarisha hilo kwa kusema haliwezi kurekebishwa mpaka wananchi wapige kura. Sisi ndio wenye nchi yao? Sasa kuwashirikisha wananchi sio ndio sehemu ya Utawala bora. Maana hii tuliyonayo kwamba tunawasemea Barazani. Ni kama vile tumechukua kitu ukaki-*dilute* yaani ukakizimua.

Representatatives democracy ni mfumo uliozimuliwa wa ushiriki wa wananchi katika kuendesha mambo yao. Sasa tulipotaka hilo na huo sio mfumo wa vituko au ajabu. Kuna nchi nadhani Sweden, Finland huwezi kurekebisha kifungu chochote cha Katiba mpaka urudi kwa wananchi wakipigie kura.

Sisi tumechagua baadhi ya mambo, tukasema sasa hiyo dhambi, na hapo kwamba tumevunja Utawala bora. Mimi naona labda huyo anayesema hivyo ana tatizo la msingi la kuelewa nini maana ya utawala bora. Nadhani tatizo lake kubwa ni yale mawazo aliyokuwa nayo ambayo nilitangulia kueleza mwanzo. Hayo ndio yaliyokuwa yanamsumbua.

Mhe. Naibu Spika, labda nitumie fursa hii hapa hapa niseme kwamba wakati tuko kwenye mchakato huu sasa hivi wa maoni ya katiba, nadhani ndio wakati mzuri wa kuiweka sawa ile misingi ya Muungano. Wakati mwengine napata wasi wasi, nasema hii hofu yangu niiseme hapa hapa kwamba tunaanza kubishana kuhusiana na watunza nyumba wawe wangapi, waendeshaji nyumba wawe wangapi, wawili, watatu, wanne au watano, lakini tatizo letu la msingi mimi nadhani ni nyumba yenyewe iweje. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nadhani hilo ndio ambalo ni tatizo, kwamba tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo ni hii biashara yetu kuwa tunaiendesha vipi au hii nyumba yetu tunaiendesha vipi. Serikali kazi yake ni kuendesha tu, ndio maana nasema tunaanza kubishana kwamba hawa watunza nyumba wawe wangapi, wakati tatizo tujadili kwamba kwani

tunataka kwanza hiyo nyumba yenyewe iweje. Kama tunakodisha faida itakayopatikana tugawanaje, nani atakayekodisha, maamuzi ya kukodisha atoe nani, atoe mmoja peke yake kajifungia. Kama tunaamua kuishi, maana mfumo wa sasa hivi mmoja anaishi nyumba kubwa na mwengine mabandani huko uwani. Huo sio utaratibu ambao tunao. *(Makofi).*

Kwa hivyo, nilidhani kwamba Wazanzibari kama hayo ndio mambo ya msingi ya kuyajadili, kuhusu idadi ya watunza nyumba. Hilo ni suala ambalo mimi nadhani kwamba wale kazi yao ni ndogo sana, na utawajua wewe mwenyewe uwaweke wangapi, baada ya kuamua kwanza unataka iweje. Ndio maana ukaona kwamba Muungano ambao umedumu unasifiwa duniani, ni *Swiss Federation.* Kwa sababu umeanza tokea mwaka 1292. Wamekwenda kwa mafahamiano mwaka 1874 wakatunga katiba ambayo wameifanyia mapitio upya mwaka 1999. Ina serikali 26, lugha nne rasmi, lugha zao sio Kiswahili na Kiingereza tu, hapana ni lugha nne rasmi na huo ndio unasifiwa ndio Muungano ambao umedumu kwa muda mrefu na ndio nchi ambayo ni *stable.* Mashirika yote ya kimataifa yako Uswiss, kwa sababu gani, kwa sababu ndio nchi ambayo imedumu na ni kwa nini Muungano huo ukadumu. Ni kwa sababu umekuwa na misingi imara ya kuhakikisha Muungano ule unaweza ukahimili mabadiliko yoyote yatakayokuja ya kisiasa.

Kwa hivyo, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe na Wazanzibari wenzangu na wananchi wote, kwamba huko mbele tusije tukalaumiana kwamba umefanya marekebisho ya kumi, umetutangazia uhuru. Wakati wa kuyaondoa yote ni hayo, lakini tutaweza kuyaondoa kama tutaweza kujielekeza katika hoja za msingi, na mambo ya msingi katika hoja hii na hapo ndipo utakapojenga utawala bora ndani ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, najua Mhe. Waziri hapa ana mambo mengi ya kujibu, hoja nyingi za kujibu sidhani kama leo tutahitaji tuongeze saa tatu tena au hata nusu saa. Kwa hivyo, baada ya kusema hayo, naomba kusema tena kwamba naunga mkono hoja, na nawaomba sana wenzangu tuipitishe hoja hii, ili Mhe. Waziri akafanye kazi, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ingetosha maelezo aliyoyatoa Mhe. Mwanasheria Mkuu, kuwa ni majibu ya wale wote walioiuliza hoja ya kuwa kama kuna utawala bora au kuna bora utawala. Sasa huu ndio utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima, na namuomba pia awajaalie wale wote waliokuwa wagonjwa wapone, ili waweze kuendelea na majukumu yao ya kulijenga taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa nyengine, ili kutoa maelezo na kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, naishukuru kwa mara nyengine tena, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa michango yake ambayo ililenga kutoa ushauri na maelekezo kwa idara na taasisi zote za ofisi hii. Michango yao imeonesha ni kwa kiasi gani kamati inavyotekeleza kazi zake kwa umahiri na umakini mkubwa katika kuhakikisha Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inafikia malengo na matarajio ya kuanzishwa kwa ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, hususan wale waliopata fursa ya kuchangia hotuba yangu kwa maelekezo yao waliyotupa, hoja na maswali mbali mbali waliyouliza na wale waliochangia kwa maandishi, michango yao itaijengea uwezo zaidi wa kiutendaji ofisi yangu, ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa rasilimali za umma, utawala bora na utoaji huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar unakuwa kwa kiwango cha hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hotuba yangu ya bajeti imechangiwa na jumla ya wajumbe 24. Kati ya hao 22 wamechangia moja kwa moja na wajumbe 2 wamechangia kwa maandishi. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue wale wote waliochangia hotuba yangu kama ifuatavyo;

1. Mhe. Ali Abdalla Ali
2. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman
4 Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

5 Mhe. Asha Bakari Makame
6 Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7 Mhe. Salmin Awadh Salmin
8 Mhe. Omar Ali Shehe
9 Mhe. Suleiman Hemed Khamis
10 Mhe. Hamza Hassan Juma
11 Mhe. Mgeni Hassan Juma
12 Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
13 Mhe. Ismail Jussa Ladhu
14 Mhe. Fatma Mbarouk Said
15 Mhe. Panya Ali Abdalla
16 Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
17 Mhe. Asaa Othman Hamad
18 Mhe. Mohamed Mbwana Hamad
19 Mhe. Abdalla Mohamed Ali
20 Mhe. Mohamed Haji Khalid
21 Mhe. Naibu Waziri wa Afya
22 Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni

1. Mhe. Abdi Mossi Kombo na
2. Mhe. Bikame Yussuf Hamad

Mhe. Naibu Spika, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kuzitolea ufafanuzi hoja mbali mbali za Wajumbe, na maswali waliouliza na maelezo yangu yatalenga moja kwa moja katika hoja za wajumbe, badala ya kujibu hoja ya Mhe. Mjumbe mmoja mmoja katika kujibu hoja hizo. Ikiwa itajitokeza hoja ya Mjumbe kutojibiwa, basi isionekane kwamba kutokujibika huko kumefanywa kwa makusudi. Bali hoja hiyo itakuwa imetolewa ufafanuzi katika maelezo yangu ya jumla.

Mhe. Naibu Spika, hoja zilizoulizwa ni 55 na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali. Hoja ya kwanza ilikuwa ni Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutoipatia kamati gharama halisi za mradi wa *E- Government*. Swali hili liliulizwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile ofisi yangu bado haijakabidhiwa rasmi mradi huu. Tunashauri kamati iendelee kuwasiliana na Ofisi ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kulifuatilia suala hili. Katika suala hili, basi wizara yangu itashirikiana na kamati ili gharama za mradi ziwezi kupatikana.

Hoja ya pili Mhe. Naibu Spika, ilikuwa kamati imeshauri idara ya nyaraka na kumbukumbu za taifa, kupanga vipaumbele vyake kwa kuzingatia majukumu ya idara. Ushauri huu umezingatiwa na utafanyiwa kazi. Hata hivyo, katika mipango ya bajeti ya mwaka 2012/2013 idara imeweka msukumo maalum katika majukumu yake ya msingi, yaani *core functions* za taasisi ya idara ya nyaraka.

Hoja ya tatu ilikuwa ni kubadilisha miundombinu ya jengo hili, ili kuepusha mmiliki wa nyumba ya jirani asitumie mlango mkuu wa idara katika kuimarisha usalama wa jengo. Ushauri wa kamati kwa kuwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, juu ya kulipatia ufumbuzi suala hili tunaendelea kuufanyia kazi, toka pale kamati ilipokuja katika kukagua shughuli zake na hatimae tutafikia maamuzi ya kuweza kuufunga mlango ule kwanza. Lakini la pili, kuweza kupata ufumbuzi wa utatuzi wa yale matatizo yaliopo pale.

Hoja ya nne, ilikuwa ni kutafuta eneo jengine kwa lengo la kujenga ofisi mpya kwa idara ya nyaraka na kumbukumbu za taifa. Ushauri wa kamati wa kuwasiliana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa ajili ya kutafuta eneo jipya la ujenzi wa jengo la idara umepokelewa na tunaendelea kuufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya tano ilikuwa ni jengo la zamani la Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake litumike kwa ajili ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kule kisiwani Pemba. Hatua za kuwasiliana na mamlaka husika zimeanza kuchukuliwa ili kupatikane eneo lenye kukidhi uhifadhi wa kumbukumbu za taifa na nyaraka. Kwa kweli sasa hivi

tuko katika hatua ya mbali sana katika kufikia muafaka kati ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hizi ofisi zote kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu juzi, kwamba hizi ni ofisi za Mhe. Rais. Kwa hivyo, tunapoona kwamba kuna jambo ambalo linatakiwa lipatiwe ufumbuzi, basi tunapokwama huenda kwa mwenyewe na anaamua. Kwa hivyo, na hili nalo litafikia pahala litaamuliwa na jengo lile tutaweza kulitumia.

Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali watu huweka utaratibu mzuri wa utoaji nafasi za mafunzo hasa nje ya nchi. Utaratibu unaotumika baada ya kupata fursa za mafunzo ya nje ya nchi, ni kuziwasilisha nafasi hizo kwa Makatibu Wakuu na wakuu wa taasisi kwa mujibu wa fani zinazoendana na majukumu ya wizara na taasisi husika. Sisi kwetu pale hatugawi hizi nafasi kwa mtu mmoja mmoja. Sisi tunazipeleka kwa taasisi zinazohusika, na huo ndio uwazi na uwajibikaji.

Idara ya Utawala Bora itumie kamati zake kuchunguza na kufuatilia mwenendo mzima wa serikali. Ushauri huu umepokelewa na kamati iliyoundwa ya utawala bora inajumuisha wakurugenzi mipango, sera na utafiti kutoka kila wizara, na wajumbe wengine kutoka katika taasisi zisizo za serikali, imepewa jukumu hilo kama ilivyoelekezwa katika sera ya utawala bora.

Hoja ya nane ilikuwa Idara ya utawala bora kusimamia masuala ya utawala bora serikalini. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Rashid Seif Suleiman walitoa hoja hii. Ushauri huo umepokelewa na tayari hili jambo linafanyiwa kazi na kwa sababu kwa mujibu wa utaratibu, ripoti hii ya mwaka baada ya kuwasilishwa kwangu mimi, inatakiwa niilete hapa Barazani. Sasa kama mtakumbuka au mtafanya *reference* katika bajeti yangu, nilitaja mpaka tarehe ya ile kamati iliyozinduliwa. Ninachotaka kukuhakikishieni ni kwamba kamati hii itafanya kazi zake, na ikifika muda uliopangwa kwa mujibu wa taratibu, basi ripoti hiyo itawasilishwa hapa na Waheshimiwa Wajumbe mtapata nafasi ya kutoa maoni yenu.

Hoja ya tisa ilikuwa ni kuimarisha taarifa sahihi za watumishi wa umma. Hii ilichangiwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Ofisi inakubaliana na ushauri wa kamati na kuzitaka wizara na taasisi zote kuhakikisha, watumishi kuwa na taarifa za utumishi ni sahihi kwa ajili ya mipango mizuri ya rasilimali watu. Kama nilivyosema tayari tumeanzisha *data base* na taarifa karibu nyingi tunazo. Tumefanya upekuzi kama ilivyojitokeza kwenye bajeti yangu katika wizara 13, kwa kuchunguza OPF ya mtumishi mmoja mmoja na taarifa hizo tayari tunazo.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya kumi ilikuwa ni serikali kuanzisha utaratibu wa kuwajazisha mikataba watendaji wanaokwenda masomoni, ili wanapomaliza masomo yao watumikie taasisi zao. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Fatma Mbarouk Said. Ushauri huo umepokelewa. Hata hivyo, ofisi yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshatayarisha mkataba huo na umeshajadiliwa katika ngazi zote za kiutendaji ikiwemo Baraza la Mapinduzi. Katika mwaka huu wa bajeti tutaanza kuitumia fomu hiyo ya mkataba rasmi kwa watumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine kwa ajili ya wale watu ambao sio watumishi. Nafikiri wizara husika nayo ambayo inatoa mikopo nayo itafanya kazi hiyo. Lakini kwa upande wa watumishi, napenda niwahahikishie kwamba mkataba huo tayari na utaanza kutumika rasmi.

Hoja ya kumi na moja ilikuwa ni malalamiko juu ya ushirikishwaji wa maafisa wa ofisi kuu Pemba, katika utekelezaji wa majukumu ya wizara yanayofanyika Pemba. Hili lilizungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kimsingi kuna mashirikiano mazuri katika ngazi zote za kiutendaji, kuanzia hatua za utayarishaji wa mipango, utekelezaji wake na mgawanyo wa bajeti.

Aidha, kwa mwaka huu wa bajeti kila idara imeweka fungu moja kwa moja, ambalo litatumika katika utekelezaji wa majukumu ya kila Idara kwa upande wa Pemba.

Hoja ya kumi na mbili ilikuwa ni kuimarisha ripoti ya ukaguzi kwa kuhusisha taarifa za misamaha ya kodi, mapendekezo ya maeneo ya kupata mapato na maeneo ya uvujaji wa mapato na yale yanayoongeza mapato ya serikali. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Wajumbe wengine wametoa ushauri juu ya jambo hili. Ushauri huo wa kamati tutaendelea kuufanyia kazi na kuiwezesha serikali kuimarisha mapato, kwa

sababu tutakapofanya hivyo na kwa sababu jukumu la wizara yangu ni kuweka uwazi, basi nitahakikisha kwamba nasimamia suala hilo na masuala haya yote ambayo *CAG* anayaomba katika taasisi zinazokusanya mapato, na wizara inayohusika na misamaha ya kodi, basi nitahakikisha kwamba mambo hayo sasa *CAG* anapatiwa taarifa ili aweze kuyafanyia kazi na taarifa hizo ziweze kuletwa ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya kumi na tatu ilikuwa ni kuimarisha ubora wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Hamza Hassan Juma, na Waheshimiwa wengine nawaomba radhi ambao sitawataja, lakini ushauri tunauchukua na jitihada zinaendelea za kuwaendeleza watumishi wa taasisi hii, ili waweze kutoa ripoti zenye kukidhi matarajio ya Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla. Pia ziwe zina viwango vya kimataifa.

Hoja ya kumi na nne ilikuwa ni kuharakisha kufanyia mapitio sheria ya ukaguzi nambari 11 ya mwaka 2003, ili iendane na mazingira na kwa mujibu wa matakwa ya katiba ya Zanzibar. Mimi hapa nataka niongezee vile vile na kwa mujibu wa makubaliano na mikataba ya kimataifa. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando walielekezea suala hili. Mhe. Naibu Spika, napenda kuwahakikishia kwamba marekebisho haya sasa ya sheria ya ukaguzi nambari 11 ya mwaka 2003, yanaendelea kufanyiwa kazi na sheria hiyo inatarajiwa kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi ndani ya mwaka huu wa fedha.

Suala la nguvu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na adhabu dhidi ya watendaji wa serikali wasiotoa ushirikiano kwa Ofisi ya Mdhibiti, yamezingatiwa na yamefafanuliwa kwa kina katika rasimu ya marekebisho ya sheria nambari 11 ya mwaka 2003 ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, katiba imeeleza nguvu za Mdhibiti lakini sheria itafafanua zaidi, na kwa sababu tunafanya marekebisho, ninachotaka kuwahakikishia Wajumbe kwamba taratibu hizo sasa tutaziweka kwenye marekebisho ya sheria ambayo tutakuja nayo hapa.

Hoja ya kumi na tano ilikuwa ni kuzingatia maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ilizungumzwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Waheshimiwa Wajumbe wengine ambao wamechangia leo, ambao ni Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Naibu Spika, hatua mbali mbali zenye lengo la kuimarisha maslahi ya watumishi wa ofisi hii yamefanyika, ikiwemo kuwapatia posho maalum watumishi wote. Hata hivyo, serikali itaendelea kuimarisha maslahi ya watumishi wote pale hali ya uchumi na mapato ya serikali yatakapoimarika. Lakini tukumbuke kwamba kuna suala la *scheme of service*. Kwa hivyo, maslahi ya wafanyakazi wa *CAG* yatazingatiwa kwa kufuatana na *scheme of service* ambayo tayari imeshapokelewa.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya kumi na sita taasisi za serikali kuharakisha malipo ya ada za watumishi wao wanaosoma katika Chuo cha Utawala wa Umma. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na baadhi ya Wajumbe wamelichangia suala hili. Ofisi yangu itafuatilia kwa karibu zaidi madeni ya wizara na taasisi zinazodaiwa na chuo. Pia nazitaka taasisi hizo kuharakisha ulipaji wa madeni yao, ili kukiwezesha chuo chetu kujiendeleza zaidi.

Hoja ya kumi na saba ilikuwa ni gharama za awali za ujenzi wa chuo kutoendana na hatua iliyofikiwa ya ujenzi. Hoja hii ilichangiwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Ofisi yetu inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili kupata ufumbuzi wa suala hili. Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba mimi rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar, alituagiza tukae wizara mbili ili tujue tatizo hili limetokana na nini na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa, kama kuna mtu amefanya makosa basi tujue makosa hayo ni yepi na hatua gani ziweze kuchukuliwa.

Hoja ya kumi na nane ilikuwa ni usimamizi wa ujenzi wa chuo kuwa chini ya Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma. Hili limeelezwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Ofisi tayari imeunda kamati maalum ya kusimamia ujenzi wa chuo inayoongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mkurugenzi wa chuo, mwanasheria wa chuo na katibu wa baraza la chuo. Aidha, kamati hiyo imeongezewa nguvu kwa kuwajumuisha Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara, Mkurugenzi Utumishi na Uendeshaji, Mhasibu Mkuu na

Mwanasheria wa Wizara. Hoja hii ni ya msingi, lakini lazima muelewe kwamba mimi kutokana na *nature* yangu niliyonayo, kila jambo nataka liwe karibu yangu katika kulisimamia. Kwa sababu mwisho wa siku Waheshimiwa Wajumbe ni nyinyi mtakuja kuniuliza. Kwa hivyo, naomba munipe nafasi libakie chini ya usimamizi wangu, lakini kwa utaratibu wa maelekezo na ushauri wa kamati ambayo inahusisha baraka za chuo, *management* ya chuo na *management* ya wizara, ili mkija kuniuliza niwe na taarifa kamili juu ya suala la ujenzi wa chuo hiki.

Hoja ya kumi na tisa ilikuwa ni kufanya mapitio ya maslahi ya wakufunzi wa Chuo cha Utawala wa Umma. Hili lilielezwa na Mhe. Mwenyekit wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Hatua mbali mbali zenye lengo la kuimarisha maslahi ya watumishi wa ofisi yamefanyika, ikiwemo kuwapatia posho maalum watumishi wote. Hata hivyo, serikali itaendelea kuimarisha maslahi ya watumishi wote pale hali ya uchumi na mapato ya serikali yatakapoimarika, lakini vile vile kwa mwaka huu wa fedha tutazingatia *scheme of service* ya chuo. Hapa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, alitoa mfano wa Chuo cha Fedha na Chuo cha Utawala wa Umma. Yuko mchangiaji mmoja amesema ni vizuri tukayasimamia mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kabla ya kupitishwa sheria nambari 2 ya mwaka 2011 ya utumishi wa umma, kila mtu alikuwa anafanya anavyotaka. Sasa napenda niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba wizara yangu hivi sasa imechukua hatua ya kuzitaka taasisi zote zinazojitegemea na zinazopata ruzuku, lazima zilete utaratibu wao wa malipo na maslahi kwa watumishi wao ili kuoanisha na taasisi nyengine, ili watu wote wawe na kiwango kimoja. Isiwe huyu yatima, huyu ana baba, huyu ana uwezo na huyu hana uwezo.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya ishirini ilikuwa ni suala la chuo kutumia OC, kwa kulipa tofauti ya mishahara ya wakufunzi. Hili lilielezwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mishahara inayolipwa inalipwa katika kifungu cha mishahara na tofauti ya fedha inayolipwa kutoka katika OC ni posho na sio mishahara. Kilichochangia zaidi kulipwa kwa mafao hayo kimetokana na kupunguza makali ya tofauti kati ya maslahi ya Chuo cha Utawala wa Umma na vyuo vyengine.

Kwa hiyo, wizara iliona umuhimu wa kuwapa maslahi zaidi hawa watumishi, lakini tukaona kwenye kasma ya mishahara haitoshi, hivyo tunatumia *OC* zao zile zinazotokana na mapato yao ya ada ndiyo wanayolipwa wanafunzi wa chuo na sio zile *OC*, ambazo ni shilingi milioni 8 kwa kila mwezi zinazotoka Hazina, zile wanatumia kupitia vifungu vilivyokubalika.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma ikae na Tume ya Utumishi wa Idara Maalum, ili kuondoa malalamiko ya kukatwa fedha Wapiganaji wa Vikosi. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala amelisema hili nakumbuka Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na waheshimiwa wengine. *(Makofi)*

Ushauri umepokelewa na Kamisheni kwanza tayari imeshaanza kuchukua hatua kulifuatilia suala hili, lakini ushauri unachukuliwa wa kukutana na tume husika, kwa ajili ya kuzungumzia kadhia hiyo na hatimae kuliondoa kabisa tatizo hili.

Lakini ninalotaka kukuhakikishieni ni kwamba kwa sababu wizara ndio msimamizi mkuu, basi mimi nitahakikisha jambo hili na kadhia hii inaondoka kabisa, kwa sababu sio haki kumkata mfanyakazi bila ya ridhaa yake. Mhe. Naibu Spika, suala la mshahara halina amri ya *command*, isipokuwa suala la kushiriki katika mstari wa mbele kwenye ulinzi ndio lina *command* na suala la mshahara ni haki ya mtu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hoja ya 22 ilikuwa ni hoja ya mgao wa ajira kwa Taasisi za Muungano asilimia 21 kwa Zanzibar na 79 kwa Tanzania Bara kufuata uwiano wa nchi na kupendekeza asilimia 40 kwa Zanzibar na 60 kwa Tanzania Bara. Hili lilizungumzwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
Kimsingi Mhe. Naibu Spika, kuhusu malalamiko umeegemea kwenye maeneo ya kiutawala zaidi, hivyo kigezo cha uwiano wa Majimbo ya Uchaguzi ya Wabunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho kigezo kilichotumika kupata asilimia ya mgao. *(Makofi)*

Kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wawakilishi tulikuwa na mjadala mpana sana, hatua ya mwanzo wenzetu walitaka tuchukue *population*, walipotaka tuchukue *population* ya watu wa Zanzibar na Tanzania Bara tulijikuta tuko katika asilimia ndogo sana.

Kwa hivyo, kwa hekima kubwa na busara tukang'ang'ania eneo hili la kiutawala na tukaona ndilo litakalotupa nafasi ya kuweza kupata kiwango kikubwa zaidi kiasilimia na kuliko kile cha *population* ya idadi ya watu.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waridhike na kiwango hiki, kama mmesikia idadi ya nafasi ambazo zimetangazwa na Ofisi ya *Management* ya Utumishi wa Umma kwa mwaka huu, ukizichukua zile Taasisi za Muungano, basi inawezekana hata zile nafasi tulizozitenga sisi hapa za ajira zikawa ni kidogo kuliko zile tutakazozipata kule. Kwa hiyo, kwa kuanzia tumehisi tuanze hapa. *(Makofi)*

Kwa msingi huo jumla ya majimbo 239 ni asilimia 100 kwa Tanzania nzima. Majimbo ya Tanzania Bara ni 189 kwa hivyo yanachukua asilimia 79 na majimbo ya Zanzibar ni 50 yanachukua asilimia 21 na mgao huu unatarajiwa kutumika hivi sasa katika mwaka wa bajeti huu unaoanza sasa.

Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa mjadala wa Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mwakilishi na wananchi kwa jumla watumie fursa hiyo kuwasilisha maoni yao kwenye Tume ya Katiba.

Lakini kwa hivi sasa bila ya kusubiri mabadiliko ya Katiba tutakwenda na mgao huo ambao tayari tumekubaliana. Mhe. Naibu Spika, makubaliano hayo tumesaini *Memorandum of Understanding* kwa ajili ya mambo haya na wala hatukwenda kibaba, isipokuwa tumekubaliana kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hoja ya 23 ilikuwa ni mchakato wa kuwapata wanafunzi waliopelekwa katika Chuo cha Diplomasia kufuata utaratibu ulikuwa wa upendeleo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala la ujomba na ushangazi lilitumika.

Utaratibu uliotumika ni kufanya usaili kwa waombaji, ambapo jumla ya vijana 35 walisailiwa katika awamu ya mwanzo na vijana 8 walifaulu, katika awamu ya pili vijana 34 waliosailiwa na vijana 10 walifaulu.
Usajili huo ulisimamiwa na Mkurugenzi na Rasilimali Watu Wizara ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa, Mkurugenzi wa Taaluma Chuo cha Diplomasia, Muhadhiri wa Chuo cha Diplomasia, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Zanzibar na Mkurugenzi Mipango Rasilimali Watu Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kati ya hao waliofaulu 13 ni wanaume na 5 ni wanawake. Wanawake wa fani waliyosomea ni *Management for Foreign Relation and Economic Diplomacy*. Katika vijana hao 17 wanaendelea vizuri na mafunzo yao ya awamu ya mwisho na mmoja hakufanikiwa kuendelea na mafunzo.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa kwamba hakukufanyika upendeleo wa mtoto wa mjomba, kama kigezo ni kuwepo mtoto wa mjomba na shangazi, wapo vijana wa Tumbatu waliomba nafasi hizi, lakini kwa sababu kulikuwa na usaili na waliomba wana *qualification* sawa sawa hawakufikia vile vigezo na hawakwenda. *(Makofi)*

Sasa kama wa Waziri hakwenda sidhani kama kuna mwengine alipeleka kinyemela. Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuwahahikishia Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba hapa hapakuwa na upendeleo uliofanyika.

Mamlaka ya Rushwa kutengewa fedha kidogo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Salmin Awadh Salmin, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Abdi Mossi Kombo walichangia. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya uanzishwaji wa mamlaka na tunategemea watumishi wengi wa taasisi hii watatoka katika taasisi za umma, ambapo tayari makisio ya mishahara yao imeshaingizwa katika wizara na taasisi husika. Kwa hivyo, zile fedha za pale ni kwa madhumuni ya uendeshaji wa kazi.

Hata hivyo, wizara yangu imepokea ushauri wa Wajumbe wa Baraza na *concern* yao ya kuona pengine fedha hizi ni kidogo kulingana na kazi kubwa ambayo inatarajiwa ifanywe na taasisi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kadri itakavyotokezea hakuna jambo litakalokwama, kwa sababu kutakuwa na kazi inafanyika na ndio maana kuna miradi ambayo tumeipendekeza ,na bahati nzuri imepokelewa na Wizara ya Fedha, mmoja wa kuimarisha Taasisi hii ya Rushwa kama mtasoma vizuri kwenye hotuba yangu nimetaja mradi unaohusiana na Kitengo hiki cha Rushwa. Kwa hivyo, pale itakapotokezea kwamba kuna haja ya kuongeza mafungu, basi taratibu za kisheria zitafuatwa, ili tuweze kuongeza mafungu hayo.

Hoja ya 25 ilikuwa ni kuhusu walimu wa *science* walioajiriwa hivi karibuni 240 hawatoshi. Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala hili amelizungumza. Ni kweli walimu hawatoshi, lakini serikali kwa kulijua hili imetoa fursa kwa walimu wa *science* kuajiriwa wakati wowote.

Hivyo, tunamuomba Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine waliopo hapa ambao wamelizungumza suala hili kama wanao walimu wa *science* waniletee niwaajiri sasa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kibali tulichokitoa cha walimu wa *science* ni walimu 500, lakini hawakujitokeza, inawezekana kutokana na zile sababu ambazo Waheshimiwa Wajumbe tokea asubuhi mmekuwa mkizisema za pengine maslahi madogo nayo hayo tutayazingatia.

Pamoja na hayo, walimu wa *science* wanatafautiana katika kulipwa mishahara yao na walimu wa *art*, hilo serikali imelifanya katika kipindi kilichopita. Lakini ushauri tunauchukua ili tuone tunawalinda vijana wetu wanaosomea *science* na tutatengeneza mazingira mazuri ya kutaka watu washawishike na kusoma *science*, badala ya kusoma art zaidi kutokana na mahitaji ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya 26 ilikuwa ni watumishi waliostaafu wana sifa gani hata wamerejeshwa kazini, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine. Watumishi waliostaafu na kupewa mikataba wana sifa tofauti kwa mujibu wa taasisi wanazofanyia kazi, na jumla yao ni watumishi watano.

Mhe. Naibu Spika, kama watakumbuka Waheshimiwa Wajumbe suala hili nililijibu juzi, nendeni kwenye *Hansard* ya majibu yangu nilitaja mpaka taasisi. Sasa jambo hili halijafika hata miezi mitatu naulizwa tena. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub akatafute *Hansard* ya majibu ya juzi, atapata idadi pamoja na sehemu gani watu wamepelekwa kwa sababu ya kuokoa muda.

Kwa faida ya Baraza hili nilisema kwamba watu hao walioajiriwa ni mtaalamu wa uandishi wa Hotuba za Mhe. Rais ambaye ni mmoja, Wahadhiri wa Chuo cha *SUZA* wawili na wataalamu wa afya wawili, mmoja Chuo cha Afya na mwengine alipelekwa Hospitali ya Kivunge.

Waheshimiwa Wajumbe, mnakumbuka kwamba wananchi wa Wilaya ya Kaskazini hivi karibuni walifanya maandamano kwa ajili ya kutaka mtaalamu wao apewe nafasi ya kuajiriwa. Sasa unapokuwa huna mtaalamu katika eneo ndipo unapolazimika kumuajiri mtu kwa mkataba kwa yule ambaye ameshastaafu kwa kutimiza umri wa lazima.

Kuhusu orodha ya mikataba ya watumishi hawa namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma afike ofisini kwangu, ili nimpatie mikataba na orodha aliyoiomba na Mhe. Mjumbe mwengine yeyote niko tayari kuitoa, kwa sababu hakuna siri wala cha kuficha. *(Makofi)*

Hoja ya 27 ilikuwa Kanuni za Utumishi wa Umma kwa nini zimechelewa na hazikuzungumzwa kwenye bajeti, na suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Kwa kweli Rasimu ya Kanunni za Sheria ya Utumishi wa Umma imekamilika na hatua inayofuata ni kuziwasilisha katika Kamati ya Makatibu Wakuu, ili kupata maoni yao.

Kwa hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa kanuni hizo zitakuwa tayari ndani ya mwaka huu. Mhe. Naibu Spika, suala hili pia nililitolea majibu, niliulizwa swali na nilitoa majibu, labda pengine Waheshimiwa Wajumbe wanasahau.

Lakini kwa nini tunaipeleka kwa Kamati ya Makatibu Wakuu, kwa sababu hizi ni Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma, kwa hiyo kila mmoja anatakiwa atoe maoni hasa wale watendaji wakuu wa serikali. Kwa maana hiyo, zitakapokamilika na tunategemea katika mwaka huu wa fedha tutaziwasilisha au zitaanza kutumika rasmi.

Mhe. Naibu Spika, hoja ya 28 kwa nini walimu wamekatwa mishahara ghafla kufuatia Zoezi la Ukaguzi wa Watumishi na Mishahara, fedha zilizokuwa walipwe mishahara yao zimerejeshwa wapi na idadi gani ya walimu hao. Suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Abdalla Juma Abdalla pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine, nakumbuka lakini kwa sababu ya muda imeshindwa kuwaorodhesha.

Waliokatwa mishahara si walimu tu, isipokuwa ni wafanyakazi wote waliotoa taarifa zisizokuwa sahihi wakati marekebisho ya mishahara ya mwezi wa Oktoba, 2011. Idara ya walimu ambao wamekatwa mishahara Pemba walimu 125 na Unguja walimu 432, na fedha hizo zimebakia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, msisahau mnatuhimiza hapa kwamba fedha za serikali zinaliwa. Sasa nilichoamua na hawa wameanza kuchukua fedha hizi katika miezi mingi ya nyuma iliyopita, lakini kwa sababu tumegundua katika kipindi hiki tumesema maamuzi ya serikali yatatolewa baadae kuhusu hatua gani itachukua. *(Makofi)*
Lakini mimi nilichochukua hatua kwa watumishi wote ambao taarifa zao si sahihi ni kusema unazipunguza zile fedha ambazo hawastahiki, na wale wafanyakazi ambao hawaeleweki mishahara yao ina-*block* mpaka ujue taarifa zao. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa hili tushirikiane, kwani hapa kunahitajika maamuzi magumu, kwa sababu ni nyinyi ndio mnaosema na mimi nimefarajika sana na michango yenu, na huko mbele baadae nitasema. Kwa mfano, mafunzo mliyoyapata na mnavyotuchezesha hapa kibatawata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nataka nikuhakikishieni kwamba na mimi nimekulia ndani ya Baraza hili, ujasiri huu nimeupata humu ndani. Sasa mkiniambia anayechukua fedha za umma asichukuliwe hatua sitawaelewa hata kidogo, na hilo kwangu mimi halina *compromise*. Mhe. Naibu Spika, hii ni rasha rasha tu masika bado. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe kwa hapa niachieni nichukue maamuzi magumu na nyinyi mvumilie. *(Makofi)*

Lakini ninachoweza kukuhakikishieni kama kuna mtumishi ambaye *Scheme of Service* yake tokea mwanzo hasa walimu, ambayo ilishakubali kwamba alipwe kiwango hiki, lakini kwenye kuweka cheti akafanya udanganyifu, basi tutaheshimu maamuzi ya *Scheme of Service* ambayo imekuja kabla ya marekebisho ya mishahara, na tutafuatilia kwa umakini zaidi, kama wamo walimu wa namna hiyo basi tutaheshimu.

Kwa upande wa wale ambao wamedanganya vyeti, basi hakuna *compromise* na huu ndio uwazi na utawala bora, pia mumeniambia kwamba nimepewa majukumu makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwa wale ambao walichangia suala la kuuangalia utendaji wa serikali nzima, basi hilo nitalivalia buti, maana ndivyo tulivyokubaliana na wala hakuna hofu katika hili. Kwa kweli nilikuwa nikisubiri nondo, ili zinipe uwezo wa kufanyia kazi, hivyo nondo tayari, sera tayari, muongozo tayari kwa hiyo nitafanya kazi niaminini. *(Makofi)*

Hoja ya 29 kuhusu kuwepo kwa watumishi wenye muda mrefu kulipwa mishahara midogo kwa kisingizio cha kutokuwa na elimu. Suala hili limezungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.

Katika upandishaji wa mishahara mipya kila mtumishi alifaidika na upandishaji wa kiwango cha mishahara kwa mujibu wa stahiki zao. Hata hivyo, serikali imeliona hili na inalifanyia kazi na jibu litapatikana kwenye *Scheme of Service*, tutazingatia hivyo na wale waliokuwa hawana elimu kubwa, kwa sasa kuna mambo mengi na kama mtakisoma hiki kitabu changu kinachozungumzia upimaji wa watumishi kupandishwa vyeo na mambo mengine. Kwa hivyo, nadhani tustahamili katika mwaka huu wa bajeti tutaanza kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika na hoja zilikuwa nyingi, naomba nitoe ufafanuuzi na mnivumilie, ili kupunguza kuja kusema mtu kwamba sikumjibu na nimefanya hivi makusudi, ili kuwe hakuna hoja na haidhuru hiyo ni jukumu lenu kuweza kuona kama nimejibu au sikujibu, lakini najitahidi kadri ya uwezo wangu. *(Makofi)*

Hoja ya 30 kuhusu Idara ya Mipango na Rasilimali Watu na Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu, kwa nini haziunganishwi wakati zinafanya majuku yanayofanana, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Zoezi la Kupitia Majukumu ya Wizara na Taasisi za Serikali, linatarajiwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha, kukamilika kwa zoezi hilo ndipo tutakapoweza kupata taarifa za kitaalamu juu ya miundo halisi ya taasisi za serikali, zikiwemo hizi idara na wala si idara hizi tu, isipokuwa ni taasisi nyingi zilizopo serikalini wizara yangu ina jukumu hilo la kupitia miundo ya taasisi, je hakuna taasisi ambazo majukumu yake yanafanana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe astahamili.

Hoja ya 31 hakuna uratibu mzuri wa kutathmini mahitaji ya rasilimali watu baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Mhe. Naibu Spika, kupitia *Program* ya Kitaifa ya Kujenga Uwezo, ofisi imepanga kufanya tathmini ya mahitaji na uwezo wa rasilimali watu, utakaoainisha mahitaji ya rasilimali watu ya sasa na ya baadae. Matokeo ya ripoti hiyo yataonesha maeneo yenye ziada au upungufu na kuweka mikakati ya kuyafanyia kazi.

Hoja ya 32 kuhusu *GSO* inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufuata mirengo fulani ya kisiasa, vijana hawaajiriwi kwa sifa, wizara haina kauli ya mwisho juu ya ajira na bado *GSO* ndio muamuzi wa mwisho, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Seif Suleiman. Ofisi ya *GSO* inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 kifungu cha 78 kama kilivyoelezwa.

Lakini ninachotaka kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba, *GSO* inafanya upekuzi (*vetting*) haiajiri na wala wao sio waamuzi wa mwisho, isipokuwa wao wanaishauri Tume ya Mamlaka ya Ajira, juu ya wale watu walioomba ajira nani ana sifa zipi, nazo zaidi hizo kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu si za kielimu peke yake na wala ya kisiasa haimo katika hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka tuihukumu *GSO* baada ya sheria mpya kupita, kwa sababu humu ndani ya bajeti yangu nimesema kwamba ajira katika kipindi hiki tulizozitoa ni ajira za walimu 240 tu na wala hizi hazikwenda kisiasa. Kwa kweli mimi nakubali kwamba huko nyuma kulikuwa na changamoto, sasa huko tukuache na tuende na sasa hali ikoje. Kwa maana hiyo, sasa lazima tutafuata taratibu na sheria na maana ya mageuzi ndio hayo. *(Makofi)*

Sasa kwenye bajeti yangu humu sheria imeanza kusainiwa Julai na imeanza kufanya kazi Julai. Kwa hivyo, tuangalie kutoka Julai, 2011 ni watu wangapi wameajiriwa na wapi wamepelekwa kwa upendeleo.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, wengine wengi kama walivyosema wachangiaji wengine wamepewa vibali na *GSO* tumepeleka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wala hawakuripoti katika vituo vyao vya kazi, lakini si kwa sababu ya misingi ya kufuata mirengo au namna gani na wala hilo halipo. Nadhani katika kipindi hiki ambacho mimi ni Waziri hilo halipo.

Hoja ya 33 kuhusu mtumishi wa Wizara ya Afya aliyesimamishwa kazi, suala hili alilizungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mramu wangu, lakini hayupo. Kwa kweli suala hili tayari limeshapatiwa muafaka baada ya kukutana naye ana kwa ana, na kukubaliana juu ya hatua za kumrejesha kazini pamoja na kumlipa haki zake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama watakumbuka Waheshimiwa Wajumbe kwamba swali hili Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aliniuliza kwenye swali la nyongeza, na tukakubaliana hapa kwamba mlete ofisini. Kwa hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba mfanyakazi huyo tayari nimeshaonana naye pia tumeshauriana na Mhe. Mwanasheria Mkuu, na hatua za kumlipa haki zake zitafuata mara tu baada ya mwaka huu wa bajeti. *(Makofi)*

Suala la mishahara ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na Uhuru wa Tume ya Utumishi ya Mahakama. Kwanza suala hili la Uhuru wa Tume ya Utumishi ya Mahakama Mhe. Mwanasheria Mkuu amelieleza vizuri sana, pamoja na tume nyengine ambazo zilichangiwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Hamza Hassan Juma rafiki yangu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kila Tume ya utumishi ina uhuru wa kutekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria. Kwa upande wa mishahara wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo suala hili linaendelea kufanyiwa kazi, na katika hatua za awali mahakimu hao wamepatiwa posho maalum, ili kuondosha zile tofauti kubwa ziliopo kati ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na wale Mahakimu wa Wilaya.

Wakuu wa Mikoa na Wilaya kufanya kazi zao kisiasa zaidi, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Asha Bakari Makame. Mhe. Naibu Spika, suala hili nataka niseme kwa ufupi kwa mujibu wa Katiba Wakuu wa Mikoa na Wilaya si wanasiasa, isipokuwa ni watumishi wa umma, naomba niishie hapo.

Hoja ya 36 wananchi kutokuwa na uelewa wa kutumia *computer*, je wizara imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi katika huko tunakoingia kwenye *E – Government*, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Mhe. Naibu Spika, ufafanuzi wake ni kwamba katika mikakati iliomo kwenye *E – Government* ni kuwahamasisha wananchi juu ya matumizi ya Serikali Mtandao. *(Makofi)*

Hoja ya 37 walimu wa *science* wanakimbia kwa sababu ya maslahi madogo, Mhe. Abdalla Juma Abdalla pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine wamelizungumzia hili. Serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri kwa watumishi wake ikiwemo walimu wa *science*. Hata hivyo, serikali itaendelea kuimarisha maslahi ya watumishi wake wote ili waendelee kutumikia taifa lao.

Hoja ya 38 kuhusu maslahi wa watumishi wa Baraza la Wawakilishi yaendane na hadhi ya chombo chenyewe, suala hili lilizungumzwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Mhe. Naibu Spika, katika kupanga maslahi ya watumishi serikali huzingatia usawa badala ya hadhi ya chombo husika, na kutofanya hivyo ni kujenga matabaka katika utumishi wa umma.

Kwa hivyo, tunachotaka tusijenge matabaka, ni kweli kuna mazingira na hilo tunalikubali, kwa sababu hata ukiangalia tofauti ya mishahara kati ya watumishi wa chombo hiki na watumishi wengine ipo kidogo lazima tuseme kweli. Lakini hatutafikia pahala tukianza kujenga matabaka makubwa katika nchi moja, ambapo fedha hizi na rasilimali hii yote inatoka katika kodi ya wananchi wale wale.

Tutajitahidi kuweka mazingira na kuzingatia katika kulipa posho zaidi ili watumishi hawa kuzingatia yale mazingira yao magumu ya kazi. Lakini ukisema kwamba mamlaka hii mishahara yao iwe na tofauti na mamlaka hii ndio pale inapokuja tunapata tabu. Tunajibu suala la wahasibu hapa na watu wengine wenye sifa. Tunaogopa kufanya hivi kila mmoja akaja na lake.

Ushauri tunaukubali lakini inabidi tuufanyie kazi vizuri zaidi ili tusije tukajenga mambo mengine. Tukianza kwa Baraza la Wawakilishi na wengine watakuja. Mfano nyinyi wenyewe mmeieleza hapa. Walianza Chuo cha Fedha, Chuo cha Habari, Chuo changu cha Utawala wa Umma na wao wanasema kwa nini na sisi tusiwe kama hawa.

Mhe. Omar Ali Shehe, kutolewa ripoti ya utendaji wa serikali na utawala bora. Sheria ya Utumishi wa Umma kifungu Nam. 15 na 28 pamoja na mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Utawala Bora vinaelekeza kutolewa kwa ripoti ya utekeleza wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo kufuata misingi hiyo ya sheria ni msisitizo alioutoa Mhe. Mwakilishi wa Afisi yangu. Afisi yangu itahakikisha kwamba ripoti hizo zinatayarishwa na zinatolewa.

Mhe. Hamza Hassan Juma, traratibu ya migomo katika kazi zimezingatiwaje katika sheria zetu. Nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu amefafanua vizuri. Kwa kuokoa muda nadhani hili liniache. Amefafanua katika sheria Nam. 1 ya Mawasiliano Kazini ya mwaka 2005 kifungu cha 62 na 67 kimetoa haki na utaratibu wa kugoma, kama alivyoeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, kufanya tathmini ya watumishi wanaopata mafunzo kuona kwamba yana tija. Ushauri tunaupokea na tutafanya kazi hiyo katika kipindi hichi cha mwaka wa fedha huu tunaoendelea nao. Mhe. Mgeni Hassan Juma, kila Wizara kuweka utaratibu maalumu wa kusikilizwa maoni ya wananchi juu ya utekelezaji wa majukumu ya tasisi husika. Ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) kuendelea kuwapatia mafunzo Wajumbe wa Kamati ya PAC ili kuwaongezea uelewa wa dhana nzima ya ukaguzi na udhibiti wa rasilimali za taifa. Nafikiri yeye anajua kwamba hilo tunalifanya na tumekuwa tukitoa mafunzo hayo kwa Kamati na kila hali ya kifedha itakaporuhusu tutaendelea kufanya hivyo. Ndani ya uchambuzi hata ile bajeti ya PAC imewekwa kwa kutambua hilo. Kwa hivyo tutaliendeleza tu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando), aliuliza serikali inachukua hatua gani juu ya ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na suala la Ajira. Ndugu yangu hapa nataka nidokeze kidogo tu. Ripoti hiyo imepokelewa serikalini inaendelea kufanyiwa kazi. Mara tu itakapokamilika Baraza lako tukufu litaarifiwa. Nataka nihakikishe Baraza lako tukufu kwamba kila aliyetajwa, kila taasisi iliyotajwa imetakiwa kutoa maelezo ya kina ili Baraza hili tukufu lije litoe taarifa iliyokamilika. Kwa hivyo Mheshimiwa ndugu yangu nadhani stahamili kidogo si muda mrefu taarifa hizi zitaletwa hapa Barazani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kuhusu asilimia ya fedha zilizopatikana kwa kila Idara na Taasisi. Namuomba Mhe. Jussa angalie kiambatanisho Nam. 8 ukurasa wa 91 na 93, asilimia tumeziweka mle kwa zile pesa ambazo tumezipata. Lakini kama pengine ulikuwa na maana nyengine nitaomba radhi unaweza ukanipa hapo ili niweze kukuelewa zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mgeni Hassan Juma majina ya vifungu vilivyotumika katika kitabu cha Bajeti vipo kwa mujibu wa muongozo uliotolewa na Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Utaratibu huo umo katika *programme* inayoandaa kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali na Wizara nyengine yoyote haiwezi kukipa jina kifungu zaidi ya lile, jina limo katika *programme*.

Ninachotaka kusema katika hili ambalo limezunguzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza kansani ya Wajumbe mimi nimeiyona na ina mantiki, lakini hapa ukibadilisha hichi kifungu, ukenda kwenye ule MTEF unatoa ufafanuzi. Kwa mfano suala la ununuzi wa "FRIJI" kuna *items* nyingi pale zimetajwa katika ununuzi wa zile friji, ukibadilisha ukitaja kama Mheshimiwa Swahibu yangu juzi alivyoletewa ile jenereta ukija sasa unataka *request* ya kutumia *programme* inakataa.

Mimi dhamira nimeielewa na naikubali lakini kwa mwaka huu wa fedha nitawaomba sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba jambo hili tulifanyie kazi. Yale maoni kwamba ni vizuri angalau Kamati za Kisekta zikapata uchanganuzi kabla. Mimi nalichukua kwa sababu mimi ndio mtu wa Utawala Bora basi nawahakikishia nitalifanyia kazi. Kwamba lazima Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawe na uwelewa. Hivi tulivyoweka kwa jumla jumla ni lazima hapa tutachezewa kibatawata.
Hii kibatawata ni ngoma moja Tumbatu, inachezwa kwenye nyakati fulani fulani. Wajumbe kutuchezea kibatawata ni haki yenu kwa sababu mnashindwa kupata taarifa sahihi juu ya matumizi. Hili litajitokeza katika kila Wizara lakini tukenda kwenye ule MTEFU mtakuta. Kwa mfano kwenye ofisi yangu kule nitakuja kusema. Naomba kwa heshima zote kwamba hili jambo mturuhusu tulifanyie kazi. Buku hili lilivyo kweli lina mapungufu na linahitaji kufanyiwa mabadiliko katika mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, wapo wajumbe waliokuwa wanadhani katika bajeti zilizopita kwamba kuwa na *draft* ya mwanzo, kuwa na marekebisho na kuwa na *items* moja moja kama wanavyofanya wenzetu. Nafikiri hatutofanya dhambi tukiiga mambo mzuri. Kuiga mambo mabaya ndio dhambi lakini kuiga mambo mazuri sio dhambi. Naamini kwamba elimu hii nilioipata naithamini na mimi nimefarijika sana.

Niliombe Baraza la Wawakilishi kwamba na sisi pengine Waheshimiwa Mawaziri, tungeshirikishwa kwenye elimu hii pengine tungekuwa na uelewa sawa na wanavyoelewa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo kwa sababu na sisi ni Wawakilishi msitunyime jamani, mtushirikishe. Mambo mazuri yasende kwa watu nusu, yende kwa watu wote.

Mimi najinasibu sana kwa ujasiri wangu, kujiamini kwangu, nimepata uzoefu ndani ya Baraza hili. Mimi sikushangaeni mnaposema hayo, mimi najikumbusha yale niliyokuwa nikiyafanya mimi na nyinyi ni haki yenu. Lazima tukubaliane kwamba kama kuna mambo kimfumo yamekosewa basi ukiihukumu Wizara unaweza ukapata matatizo katika utendaji. Tunaweza tukajishtukia tunarudi kulee tulikotoka kwamba asilimia ya fedha zilizoingizwa katika Wizara ni asilimia 70. Asilimia ya kutendea kazi ni asilimia 5.

Mhe. Naibu Spika, tukirudi huko nadhani vile vile Baraza hili litakuja kutuhukumu, pesa hizi mnazilipa mishahara hao wafanyakazi wanaolipwa wanafanya nini, wame *achieve* kitu gani. Mimi kwa hili sijui nisemeje, lakini kama ingelikuwa kwenye yale majukwaa ya kuomba kura basi ningetafuta lugha ya kusema nikaomba ili hili jambo likawa *release* na Baraza la Wawakilishi. Makosa yapo katika mfumo hili lazima tulipe hatua ya utekelezaji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, sare kwa watumishi wa umma. Suala hili tumelichukua na ni jambo zuri sana. Nafikiri tutalifanyia kazi, kwa sababu sisi ndio tunaotoa miongozo na matoleo ya watumishi. Tutahakikisha kwamba iwepo sura ya kiutumishi utumishi. Wazo lako ni zuri na tutalifanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, suala la uwiano wa watumishi na idadi ya watu. Kutokana na kuwa na sekta binafsi ambayo haijaweza kukua na kuajiri vijana wengi. Serikali inalazimika kuendelea kutoa ajira kwa wananchi wake. Aidha Serikali inaendelea kuwaajiri kutokana na mahitaji halisi iliyopo. Wizara ya Kazi hapa itakuja kueleza

mikakati yake. Itakapokuja na wakati sekta binafsi itakuwa imeshaimarika katika kuchukua ajira, mimi nadhani hatua kwa hatua tutaiona. Mzigo uliopo serikalini utakavyokuwa unapungua hatua kwa hatua.

Mhe. Panya Ali Abdalla, tarehe za kuanza kutumika sheria ya rushwa. Kwa mujibu sheria iliyosema sheria hiyo itaanza kutumia siku iliyotiwa saini na Mhe. Rais. Kwa mnasaba huo mtu yeyote atakayeshtakiwa kwa makosa haya hivi sasa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria iliyopo. Kama mnavyojua kwamba Sheria hii tayari ipo lakini kinachofuata ni kuunda taasisi. Nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe muidhinishe bajeti yangu, baada ya kuidhinisha bajeti hii saa yoyote Mhe. Rais atachukua hatua za kufanya majukumu yake na sisi kama Wizara tutachakua hatua ya kuweza kuunda hii taasisi ili sheria hii iweze kufanya kazi mara moja.

Walimu waliopunguziwa mishahara zaidi ya kiwango walichokuwa wakipata kabla ya marekebisho. Hii inajirejea, wameizungumza Waheshimiwa wengi. Ikiwa tatizo hilo lipo tunawaomba walimu waripoti haraka kwa marekebisho. Alikuwa anatusaidia, ni kweli kama yupo mwalimu anahisi hakutendewa haki katika hili zoezi la kuzuia, basi tunamuomba atumie utaratibu uliopo alete malalamiko yake na malalamiko yake yatashughulikiwa.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali, ripoti ya zoezi la ukaguzi wa wafanyakazi na mishahara. Ripoti kamili ya mambo yaliyobainika itawasilishwa baadaye. Hatua za awali kwa wafanyakazi ambao hawakujitokeza katika zoezi la ukaguzi zimechukuliwa kwa kuzuia hadi hapo zitakapotolewa taarifa.
Mhe. Abdalla Mohammed Ali na Mhe. Mohammed Haji Khalid, jumla ya maombi ya nafasi mpya 6,817 za ajira yaliyowasilishwa. Nafasi 3,356 ziliidhinishwa na nafasi 2,552 zimekubaliwa. Nini tafsiri yake.

Mhe. Naibu Spika, maombi yaliyowasilishwa kutoka katika Mawizara ni 6,817. Baada ya majadiliano ya nafasi zilizoidhinishwa, maana mawizara yanapoomba yanakuja kutetea uwajiri huu kwa mujibu wanavyoona mahitaji yao. Kama taasisi nyengine yoyote inavyokwenda Wizara ya Fedha kutetea bajeti na suala la watumishi na ajira mpya nao huwa wanakuja kusema sisi mahitaji yetu ni haya. Kunakuwa na majadiliano ambayo yanazingatia vigezo vya nafasi. Nafasi tulizozikubali kwamba hizi zinaweza zikaajiriwa zilikuwa ni 3,356. Kutokana na uwezo wa serika kifedha katika bajeti ya mwaka huu basi nafasi zilizokubaliwa ni 2,552, hii imetokana na uwezo tulionao.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, elimu ya Uraia kutolewa Unguja tu na kutokutolewa kwa upande wa Pemba. Tunachotaka kumuhakikishia Mheshimiwa elimu pia imetolewa kwa upande wa Pemba angalia katika ukurasa wa 30, kifungu cha 69.
Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, usumbufu wa mshahara kwa wafanyakazi imechukua mwaka mzima kushughulikia. Suala hili litamalizika baada ya kumaliza mapitio ya taarifa za kielimu za wafanyakazi zikilinganishwa na uzoefu wao. Hizi ni kazi zetu za msingi katika Wizara ya Utumishi wa Umma kupitia taasisi zake mbali mbali. Hii si kazi ambayo itaisha siku moja, tutaendelea nayo. Lakini kwa pale ambapo tutakuwa tumejiridhisha ndio pale tutakapoweza kutoa taarifa ya idadi ya watu ambao wamegundulika.

Hoja ya mwisho ilikuwa kuhusu posho kwa mashirika na taasisi zinazojitegemea zinapangwa kiholela. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alilisema hili na Mhe. Asaa Othman Hamad alilisema hili. Nafikiri nimeshatoa ufafanuzi, suala linashughulikiwa kwa kuanzia tumewataka Wizara, Mashirika na taasisi zinazojitegemea kuleta taarifa za malipo ya mishahara na maposho pamoja na miundo ya utumishi yao ili tuweze kuifanyia kazi haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja za mafungu ambazo zimeulizwa, nazo naomba nitoe ufafanuzi mbali na ile niliyoitoa ya jumla lakini naomba niongeze kutoa ufafanuzi.

Idara ya Utawala Bora fungu 311205 kifungu cha Ununuzi wa Friji, kifungu hichi ni kwa ajili ya ununuzi wa mambo yote yanayohusiana na mafriji, PA *system*, kutokana na kifungu maalum cha ununuzi wa jenereta matumizi yake yanaonekana hapa. Yaani wajumbe wametushauri sana hapa tutoe elimu, tutoe taaluma. Hivi sasa Idara yetu ya Utawala Bora inapokwenda Vijijini kutoa taaluma tunakodi jenereta, tunakodi PA *system*, tunakodi kila kitu.

Kwa hiyo kifungu hiki kwa sababu zile nilizozisema mwanzo kwamba ni *program* ambayo tayari ipo kule kwenye mfumo wa malipo. Lakini ukenda kwenye MTEF unapata ufafanuzi wa *items* ngapi ambazo zitatumika katika kifungu hiki. Naomba sana kama nilivyoomba waheshimiwa wajumbe waone kama hili jambo tutaweza kulifanyia kazi vizuri na kulifatilia.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wajumbe wamesema kama kuna friji nyengine imejirejea. Hapa inahusisha masuala ya ununuzi wa AC na vitendea kazi vyengine kwenye hii Idara ya Utawala Bora. Ukenda kule kwenye MTEF kwenye *item* moja moja unakuta hii, kwa hiyo uchambuzi wake unapatikana kwenye MTEF.

Idara ya Miundo ya Taasisi kifungu cha 220401 Gharama za Petrol, gharama za mafuta zimepungua kutokana na upungufu wa *activities* zinazofanywa nje ya Ofisi, kwamba mwakani tunategemea *activities* zitakazofanywa nje ya Ofisi zitapungua. Ndio maana gharama zimeshuka.
Afisi Kuu Pemba Kifungu cha 220501 kifungu cha Vifaa vya Kuandikia. Shughuli za Idara zote za Unguja ambazo zinatakiwa kufanyika Pemba fedha zake zimetengwa Ofisi Kuu Pemba. Hivyo gharama za vifaa vya ofisi, chakula na vinywaji zimeongezeka. Hapa hapa Baraza hili limetuhimiza kwamba Pemba tusiwaache nyuma, tumezingatia hayo Waheshimiwa Wawakilishi.

Kifungu 311207 Kifungu cha Ununuzi wa Kompyuta. Kifungu hichi fedha hizi zinatarajiwa kulipia deni la kompyuta 7 pamoja na ununuzi wa compyuta 3. Watu wengine wameuliza hapa hizo kompyuta kila mtumishi. Kwa kweli uwezo ukiwepo kila mtumishi anatakiwa awe na kompyuta, mambo yanabadilika. Tulizowea kwamba kompyuta inakaa kwa Katibu Muhtasi tu wa kiongozi. Utaratibu wa sasa inatakiwa kila mtumishi awe na kompyuta na Baraza hili hili limetuhimiza tumejipangaje katika suala zima la kuingia katika serikali mtandao.

Kifungu 220401 Gharama za Petroli, shughuli ambazo zinatarajiwa kufanyika nje ya ofisi zimepungua ndio ikaonekena kupungua kwa gharama za mafuta. Kama nilivyosema katika kile kifungu chengine.

Idara ya Mipango sera na Utafiti. Kifungu cha Miradi ya Maendeleo kuwekwa kwenye Mipango Sera na Utafiti. Hapa wamesema kifungu hiki kikubwa kimewekwa katika Idara ya Mipango, katika mgawanyo kimewekwa katika Idara mbali mbali. Idara ya Mipango Sera na Utafiti ndio yenye jukumu la kuratibu shughuli zote za maendeleo ya Wizara. Katika kitabu cha hotuba ya bajeti, idara husika ndio imeeleza utekelezaji wa shughuli zake.

Hapa tunaweka kwamba Mkurugenzi Mipango au Katibu Mkuu ajue kwamba hili fungu la maendeleo limewekwa kwa madhumuni katika kila idara. Ili isijeikatokezea idara hii imepewa kisichostahiki na idara hii imenyimwa kinachostahiki. Kwa hivyo Idara ya Mipango ni kama msimamizi, lakini kila idara inajua fedha zake za maendeleo ni *amount* hii. Kule Idara ya Mipango katika kuweka fungu kubwa ni kwa sababu yeye ni msimamizi tu.

Kifungu 22 kifungu cha Huduma Mtandao wa Serikali, yaani *e-government*. Kwa sasa Idara hii haijaundwa na imeshauriwa fedha zake za utelezaji wa shughuli ziwekwe katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa hivyo fedha zake zipo na itakapoundwa tutaipa fedha hizi. Tumefanya hivyo kwa busara zetu sisi wenyewe, kwa sababu kwa kweli tulipokwenda kupeleka maombi yetu tuliambiwa mafungu yameisha. Sisi wenyewe tumesema basi katika fedha za Mipango Sera na Utafiti ni lazima tutenge fedha kwa ajili ya Idara hii ya Mtandao.

Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa, Kifungu 331214 Kifungu cha Ununuzi wa *Television*. Fedha hizi zinatarajiwa kutumika pia kwa ununuzi wa CCTV na vifaa vyengine kwa ajili ya kuhuisha nyaraka. Kama nilivyosema mwanzo kwamba lile ni jina ambalo lipo kwenye *program*. Mimi *concern* naikubali, tutashauriana serikalini lazima tubadilike katika *program* ambayo iliyopo na haitoi taaswira halisi ya matumizi ambayo yameainishwa kwenye vifungu.

Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, kifungu 281402 Kifungu cha Gharama za Ukodishaji wa Ukumbi wa Mikutano. Fedha hizi ni kwa ajili ya gharama za mkutano wa APAM ambao unatarajiwa kujumuisha viongozi wa nchi za Afrika wanaotarajiwa kufikia 500. Kuna *association* ya taasisi za utumishi za Afrika. Mwaka jana mkutano huu ulikuwa Malawi ambao mkutano huu huwa unawashirikisha, viongozi wa *Public services* Afrika nzima, tunategemea tutapokea wageni kutoka nnje 400 na wenyeji 100, jumla yao 500. Fungu lile limeonekana kwa ajili ya kukodi kumbi na mambo mengine kwa sababu ya mkutano huo. Kuna faida nyingi katika kuufanya mkutano huu. Nchi yetu tunasema kuna Sera ya Utalii kwa Wote, moja kati ya kuhamasisha utalii kwa wote ni kufanya hii mikutano ya Kimataifa. Gharama hizi zitatumika kwa ajili ya mkutano huu wa APAM.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa Afisi ni kidogo. Ufafanuzi nadhani nimeshautoa, fedha zilizoombwa Wizara ya Fedha zilikuwa ni milioni 650. Kutokana na uwezo mdogo wa serikali na *ceiling* tumepewa kiasi hicho cha fedha. Sisi tuliomba nyingi ambazo ni 650 lakini hicho ndicho tulichopewa.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma 220803 kifungu cha Matengenezo ya Magari, fedha zilizotengwa katika kifungu hichi zitatumika katika kufanywa manunuzi ya speya na kulipia gharama za matengenezo ya vyombo vya usafiri. Kama mnavyojua Kamisheni ni mpya haina hata chombo kimoja cha usafiri.

Kifungu 220305 kifungu cha gharama za safari. Fedha zilizotengwa zitatumika kwa ajili ya malipo ya gharama za hoteli za safari za kikazi. Yaani ziara tano Pemba kwa Makamishna na kwa kuwa Afisi hii ni mpya tunatarajia kwenda kujifunza na kushiriki katika mikutano na foram mbali mbali. Katika Jumuia ya *Africa Association for Public Administration and Management* yaani ile (APAM). Kwa sababu taasisi hizi ni mpya na watendaji wake ni wapya inabidi tukajifunze kwa wenzetu wanafanya nini katika kufikia kile kiwango cha juu cha utumishi wa umma. Ndio madhumuni ya fungu hili.

Tume ya Utumishi Serikalini 211116 kifungu cha Vikao vya Kamati. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuhudumia vikao 24 vya uendeshaji wa Tume ya Uchumishi Serikalini. Kama mnavyojua sasa ajira yoyote hao watu 2552 lazima tume ikae kwenye vikao kuidhinisha ajira. Lazima tume ikae kusikiliza malalamiko ya watumishi serikalini, fedha hizi ni kwa ajili hiyo.

Chuo cha Utumishi wa Umma au Chuo cha Utawala wa Umma hakuna uwiano wa fedha zilizoainishwa katika makisio ya bajeti na uchambuzi wake. Hili limechangiwa na wengi hasa Mhe. Asaa bilioni moja milioni mia mbili sitini na saba na laki tano, uchambuzi wa fedha hizo unapatikana kwa kujumlisha mapato ya Chuo na ruzuku ya milioni mia sita na tisa na laki tano, milioni mia sita hamsini na nane na Tanzania Shilingi milioni mia tatu kwa kazi za maendeleo. Hii milioni mia sita hamsini na nane ni mapato ya Chuo kwa kazi za maendeleo ambazo hazikujumuisha, zikijumuisha ndio zinapatikana hizo bilioni moja milioni mia mbili sitini na saba.

Aidha milioni mia tatu na thamanini na saba kwa ujenzi wa Chuo kwa mwaka wa fedha uliopita sio mwaka huu, mwaka huu ni milioni mia tatu, mwaka wa fedha uliopita ni milioni mia tatu na thamanini na saba.

Ufafanuzi wa bajeti za mafunzo, fedha hizo zitatumika kwa mafunzo ya muda mrefu, mafunzo ya muongozo wa ukaguzi, mafunzo ya ukaguzi yakinifu na mazingira ya mafunzo ya ukaguzi kwa kompyuta. Na hayo mafunzo tunategemea kuyafanya hapa ndani lakini tutayapata vile vile kwa kushiriki mikutano ya kimataifa.

Kifungu 211116 posho za vikao vya kamati, fedha za kifungu hiki zinatumika kwa malipo ya gharama za usafiri kwa washiriki wanaoalikwa kuja kutoa michango yao kitaalamu kwenye shughuli mbali mbali zinazofanywa na Wizara. Mimi nataka niliambie Baraza lako tukufu kwamba, mimi mwenyewe binafsi na ninawashukuru sana watendaji wangu nilitoa agizo la kutomlipa posho la kikao mfanyakazi wakati wa kazi. Na katika Wizara yangu hakuna mfanyakazi anayelipwa posho la kikao wakati wa kazi, isipokuwa analipwa posho anapokwenda safari nje ya pale kwenye kituo chake cha kazi. Kwa hivyo zaidi *nature* ya Wizara yangu ni vikao vya majadiliano na watu mbali mbali kutoka taasisi za nje.

Kwa hivyo fedha hizi ambazo mnaziona zimo humu si kwa madhumuni ya kuwalipa posho, Mhe. Jaku unaonesha saa lakini weye weye utakaekuja kunipigia buti hapa, kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe naomba sana muelewe hivyo, *nature* ya kazi za Wizara yangu nyingi zinategemea vikao vya majadiliano na taasisi za umma, na taasisi za binafsi na washauri mbali mbali katika kuelekea huko kwenye mageuzi ya utumishi wa umma.
La jumla nilikuwa nataka niliseme Mhe. Naibu Spika, kupitia kwako Wajumbe wote ambao wametoa maoni yao na michango yao, wametoa maoni yao kwa nia njema kabisa kama walivyonambia wengine, wala si kwa kutaka kunikomoa, kwa sababu hatupo hapa kwa kukomoana. Tupo hapa kwa kushauriana na yale yote ambayo tunahisi tuyachukulie hatua basi Wizara yangu imeyapokea na itayafanyia kazi. Mwaka jana mlinishauri katika kitabu kilichokuwa na kurasa 56. Kutokana na ushauri wenu mwaka huu nimekuja na kitabu kina kurasa 99, ya mwaka jana si ya mwaka huu. Ninachotaka kuhakikishieni kwamba mwakani ninaweza kuja na kitabu kikubwa zaidi itatokana na ushauri mlionipa na yale majukumu yangu ya msingi ambayo nimetakiwa niyafanye, nitakuja kuyaeleza kinaga ubaga kama nilivyoeleza kwenye bajeti yangu sikuficha kitu.

Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara yangu sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti mimi narudi pale pale kwenye utaratibu, mafungu anavyoyataja kila anapotaja kifungu zero ngapi anaposema fungu hili na ukurasa, kwa sababu vyenginevyo atatuchanganya. Hata akiwa mpya lakini vile vile ataje na ule ukurasa.

Kifungu 0101

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na hasa leo nilimtaka Mwanasheria wangu anijibu hili suala hili la utawala bora katika misingi ya utumishi hasa katika mahkama, na kuna katiba ambacho kifungu cha 102 naona leo Mheshimiwa wangu Mwanasheria hakuweza kunijibu ili kuweza kufahamu. Na kwa nini nikasema hivyo kwa sababu kule kuna mchanganyiko wa posho, fedha ambazo tangu zimeanza makarani uwiano haupo. Kwa sababu mahkama ya mwanzo wanalipwa posho la shilingi 250,000, mahakimu wanalipwa posho laki tisa. Sasa hiyo ndio maana nikataka kupata mchanganuo, leo mwanasheria wangu kaninyima hapa hakunijibu kutokana huku kuna katiba na huku kuna maelezo ya Wizara, lakini kidogo nataka nipate ufafanuzi tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Kwanza ilivyokuwa Mwanasheria katoa ufafanuzi vizuri sana namna ya kamisheni naTume zinavyofanya kazi, lakini mimi nilikuja nikaongezea *specific* namna ya hawa mahakimu wa mahkama ya mwanzo tulivyowashughulikia katika kuwasaidia kuwapa maslahi. Mhe. Mramu wangu alikuwa hayupo na Mheshimiwa ulisema hapa, sasa anapotaka niseme sasa ngumu, taratibu zetu hazikubali. Mheshimiwa mambo yake yote aliyoyasema nimeyatengeneza vizuri na nimeyatolea ufafanuzi vizuri, lakini wakati natoa ufafanuzi hayupo, niliangalia tena nikamuuliza jirani yake mramu wangu hayupo ningefurahi angekuwepo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Waziri wangu amejitetea lakini kwa kuwa amesema vizuri, lakini mimi nilitaka anitamkie mwanasheria wangu na yeye vile kama alivyoeleza nilikuwa sipo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nimeamua kusimama hapa kwa sababu ni kifungu cha mwanzo na kinachohusu Wizara hii na nitakachokisema hapa kitahusu Idara nyengine zote. Nimesimama hapa kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina sio tu zile hoja alizozitoa, lakini pia vile vifungu ambavyo nimeviuliza katika maeneo mbali mbali.

Nilichokigundua kimoja ambacho nimeona bora nikiseme kabisa ili akichukue kwa sababu yeye ndie Waziri anaeshughulikia Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama alivyojieleza katika maelezo yake Mhe. Mwenyekiti, kwamba Waheshimiwa Wawakilishi watakuwa wanapata matatizo kwa sababu vifungu namna vilivyokaa humu ndani na maelezo yaliyotolewa katika mafunzo yatatupa shida. Kwa sababu humu *sub vote* inaeleza kwamba ununuzi wa mafriji, sasa ukija ukimwambia Mhe. Mwakilishi ununuzi wa friji unajumuisha ununuzi wa jenereta hawezi kukuelewa.

Sasa nimeelewa leo kumbe kosa si la Wizara, ni Wizara inayosimamia ambayo ni Wizara ya Fedha, hili wakakae walirekebishe. Na katika maelezo yake Mhe. Waziri kayagusa, lakini kwa kikao hiki tunachoendelea nacho basi angalau huo muongozo wa MTEF tunaoambiwa unatumika tungepatiwa nakala Wawakilishi wote ili tukajua kwamba unapozungumzia *sub vote* hii yenye namba hii na maelezo haya inajumuisha nini na nini. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti hata sisi hatutendi haki juzi tumekaa mpaka saa kumi hapa tumepoteza pesa za walipa kodi imebidi tuahirishe kikao, kumbe pengine tungekuwa na maelezo yale tungezinusuru fedha za walipa kodi zile tunazozitetea sisi, lakini ningeomba hili Wizara ya Fedha wajifunze. Hivyo kwa kikao hiki kinachoendelea watupatie hiyo ili ituongoze katika Mawizara ambayo yanafuata baada ya hapo.

Lakini nimpongeze Mhe. Waziri katumia muda mrefu lakini kajibu kwa ufasaha kwa kina na nitumie fursa hii niwaombe Mawaziri waliobakia watatuokolea sisi wakati ikiwa watakuja na majibu fasaha yanayokwenda moja kwa

moja kwenye hoja kama alivyofanya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nadhani katika hili wajifunze sana, unaweza ukadhani ukitoa maelezo mengi ndio yanakusaidia kumbe pengine ukenda kwenye hoja unakuwa na jibu la hoja inapunguza. Kwa hivyo nimpongeze Mhe. Waziri na wengine wajifunze, lakini na hili la Wizara ya Fedha wajirekebishe ili wapate kuepuka mambo kama haya. Lakini haioneshi Mwenyekiti kwenye baadhi ya vifungu kama tutahitaji maelezo ya ziada bado tutaomba hapa na pale. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru sana unajua Mhe. Mwenyekiti Mhe. Haji Omar mimi rafiki yangu sana, lakini zamani mimi nilipokuwa Waziri kuna Mkurugenzi wangu mmoja alipokuwa anasikia Mhe. Haji Omar anakuja na kamati yake basi anaharisha kucha, sasa asione tabu lakini huo ulikuwa *just* utani. Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa na hoja yangu, na nilipokuwa nikichangia nilisema kabisa kwamba nitazuia fungu ikiwa sijapata maelezo ya kuniridhisha. Na kwa bahati nzuri Mhe. Mshimba yeye alikuwa hayupo lakini katika maelezo yalipotolewa mimi nilikuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mishahara wanayolipwa mahakimu wa Wilaya mimi siamini kwamba mishahara hii kweli imepitishwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama. Mheshimiwa huwa sipendi na si vizuri kutaja mishahara ya watu hadharani, lakini viwango vilivyokuwepo mwanzo vilikuwa vinatofautiana alau kwa shilingi laki moja moja. Lakini sasa hivi viwango vya mahakimu wa mikoa na mahakimu wa wilaya vinatofautiana kama laki mbili. Lakini mahakimu wa mwanzo ni hatari wanatofautiana, *difference* haipungui karibu milioni hii ni hatari tunatengeneza rushwa kule.

Mheshimiwa kazungumza vizuri kwamba hili linazungumzwa lakini je hapo litakapofikia muafaka je hawa watalipwa *arrears* zao? Kwa sababu ninaamini Tume ya Utumishi ikikaa na Tume ya Utumishi ya Mahkama wakikaa vizuri, mimi nadhani hili lazima watafanyiwa marekebisho yao je hapa tunaangalia *arrear*s zao zitakuwa vipi? Ukiangalia hata katika posho vile vile hata hiyo *difference* vile vile ni kubwa sana, hao mahakimu wa wilaya tumewaweka kama mayatima na huu ni muhimili ambao hapa hauna nafasi ya kuja kujitetea. Naomba hili ikiwezekana hata Mwanasheria Mkuu niko radhi, lakini asinitolee mafumbo aniambie tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya ziada baadae Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wa Katiba ikihitajika wanaweza wakasema, lakini mimi nataka nitoe maelezo ya kiutumishi.

Mheshimiwa kwanza niwe wazi nasimamia hili ambalo mmenisisitiza sana hapa kwa mujibu wa taratibu za malipo, mshahara ambao haujawa haki ya mtumishi na haujaidhinishwa hauwezi kulipiwa *arrear*s. Kwa hivyo hili niwe wazi Mhe. Rafiki yangu Hamza kwamba *arrear* watakaporekebishiwa baada ya marekebisho yao baada ya makubaliano kuthibitishwa huo mshahara mpya watakaolipwa, hakutakuwa na *arrear* kwa sababu *arrear* unalipwa baada ya kile kiwango kuidhinishwa kwa mujibu wa taratibu.

La pili Mheshimiwa ni kweli tumeliona hilo, na nimesema ndio maana katika hatua ya awali kuna mambo ya kiufundi yapo pale kulingana na sifa maana kuna vigezo viwili, kuna kigezo cha *qualification*, kuna kigezo vile vile cha uteuzi na ngazi ya ile mahkama. Sasa kwa busara tumetakiwa tukae tuangalie uwezekano wa kuweza na wao tusiwafanye watoto yatima. Nakuomba sana Mheshimiwa utuamini kwamba tutafanya hiyo kazi kwa kuzingatia ubinaadam. Kwa sababu hawa mahakimu wa mahkama ya mwanzo wengine wana *certificate*, lakini ni mahakimu wa mahkama ya Wilaya, wengine wana diploma wengine wana digrii.

Sasa mimi nadhani lazima maamuzi tutakayoyafanya yaendane na zile taratibu ambazo tumeziweka sisi wenyewe. Sasa kama kuna *exemption* lazima hilo serikali ikubali kwa jumla, ninachoweza kusema kwamba nimesikia *concern* ya Wajumbe na ndio maana tukathubutu kuwalipa posho hawa kwa kujua ile hali halisi ya mazingira ya maisha magumu. Mheshimiwa ninakuomba nikuhakikishie kwamba sisi tutaendelea kulifanyia kazi, na kwa sababu tokea mwanzo Tume ya Utumishi, amesema Mwanasheria Mkuu hapa Tume hizi zilikuwepo lakini zilikuwa zinashindana katika kupanga maslahi ya watumishi wao. Lakini bahati mbaya hawa walisahauliwa, sasa kama walisahauliwa na hizo Tume zenyewe, mimi ambaye ninaangalia ndio maana sasa hivi Tume zinatakiwa zipendekeze zipeleke kwenye kamisheni ili kamisheni iweze kuoainisha maslahi yawe yanalingana yasipishane sana.

Sasa kwa sababu utaratibu huo upo kisheria, nakuomba sana rafiki yangu Mhe. Hamza utuachie twende tukalifanyie kazi. Na ni kweli nakumbuka ulipokuwa Waziri mimi *back bencher* kuna Mkurugenzi wako mmoja alikuwa halali.

Lakini nataka nikuhakikishie mwaka 1996 wakati wewe hujawemo humu kulikuwa Waziri anatokwa na vitu vyengine visivyotokwa nikisimama. Kwa hivyo bado naelewa mimi sioni geni kuwa Mjumbe anapoamua kutetea maslahi ya wananchi na haki, wapo mawaziri tafuta, fanya *research* walikuwa wanatoa vitu vyengine nikisimama. Kwa hivyo naelewa sana namna ya wajibu na majukumu ya Mhe. Mwakilishi ndani ya Baraza la Wawakilishi anapotaka kujua kitu, na wala si katika hao wanaoona kwamba kwa nini umenihoji hapana, mimi naona ni haki yako na lazima ukiniuliza nikupe jibu linalokubalika. Lakini nisikupe jibu la udanganyifu pia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu atawajaalia mawaziri wasije wakatoka vitu visivyostahili. Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na hoja ya Mhe. Haji Omar kama nilivyosema nimemsifu sana ni msikivu, mtekelezaji, mtendaji lakini hili Mheshimiwa haya ni maisha ya wenzetu, na kama alivyosema kwa kuwa mshahara huu haujaidhinishwa wala ndugu zetu hawa hawategemei alau kuja kupata zile *arrears* zao kwa kweli haya ni maumivu makubwa. Sasa mimi naomba Mheshimiwa tuliomba *data base* hapa umechukua ninafikiri *hardly* miezi mitatu tu umetuletea. Sasa hili hebu naomba kaa na Tume ya Utumishi ya Mahkama, na kwa kuwa wamekiri wamesahau na hapa ukiangalia kweli waliwasahau hawa, mimi nadhani kiubinadam alau japo na hawa wahisi kwamba na wao kuna watu wanawatetea hapa Barazani.

Mimi ninafikiri kwa kuwa umeeleza vizuri linashughulikia mimi hasa hiyo ilikuwa ndio hoja yangu sasa hivi, tena lisichukue muda na kama sasa hivi tunapitisha bajeti, na tunashukuru umetenga mpaka fedha kwa ajili ya haya marekebisho, basi hawa waangaliwe katika *priority*.

Kifungu 0101 177,548,000

Kifungu 0111

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa natoa mchango wangu nilizungumzia juu ya madereva wetu, watumishi, lakini madereva kwa kujali muda wao mwingi ambao wanaupoteza bila ya kuwa na kazi ya kujiongezea kipato. Nilitaka kujua tu ufafanuzi zaidi kwa sababu Mheshimiwa alieleza kwa ufasaha zaidi lakini bado sikupata kuwasikia kwa sababu wafanyakazi hawa wana jina maarufu ambalo linajulikana kama madereva.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi waliochangia suala la madereva walizungumzia hata madereva wa viongozi. Nataka niwahakikishie kwamba madereva wote wa viongozi kuanzia Mkurugenzi, wanalipwa posho maalum kwa ajili ya kazi ya mazingira na kiwango kizuri tu wote, na na-*challenge* kwa yule ambaye hajalipwa Mheshimiwa amlete ofisini kwangu ili niweze kuchukua hatua pamoja na huyo asomlipa. Maana Wizara hii imepewa jukumu la kutoa miongozo na matoleo juu ya maamuzi ya kiutumishi. Sasa kama yupo mtu ambaye hajatekeleza basi niletewe tu, hatua za nidhamu kwa mujibu wa sheria zitafuata.

Lakini madereva ambao wapo kwenye *pool* hawawaendeshei viongozi, na kwa nini tumefanya hivi kwa madereva wa viongozi kwa sababu leo unaweza ukawa dereva wa kiongozi kesho ukawa sio dereva wa kiongozi, inabidi sasa posho ile ibakie kwa yule ambaye atakuja ndio utaratibu wa kiutumishi ulivyo. Wafanyakazi wa kawaida, madereva wa kawaida, nimesema kwamba wengi wamesema na nia ya serikali na ndio maana tukaweka pesa za nyongeza kwa kuzingatia *scheme of service* ya kuzingatia muda wa mtu ambaye ameufanyia kazi, kupandishwa kwake cheo, uzoefu wake alionao, katika mwaka wa bajeti Wajumbe pitisheni bajeti hii ili hayo mliyoyaomba niweze kutekeleza, msipopitisha siwezi kukiuza kisiwa cha Tumbabu nikapata kuwalipa hawa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia maslahi ya wafanyakazi wa ngazi ya chini katika nyongeza za mishahara, Mhe. Waziri ninamshukuru amejibu vizuri lakini wafanyakazi wana njaa, yeye kawawekea mbele sana mpaka *scheme of service* itengenezwe, sasa wenziwao wameshapata tokea Oktoba mwaka jana. Sasa yeye anawapa ahadi gani wafanyakazi hawa kwamba na wao mambo yao yatakuwa mazuri, kwa sababu kama tulivyosema kwamba *fomular* iliyotumika iliwa-*consider* wale waliosoma tu. Lakini hawa wametumikia muda mrefu miaka 30, 20, kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atupe ahadi yake wafanyakazi hawa watapata lini nyongeza ili na wao waweze kwenda pamoja na wakati.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Ninashukuru kwa maoni ya Mheshimiwa lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa kila kitu kilichomo katika *increament* kwa maana ya nyongeza. *Scheme of Service* ina taratibu zake, sio wafanyakazi wote watapata *increament* siku moja, kuna utaratibu wake kwa muda ambao tarehe ambayo ameajiriwa, imetimia, lakini katika mwaka sio wote wanaajiriwa siku moja na sio *automatic* na taratibu hizo lazima tuzifuate. Na hilo suala la *scheme of service* vile vile lina taratibu zake. Kwa hivyo Mheshimiwa atuamini tu, tulitaka tuyatekeleze haya kwa wakati mmoja Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliangalia *ceiling* ya bajeti ambayo tulikuwa nayo katika nyongeza ile ya kima cha chini, na mwaka jana karibu wafanyakazi wote wamepata *increament* zao za nyongeza ile katika kipindi cha miaka mitatu ambayo ilikuwa haijalipwa.

Lakini tumesema sasa hii ili tusiwe na kasoro ile iliyokuwa imetokezea kiutumishi, hii itakuwa inalipwa kila mwaka na ndio kwa mujibu wa taratibu zake. Tume-*practice* mwaka jana na mwaka huu tuna-*practice*. Na suala la *scheme of service* vile vile lina taratibu zake. Kwa hivyo Mheshimiwa yeye alikuwa mwalimu *by profession*, mshahara aliokuwa akilipwa wakati ule haulingani na mshahara wanaolipwa walimu wa sayansi kama alivyo yeye sasa hivi. Lakini walimu hao ambao wapo sasa hivi kazini ambao wengine walikuwa nae, na wao walitumia busara ya subra kwa sababu ya taratibu zilikuwa hazijakamilika na uwezo ulikuwa haujakuwepo.

Kwa hivyo mimi nataka niliambie Baraza lako tukufu kwamba lituamini kwa sababu bajeti ipo ya nyongeza na ya *scheme of service*, tutazingatia hayo kwa nguvu zetu zote ili tuweze kuwasaidia watumishi wetu wa umma ili na wao wajisikie kwamba ni watumishi, wawe na furaha katika kufanya kazi ya utumishi wa umma.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti nakubaliana sana na maneno mazuri anayotoa Mhe. Waziri lakini tunachozungumza sisi hajatufahamu vizuri au ninachozungumza mimi hajanifahamu vizuri. Wale wafanyakazi si nyongeza tunazozungumza za kila mwaka, wale wafanyakazi wa ngazi ya chini ambao kiwango chao cha elimu ni chini ya darala la 12 hawakuwekewa utaratibu wakati ule wa ongezeko la mishahara mwezi Oktoba, 2011, na haya yamethibitishwa na Wakurugenzi wa Wizara zinazohusika zaidi Miundombinu na Mawasiliano na Majenzi ambao wengine wanajenga majengo makubwa haya wengine hivi, ile *fomular* haikuwakubali kwa sababu hawana cheti cha *form four*. Sasa walijikuta wana miaka 30 lakini walipata labda shilingi elfu moja kila mwaka ya nyongeza lakini ule mshahara haukuongezeka, sasa hawa ndio tunaowazungumza. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri ende akakae na Wakurugenzi wa Wizara zinazohusika waone ni kitu gani kitakachofanyika ili wafanyakazi wale wa ngazi ya chini na wao wanufaike na hii nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Rashid na nilimfahamu tokea mwanzo makusudio yake. *Scheme of Service* inazingatia hayo yote. Wizara moja tu ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo iliyokuwa imetekeleza mpango huu wa *scheme of service* katika kipindi kilichopita. Taasisi zote ziliacha, kwa hivyo kwa sababu utaratibu huu unarejeshwa, hayo aliyoyasema Mhe. Rashid na niliyonayo mimi watakayofanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu na taasisi zangu zote hivi sasa *scheme* zote zimeshafikishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, kutokana na mapendekezo ambayo yamependekezwa kutoka huko hayo aliyosema Mhe. Mwenyekiti yote yanazingatiwa.

Kwa hivyo aniamini na hilo litatekelezwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti tulimuamini zamani hajui tu yeye.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, sasa na hili nataka kumwambia Mhe. Waziri alipotoa hoja mimi nilikuwepo, alitoa hoja ya wale ambao waliokuwa wamefanya *forgery* katika vyeti vyao. Lakini ninachotaka kumwambia kuna suala langu ambalo nimesema mapema kuna watu ambao waliajiriwa tangu tarehe 2/4 na wakalipwa mishahara yao jana, hao ni watu ambao walikuwa ni walimu wa sayansi na wamejaza mikataba. Sasa katika kulipwa kwao wamelipwa mapungufu. Sasa je hili Mhe. Waziri fedha zao zitapatikana wapi? Je ni sheria wakati wameshafungana na mikataba, ndio maana nikasema mwanasheria wangu naomba uwe karibu na mimi.

Kwa sababu ninavyojua ukifunga *agreement* tayari umeshaji-*comment* ninavyojua mimi ulivyonisomesha wewe mwanasheria. Itakuwaje leo mkataba huu uvunjwe mtu alipwe pesa kidogo? Ndio maana nikasema lakini hapo hapo Mheshimiwa kuna kitu kimenisumbua akili yangu, kuna hili posho la vikao vya kamati mwaka jana laki mbili, leo

naona mwaka huu ishirini na moja elfu na laki tano, hebu kidogo naomba Mheshimiwa wangu anifahamishe hizi zimekujaje kutoka laki mbili mpaka ishirini na moja na yeye ni mtaalamu wa kuzungumza hebu naomba na hili anisaidie vipi pesa hizi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Hili la mwisho alilolisema akisema nimuelezee bado nasema mimi nimetoa ufafanuzi wa kifungu kimoja baada ya kimoja kilichohojiwa hapa na mimi nimetoa taarifa. Kwa hivyo kama hajanisikia atafute *hansard*, au nitampatia hivi vifungu vyote vilivyoulizwa na nimevitokea ufafanuzi wake. Lakini kuhusu suala la kadhia ya walimu walioajiriwa na kulipwa *arrear* ya mwezi Aprili, katika utumishi kuna taratibu, mfanyakazi yeyote anayeanza kazi kuanzia tarehe 15 halipwi mshahara kamili. Lakini kwanza nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba wafanyakazi hawa mshahara wa Mei, Juni, wamelipwa. Kwa sababu walipoajiriwa hawakuanza tarehe 1 Aprili, wako walioanza kazi kuanzia tarehe 15, wapo walioanza kazi kuanzia tarehe 24, 25, na tarehe aliyopewa barua ya kuripoti kazini. Sasa hawa kisheria huwezi kuwalipa mshahara wao kamili wa mwezi Aprili, ndio taratibu za kiutumishi na taratibu za mishahara.

Mhe. Mwenyekiti kwa taarifa ya Baraza lako kama nilivyosema kwamba tunakuja na *pay policy*, sera ya malipo itafafanua hii mambo hayo. Kwa sababu naona sasa watu wanapata tabu katika kuelewa hasa malipo yanakuwaje katika kuwalipa watumishi wa Umma. Kwa hivyo ninachotaka kusema kwamba, wafanyakazi hawa ambao wamelipwa pesa pungufu hawakufanya kazi mwezi mzima. Lakini kama yupo ambaye ana barua yake aliyeanza kazi tarehe mosi akawa kalipwa pungufu kama kawaida yake Mhe. Mshimba aniletee hao watu Ofisini na tutaweza kuwashughulikia.

Lakini kwa taarifa nilizonazo mimi na alitumia lugha ya kupigwa changa la macho, mimi nataka nimwambie kwamba sikuja mjini kwa mwenge nimeaga, nilipoondoka kwetu nimeaga nakwenda mjini, kwa hivyo ada zile za kuaga zikafanyika. Kwa hivyo, hakuna mtu ambaye anaweza akanipiga changa la macho mana nimeaga. Sasa Mhe. Makame Mshimba akubali kwamba kama yuko ambaye hajatengenezwa vizuri, hajalipwa vizuri aniletee huyo mtu wala hakuna ugomvi.

Kwa hivyo ninachotaka kusema kama kuna mfanyakazi kalipwa pesa pungufu hakuanza kwa tarehe ambazo alitakiwa alipwe mshahara kamili na kama yupo Mhe. Mshimba aniletee.

Ninazo taarifa kwamba kuna mfanyakazi mmoja alikuwa Skuli ya Pale Jimboni kwangu na sasa hivi yuko Skuli ya Karume. Huyu ametovukwa adabu, kwa hivyo kuna hatua za kinidhamu na katika hao wafanyakazi ambao wamelipwa mwezi wa Aprili malimbikizo yao huyu kwanza hajalipwa mpaka atakapokamilisha kupeleka barua yake ya kujieleza juu ya hayo mambo ambayo ameyafanya. Mamlaka ya nidhamu imemchukulia hatua, huyo namjua. Lakini waliobakia wote wamepewa mishahara yao ya malimbikizo ya mwezi wa Aprili kwa mujibu wa tarehe mtu alivyoanza kazi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri lakini bado sijaridhika nayo na sababu niliyokuwa sijaridhika nayo nitaeleza. Ninachozungumza mimi sheria, sheria, watu wamefungishwa mkataba tarehe 2 ni masafa madogo tu hapo itakuwa kuzubaa kwa mwenyewe muajiri ndio akafika tarehe 2, nataka hapo mnielewe vizuri. Mhe. Mwenyekiti, wamelipwa mshahara tarehe 4 mwezi wa saba, hii hapa yote iko wapi halafu kwa vocha ya aina gani. Ndio maana nikasema hapa sitaki kusema kamati teule nilipokuwa nikichangia kwa sababu naona si pahala pake. Sasa Mimi nilikuwa nikitaka hapo tu Mhe. Mwenyekiti.
Je, hawa watu hapo katika mishahara yao kati kati iko wapi? Hilo ndilo nililomuuliza Mheshimiwa wangu. Nimesema kweli kapigwa changa la macho, lakini hapa leo kanambia kuwa kuna mtu ambaye tayari ameshaajiriwa na mafao yake hajapewa. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi umeniita shemegi, lakini naomba shemegi saa nyengine nikikwambia ukweli basi uniamini ukweli. Sasa kama unataka nikuoneshe kuwa kweli changa la macho limetendeka hapa nipe jibu la marejeo utanijibu vipi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wetu wa kawaida unakaribia kumalizika na kazi hatujamaliza namuomba Mwanasheria Mkuu atoe utaratibu ili tuweze kuendelea na kazi zetu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli iliyoko mbele yetu bado haijamalizika na kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kukamilisha shughuli hii katika muda wa kawaida, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liridhie kutengua kando Kanuni ya muda mpaka tutakapomaliza hoja iliyoko mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nadhani ugomvi hakuna hapa mimi toka mwanzo nilisema kama yupo huyo ambaye amefunga mkataba kuanzia tarehe hizo alizotaja Mheshimiwa alete, Wizara yangu ni ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, mbali ya kushughulikia mambo ya mishahara lakini tunashughulikia pia wanaoonewa. Kwa hivyo, mimi namuomba aniletee tu huyo mtu na wengine mbona ananiletea, aniletee tu. Lakini kwa kumpa jibu hapa kwa maelezo anayoyasema kwa sababu nitakuwa sina uthibitisho lakini uthibitisho wangu ni huu nilionao kwa hivyo namuomba Mheshimiwa kesho siku ya kazi niletee ofisini.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, niseme ni kweli nilimpelekea jamaa na hapa leo akanambia kaajiriwa lakini mpaka sasa hivi kusema kweli kaniletea ujumbe kuwa hajaajiriwa. Lakini hata hivyo niseme kwamba na hao wengine ambao nimekusudia itakuwa ni kazi ile ile, lakini wajibu wangu kutekeleza kusimamia mwananchi aliyedhulumiwa nitampelekea mimi sioni tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili naomba bado sijaridhika, tuendelee.

Kifungu 0111 Idara ya Miundo ya Taasisi,
Utumishi na Maslahi ya Watumishi - Shs. 150,471,000
Kifungu 0301

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii tena na naendelea kumshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina wa vifungu mbali mbali tulivyoviulizia vikiwemo vya Ofisi Kuu ya Pemba. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu hivi mbali ya vile ambavyo alivitolea ufafanuzi nilivyovihoji ambavyo vilikuwa vina ongezeko, viko vifungu ambavyo niliuliza kwamba kwa nini kwa upande wa Pemba hakuna ongezeko ukilinganisha na idara nyengine, hasa katika maeneo ambayo kwa jumla tulivyoelezwa hapa kwama hivi vimeongezeka kutokana na kupanda kwa gharama kwa mfano, masuala ya mafuta.

Ili nisipoteze muda wako Mhe. Mwenyekiti, nimrejeshe Mhe. Waziri katika ukurasa wa nne fungu 220400 gharama za mafuta na viainisho, nilivisoma wakati nilipotoa mchango wangu. Kwamba gharama za petroli kwa mfano mwaka jana zilikuwa shilingi 5,570,000 mwaka huu shilingi 5,556,000. Gharama za dizeli shilingi 5,000,000 mwaka jana na mwaka huu shilingi 5,290,000. Gharaza za vilainishaji mwaka jana shilingi 300,000 mwaka huu shilingi 500,000 pana ongezeko dogo. Lakini kwa mfano gharama za umeme shilingi 1,800,000 mwaka jana na shilingi 1,800,000 mwaka huu. Sasa nilikuwa naomba anisaidie tu kwa sababu kumekuwa na ongezeko takriban katika kila idara kwa sababu wanatwambia mafuta yamepanda bei na umeme umeongezwa bei. Kwa nini kwa Ofisi Kuu Pemba hatujaona ongezeko hili katika ofisi yake nilikuwa naomba anisaidie hilo yale mengine nashukuru kwamba amenipa ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa kwa kutaka ufafanuzi katika vifungu hivyo. Ni kweli nilitoa ufafanuzi juu ya vile vifungu ambacho vimepungua kwa upande wa Pemba na upande wa Unguja lakini nafikiri sikuvitaja vifungu vyote. Lakini katika kuhakikisha fedha za wananchi zinatumika vyema pia tulikwenda katika hali halisi ya matumizi, kwamba Ofisi Kuu Pemba katika vifungu hivi tulikuwa na gari nasikitika kusema kwamba gari yetu ilipata ajali na tunategemea tutapata gari mwaka huu.

Lakini vile vile katika suala hili la kuona kwamba tunapanga matumizi kwa uhalisia wa mambo vile vile imetupelekea kuona kwamba mahitaji kwa upande wa Pemba yanayohusu Ofisi Kuu Pemba ni haya yaliyopo na hasa tukizingatia kwamba kwa zile *activities* ambazo shughuli zake zimepangwa na Wakurugenzi kutoka Unguja mafungu yake mengine yanatoka huku kwa mfano masuala ya semina na mambo mengine yatakwenda kule Pemba wakiwa na *package* yao kwa hio Ofisi Kuu inachofanya ni kuratibu.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Ismail Jussa aelewe hivyo kwamba sio suala la kuzidi tu, lakini na suala la kuangalia uhalisia wa matumizi katika kila kifungu. Umeweka ununuzi wa *stationary* shilingi 12 milioni je, kweli ukitumia shilingi 12 milioni *stationary* hizo utazitumia kwa mwaka au namna gani. Kwa hivyo katika kupanga bajeti tumezingatia hayo na tulikaa tukakubaliana kwamba kila mtu alete uhalisia wa matumizi yake kufuatana na mwenendo wa matumizi ya kipindi kilichopita. Na kwa sababu hatutaki vile vile kila wakati kuwa kuna kifungu kimevimba halafu unakihaulisha unakipeleka kwenye matumizi mengine, katika utaratibu mzima wa kufuata utaratibu wa matumizi mazuri ya fedha za umma. Kwa hivyo, ni hilo tu ninaloweza kulisema Mhe. Mwenyekiti. Namuomba Mhe. Ismail Jussa aelewe hilo ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri na naomba iwe hivyo alivyotueleza kwamba tunafanya utaratibu huu kuwa katika yale maeneo ambayo kulikuwa kuna ongezeko ambalo halihitajiki ama libakie pale pale au lirudi nyuma. Kwa sababu nina bahati ya kuwa ni mjumbe ambayo wewe Mhe. Mwenyekiti ndiye unaeiongoza vile vile nadhani tutapata fursa nzuri ya kujiridhisha tutapokuwa katika ziara Pemba. Baada ya maelezo hayo naomba tuendelee ahsante sana.

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii nikapata ufafanuzi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilieleza namna ya mafunzo tulivyoyapata na nilieleza wazi wazi kwamba tunapopanga bajeti kwanza kuna vitu karibu vine tunaviangalia, kuangalia *MDG* (*Millennium Development Goal*), tunaangalia *Vision 2020*, tunaangalia MKUZA halafu tunaangalia *MTF*. Sasa Mhe. Waziri katoa ufafanuzi na katoa ufafanuzi mzuri kwamba kwanza kakiri kuna makosa lakini basi angalau angetuletea japo *item* mbili, angeleta lile buku la *MTEF* japo *item* mbili. Kwa sababu mimi nilizungumza kabisa MTEF na ndio maana watendaji wanatakiwa wakae vizuri watusikilize kwa sababu zaidi tunapokuja katika masuala ya chakula na vinywaji, ununuzi wa zawadi hatuna tatizo, lakini chakula na vinywaji halafu kuna viburudishaji sisi mwanzo tulisema labda viburudishaji kuna mziki, lakini mziki kila idara.

Sasa unaposema vyakula na vinywaji viwanywaji sisi tunajua ndio hiyo hiyo *refreshment* ndio maana Mhe. Mwenyekiti, nikasema kwamba, pamoja na yote lakini Mhe. Waziri nitamuomba hili fungu moja hasa linalohusu vinywaji na viburudishaji na *refreshment* basi tupate maelezo ya ziada na vifungu hivi tuvibane, tutavipitisha lakini katika hali ya *incubator* kupitia katika kamati ili wakapate ile *break down*. Kwa sababu tujue viburudishaji, chakula na kinywaji, zawadi hana matatizo wala Mhe. Waziri zawadi hana nyingi, lakini viburudishaji na vinjwaji labda atutafsirie viburudishaji hasa wamekusudia nini mziki watu wakishakula wakisha kunywa.

Sasa mimi niseme vifungu hivi tutavipitisha lakini katika hali ile hali ya angalizo. Mimi kamati yangu nimepewa kati ya kwenda kuangalia na mimi sioni tabu kwamba Mhe. Naibu Spika, kwanza tunakusumbua na haipendezi kukuweka kama uko kwenye kamati mwakani tunakuondoa usishiriki katika, lakini angalau ukatuchukulie *break down* ili uje uturidhishe na jawabu hizi tunaomba katika Baraza lijalo umetupa maelezo kama hatukupata maelezo ya kutosha basi vifungu hivi tutoe maagizo viondolewe katika viburudishaji vikatumike katika mambo ya msingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tuendelee?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Tuendelee katika hali ya kukubali waziri kwamba tunamuweka katika *probation period* chini ya udhibiti wako na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ile ya mwanzo naikubali ya *MDG*. Ya pili chakula na vinywaji na kuna kitu wewe unajua vizuri zaidi kingereza kuliko mimi bi*ting* vitafunio ndio hii iliyokusudiwa humu, kwanza naomba ufafanuzi huo. Kwa hivyo, chakula na kinywani ile *lanch* au *dinner*, *biting* ni vile ambavyo umekuja ofisini kwangu viburudishaji biskuti, katlesi, na nini wala si mziki. Kwa hiyo

naomba nitoe ufafanuzi huo lakini vile vile nakubali ushauri wa kuipa kamati kuja kufaya uhakiki na uangalizi mzuri zaidi katika matumizi husika. Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nishaelewa kila kitu lakini unajua hofu inakuja wapi, bajeti ya mwaka jana ilikuwa inasema milioni tatu na laki sita, bajeti ya mwaka huu ni milioni ishirini na sita.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Hamza si umesema Mwenyekiti na mimi tufuatilie.

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba Shs. 489,351,000
Kifungu 0401

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru inawezekana ni hoja yangu ya mwisho asiwe na wasi wasi Mheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia kuhusiana na hii Tume ya Uhakiki iliyofanya kazi karibuni na kugundua kwamba kuna udanganyifu katika vyeti na baada ya hapo kwa ushahidi niliopata mimi zaidi ni walimu, lakini Mheshimiwa mwenyewe kakiri kwamba na wafanyakazi wengine vile vile wamo wamekatwa mishahara yao.

Suala ambalo nililiuliza nilisema ni kwa nini hawakuandikiwa wafanyakazi hawa kabla ya kukatwa ile mishahara na hawa wafanyakazi ikiwa ni walimu wako chini ya Mwalimu Mkuu. Kikawaida mfanyakazi anapopata tatizo hilo na kuchukuliwa hatua anaandikiwa barua na nakla inakuwa kwa Mwalimu Mkuu, kwa hivyo Mwalimu Mkuu anakuwa na taarifa na mwenyewe anayo taarifa. Sasa kwa nini hawa wakachukua hatua ya kuwakata mshahara moja kwa moja bila ya kuwapa taarifa jambo ambalo linashusha morali ya wale waliokatiwa mishahara hata kama wamefanya kosa.

Lakini pia kama ingekuwa hawana kosa kama ambavyo ulijieleza waje walete malalamiko baadae haionekani kwamba wangepelekewa barua imezuilikana vile vile hali hiyo. Hebu Mhe. Waziri tueleze kidogo ni kwa nini ikachukuliwa hatua ya moja kwa moja kukatwa mshahara wakati hawa ni wafanyakazi wa mkataba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rashid Seif na mimi naelewa kwamba hafanyi nishituke anafanya kwa kutaka kujua ufafanuzi. Lakini nilipokuwa nikisema tunapogundua kwamba kuna fedha zinapotea hatua ya mwanzo ni kukinga kwanza zisiendelee kupotea, ndicho tulichofanya. Na kabla ya kuzuia tulitoa barua kwa Mamlaka ya Ajira inayohusika na Wizara ya Fedha kwamba wafanyakazi hawa wamegundulika wana tatizo kadhaa kwa hivyo tunaomba. Sasa Mamlaka ya Ajira ina haki ya kumuandikia muajiriwa wake juu ya tatizo ambalo limejitokeza. Sasa kama Mamlaka inayohusika haikufanya kazi hiyo basi mimi nadhani ofisi yangu itakachofanya ni kuwakumbusha wachukue hatua hiyo badala ya kufanya hivyo.

Lakini mimi nilichofanya na ndio utakuwa utaratibu huo, ni kwamba fedha inatumika kinyume na hali halisi ilivyo kitu cha kwanza cha kufanya ni kuzuia pesa ile isiendelee kutumika katika utaratibu uliokuwa haustahiki. Nilipokuwa nikijibu swali nilisema kwamba tumetoa *room* ya mtu kama ana malalamiko aje ofisini afuate taratibu tutachukua hatua hiyo. Kwa hivyo, Mhe. Rashid Seif nataka nimuarifu kwamba sisi kama Utumishi wa Umma tulipoamua kuzuia tuliwaarifu Wizara ya Elimu na taasisi nyengine zenye watumishi kama hao na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sasa kama muajiri hakuchukua hatua hilo litakuwa ni suala jengine lakini sisi kama Utumishi wa Umma mambo yetu yanakwenda kwa maandishi hayendi kienyeji enyeji tu yanakwenda kwa maandishi. Kwa hivyo, Mhe. Rashid nimemuelewa na yeye anielewe kwamba sisi kama Utumishi wa Umma tumechukua hatua ya kuwaandikia wahusika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Waziri lakini akumbuke kuwa keshawatupia mzoga Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, kama wao wataubeba tutakuja kuonana nao tukijaaliwa *Inshaallah.*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika ukurasa wa 48 katika asilimia Zanzibar ilipata asilimia 21, nikasema asilimia 21 Zanzibar kama ni nchi ni ndogo, anieleze Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ningependa iwe asilimia hamsini kwa hamsini, mana Zanzibar ni nchi tumeungana tukiwa nchi na Tanganyika wakati ule ilikuwa nchi kwa hivyo nchi mbili zimeungana. Lakini tunapokwenda katika uhalisia na utekelezaji lazima tuwe wakweli

kwamba hata hivi sasa mimi Mhe. Jaku Hashim aniamini na ndio hali halisi ilivyo kwamba, asilimia 21 na asilimia 4.5 asilimia 21 ni kubwa zaidi. Mlimpigia makofi sana hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu namna alivyojibu hoja, vile ndivyo tunavyokuwa mnatuona hapa tunakuwa labda vipi, lakini kwenye vikao vyetu kule *style* ile ya Mwanasheria Mkuu ndio tunavyokuwa.

Lakini sasa unajadili hoja kwa utaratibu hujadili hoja kwa nguvu tu, mnakwenda pahala mnakubaliana mnakwenda pahala hamkubaliani mpaka mkifika aah hapa nilipopata kwa sasa kwa kuanzia sihaba tunakubaliana na hilo. Na hili kama makubaliano yetu kwenye mkataba wetu unavyosema ni la muda, hili la asilimia 21 kwa 79 ni la muda, kigezo tulichokitumia ni kigezo cha kiutawala kupitia Wabunge waliopo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimesema vizuri wakati nilipokuwa nikitoa ufafanuzi.

Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim kama atamsikia Waziri wa *Management* ya Utumishi wa Umma nafasi ambazo ataajiri mwaka huu nilisema hivi, ukichukua zile taasisi za Muungano kwa maana zetu sote Zanzibar na Tanzania Bara basi hata kile kiwango ambacho tumekiweka sisi kwa uwezo wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kitakuwa ni kidogo kuliko kile tutakachopata kwa asilimia 21 na ukizingatia benki tuliyonayo ya vijana ambao wamemaliza vyuo hawajaajiriwa ni kama elfu tano na kitu. Hii ni kazi ya kila mwaka hivyo Mhe. Jaku naomba anielewe kwamba tungependa sana mimi ningependa na ndio mawazo yaliyokuwa 50 kwa 50, lakini wenzetu walijenga hoja ya *population* tukaona kwa *population* tutazidiwa sana pengie tungepata asilimia saba tukatumia mbinu hii sasa mnatufanya tuseme mambo ambayo saa nyengine wenzetu tukenda kule wajue mikakati yetu tuliyonayo. Mimi nataka mtuamini kwamba asilimia 21 kwa asilimia 79 kwa kuanzia si asilimia ndogo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Waziri kavaa koti leo na kakubali sina tatizo naye tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru japokuwa si utaratibu kumsaidia waziri lakini tumwambie tu Mhe. Jaku Hashim tutapata asilimia mia moja ikishasimama Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na *Inshaallah* itasimama karibu. Mhe. Mwenyekiti nukta yangu katika mchango wangu nilihoji swali namshukuru Mhe. Waziri kalitolea ufafanuzi nalo linahusu mradi wa *E-Government*. Nimelisimamia hapa kwa sababu fungu lake limewekwa hapa lakini pia kwa sababu hakuna fungu lake jengine.

Mhe. Mwenyekiti, hili kama unakumbuka pia hata kamati kwa hivyo nasimama kwa namna mbili hapa kama Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe lakini vile vile kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Maelezo yake Mhe. Waziri nimemfahamu kasema suala tuendelee kulifuatilia katika wizara inayohusika. Lakini naomba hebu anisaidie zaidi Mhe. Waziri. Kwa sababu maelezo yake hayana utata katika kuyafahamu, lakini suala hili mwaka jana kama Mhe. Waziri atakumbuka nililisimamia lilipokuja hapa na nikataka kujua kwa nini fungu lake lilikaa Wizara ya Fedha. Kwa sababu ilivyoelekea mambo ya mawasiliano na mkonga wa taifa yaweko katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na tukapata *commitment* ya Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba usimamizi wake utakwenda Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Sasa nalisema hapa kwa sababu serikali hapa inawajibika kwa pamoja.

Lakini nikasema mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, kwamba mradi huu umekuwa kama vile kinyang'anyiro, Wizara ya Mawasiliano ilipokuja ikautaja, ilipokuja Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakautaja kwa sehemu yao, walipokuja Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakasema wao ndio walioratibu kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na wakautaja. Halafu alipokuja Waziri wa Fedha mwenye fungu naye akalitaja. Sasa leo ndio hilo jibu linalopatikana hapo Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunahoji matumizi ya fedha zile tunataka *break down* utekelezaji kawekewa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mimi simlaumu yeye kwa sababu yeye fungu hili halikuwa kwake yeye kakabidhiwa mradi kwamba sasa umekamilika. Sasa nilikuwa nataka anisaidie tu kwamba kasema sisi kama kamati tuendelee kulifuatilia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais lakini nasema mradi huu sasa hivi uko kwake. Sasa anisaidie hili je, anakusudia kwamba kwa madhumuni ya Baraza hili kama wasimamizi wa fedha za wananchi wa Zanzibar kwamba tuje tulihoji katika Wizara ya Nchi ikifika wizara yake au anakusudia kwa sababu liko katika wizara yake kamati hii sasa iendelee kufuatilia nje ya utaratibu wa Baraza. Naomba anisaidie hili ili nipate kujua kabisa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, katika hili suala la uendeshaji mimi ndiye mhusika, uendeshaji wa ile serikali mtandao wenyewe kwa maana ya *administration* na kuendesha na nini kwa hiyo kamati moja kwa moja inahusika. Lakini kamati hii pia nilisema kwamba suala hili la usimamizi wa kuutengeneza huu mradi wenyewe liko Wizara ya Fedha na serikali iliamua hivyo.

Serikali iliamua Wizara ya Fedha itasimamia kuanza huu mradi, miundombinu itasimamia *in structure* ya haya mambo yenyewe, *management* ya uendeshaji itakuwa ya Utumishi wa Umma. Ndio mgawanyo wa mamlaka katika uendeshaji.

Kwa hivyo mimi nilisema vile vile nitatoa mashirikiano kwa kamati, kushirikiana nao katika kuhakikisha inapatikana *break down* ya matumizi ya mradi kule Wizara ya Fedha, lakini waliosimamia matumizi ya fedha ya huu mradi ni Wizara ya Fedha. Sasa hata nikisimama mimi kutaka kutoa au mwengine tutakuwa tunababaisha.

Lakini mimi nipo tayari Mhe. Ismail kutoa mashirikiano na kamati yangu kupatikana *break down* ya matumizi ya mradi, mimi nipo tayari lakini wanaoweza kutoa ufafanuzi zaidi wa namna gani matumizi hayo yamefanyika ni Wizara ya Fedha. Kwa hivyo Mhe. Ismail ninajua kuwa ameuliza hili kwa faida ya Baraza na mimi ninakubaliana na yeye, lakini hivyo ndivyo utaratibu ulivyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi alivyokuwa muwazi katika kuzijibu hoja zetu. Ninashukuru kwa hilo na mimi ninasema ninaheshimu ofa yake kwamba atatoa mashirikiano kwa kamati katika kulifuatilia.

Lakini ninataka kusema kitu kimoja kwamba, katika hili tunajifunza kitu Mhe. Mwenyekiti, na ninadhani hili serikali ijifunze kwa sababu Baraza unaona linavyobadilika hili, kuna siku tutakuja kuiwajibisha serikali tulazimike kufanya maamuzi magumu ambayo hatuyapendi.

Kwa nini ninasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama Baraza hili Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio anasema si lake, lakini ninalibana hapa kwa sababu limemalizikia kwake, kwamba alitoa *commitment* ndani ya Baraza hili, na ninakumbuka alisema mara tatu kwa sababu yale maneno yalikuwa hayaridhishi mpaka mwisho akasema labda Kiswahili changu hatuelewani kwamba msimamizi wa mradi huu unahamishiwa Wizara ya Mawasiliano.

Sasa inadhihirika na imekaa katika *record* ya hansard ninashukuru leo kwamba maamuzi yale au *commitment* ile ya serikali, ninasema ya serikali ndani ya Baraza hakuheshimiwa bado Wizara ya Fedha inang'ang'ania mradi ule, mpaka leo tukaukwamisha na ndio leo tunapoomba *break down* tunaambiwa tuende Wizara ya Fedha na sio Wizara ya Mawasiliano.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nina wasi wasi kwamba hata Mhe. Waziri Omar Haji Kheri anasema tu kwa sababu sio pahala pake, kwamba hata hiyo miundombinu mimi siamini kama imesomwa na Wizara ya Mawasiliano Mhe. Mwenyekiti.

Lakini ninasema tutalifuatilia na Wizara ya Fedha itakuja hapa mwisho kusoma bajeti yake. Ule mchezo aliosema Mhe. Haji mchezo wa Kitumbatu, mchezo wa kibatabata. Atakuja kuucheza na mimi nitamuongezea na kipato cha Kimakunduchi atakuja kuucheza Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Lakini kwa sasa ninasema wacha tuendelee, ninakubali ofa yake Mhe. Waziri kuwa atashirikiana na sisi kufuatilia, lakini ninasema bado fedha zile bilioni 18 tunahitaji tupate maelezo ya kina. Lakini hivi sasa ninasema tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti shs.600, 058,000,000
Kifungu 0501 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo ninaona kama kifungu kimerukwa hapa au sijui macho yangu hayaoni vizuri.

Kifungu 0402 Utawala wa Umma

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi maana nilikuwa hiki kifungu nilikuwa ninakisubiri, nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo. Nilipokuwa nikichangia mchango wangu kwenye hotuba yake hii nilizungumzia suala zima hili la ujenzi wa chuo hiki. Maana kinaonekana chuo hiki sasa kimeshakuwa mradi usiomalizika huu.

Kila bajeti inayokuja inaingizwa mafungu ya fedha, lakini umalizikaji wake au ule ufanisi hauonekani. Sasa nilikuwa ninataka maelezo kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri, hebu atusaidie huu ujenzi hasa, nani ni mkandarasi pale, lakini kiasi gani cha fedha ambacho kimeshaingizwa pale, ili tuone na hizi nyengine ziendelee kuingizwa au tuseme aah! zinatosha hizi zilizopatikana kwa sababu utakuwa mradi hauishi.

Amejaribu kutoa maelezo Mhe. Waziri alipokuwa aki-*wind up* hapo lakini bado sikuridhika na maelezo yake, ninataka maelezo ya ziada katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpe maelezo ya ziada ndugu yangu Mhe. Mtando kwamba, nipende kuwaarifu Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaotaka kwenda ku-*visit* Tunguu kwenye Chuo cha Utawala wa Umma na kuona maendeleo, na kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu mwaka huu wanaanza kusoma mwezi wa nane katika chuo cha Tunguu, ninawakaribisha.

Ni kweli huu ujenzi umeanza muda mrefu. Umeanza tangu mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza. Mimi mwenyewe binafsi nilikagua chuo kile nikiwa Mwenyekiti wa kamati kama mara mbili.

Kwa hivyo hoja ya kuwa umeanza muda mrefu ni kweli, mimi ninaelewa vizuri na ndio maana sisi tukaamua sasa kuweka utaratibu wa kufuatilia kwa karibu zaidi. Na haikosi pengine Waheshimiwa Wawakilishi wanaokaa maeneo ya Fuoni huniona siku za *week end* na hata ninaelekea huko.

Kamati yangu inakwenda kila Jumapili kwenye *site meeting* pale. Lakini na mimi ninakwenda *site visit* kila Jumapili, na kuhakikisha kwamba wanafunzi wa chuo hiki kwa eneo la *floor* ya kwanza chini linahamiwa mwezi wa Agosti.

Sasa hayo yaliyopita nyuma kama nilivyosema Wizara yangu haikuyasamehe bure bure. Tunafanya mazungumzo na Wizara ya Nchi Ofisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kujua kadhia iliyosababisha ucheleweshaji wa jengo lile uwe haujamalizika angalau kwa awamu ya kule chini mpaka leo.

Lakini bajeti yangu ya mwanzo ya maendeleo ni hizi fedha ambazo hivi sasa mkandarasi yupo na anafanya kazi, na ninawakaribisha Waheshimiwa Wajumbe twende tukaone. Hiyo kadhia tutaizungumza na hatimae kamati itajua nini ambacho kinaendelea.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Naona suala unalolizungumza lipo kwenye mpango wa maendeleo sio hapa tunapozungumza ukurasa wa 726

Mhe. Mwenyekiti: Lakini yeye anazungumzia Chuo na hapo kimezungumziwa chuo

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ndio ujenzi wa chuo

Mhe. Mwenyekiti: Ndio tunaozungumzia

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: 726 Mipango ya Maendeleo sio hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninadhani tupo katika hatua ya mwisho; Mhe. Mtando.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na maelezo marefu, mimi nilikuwa ninataka kutanabahisha. Unajua Mhe. Mwenyekiti, hizi ni fedha kuwa tunaziingiza pahala ambapo

tayari pana tatizo na lipo lile tatizo halijatatuliwa, wasi wasi wangu ni kwamba tutakuwa tunaziingiza pahala pabaya zitakwenda kuharibika.

Sasa ndio maana nilikuwa ninataka yale maelezo, kwanza yale maharibiko yalikuwaje mpaka tukafikia pale, angalau tupate yale si kwa sababu ya kusema kuwa wizara yangu hivi sasa ndio imeanza kuchukua na hata huko nyuma na wizara ni serikali.

Kwa hivyo Wizara ilikuwa ikiongoza huko, wizara ilikuwa wapi hilo si tatizo lakini hizi fedha tunazikabili serikali kwa ajili ya matumizi. Sasa kama yale matumizi ya mwanzo hayakuwa sahihi au hayakutumika vizuri. Ni vigumu sana kuendelea kuingiza fedha mpaka tukapata ufafanuzi wa kwanza.

Kwa hivyo mimi nilikuwa ninashauri kwanza nafikiri tuzuie hili fungu mpaka tupate maelezo ya kina ya matumizi ya fedha zile za mwanzo na namna gani zilitumika. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tupate ufafanuzi mzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Ninadhani Mhe. Mtando inaonesha sasa nitumie kiti cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, mimi ndiye Mwenyekiti na tumefuatilia hili.

Kwanza mkandarasi wa mwanzo wa kujenga ilikuwa ni KMKM ambavyo ni vikosi vyetu maalum. Baada ya kuonekana kafanya sivyo, kakatishwa mkataba na utaratibu unaendelea na kupewa Chuo cha Mafunzo anamalizia ili vijana wetu wapate kusoma, kwa sababu katika hotuba kama ulisikiliza watu wanasoma vipindi sita kwa siku moja.

Sasa wamepewa wenzetu na wameahidi mwezi wa nane watamaliza hiki Chuo. Sasa na hilo kama kamati yangu tushakwenda na tumeshakagua, kamati imeundwa tunaijua inafuatilia kila siku ili mwezi wa nane waweze kusoma na hao waliofanya dhambi utaratibu wa kisheria unafuatiliwa, kama kurejeshwa fedha ama utaratibu mwengine wowote utakaokubalika.

Naomba nisaidie hivyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio kumetumika rungu la Mwenyekiti, sasa mimi unategemea niseme nini, nikubali tu tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninataka niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe na wananchi isiwe kaona mheshimiwa kazuia kifungu, akaona labda anazuia matumizi. Lakini wakati mwengine vile vile ni kumsaidia waziri ili kumpa nguvu katika kufanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma mimi nilisoma pale *course* ya *management*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho nilichokiona katika hotuba yako Mwenyekiti, kwa hivyo hivi sasa ninakisaidia kiti na ninamsaidia na Mhe. Waziri. Chuo hiki kinadai fedha nyingi serikalini. Mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, katika deni la ndani la serikali kwa sababu kuna deni la nje na deni la ndani, hili halikuoneshwa.

Leo Mhe. Mtando anataka kuzuia ruzuku ya shilingi milioni mia tatu wakati chuo kinadai fedha nyingi zaidi ya shilingi milioni mia tatu. Sasa kwa nini Mhe. Waziri ulishindwa kujenga hoja ya kuzidai zile katika lile deni la ndani upewe pesa zako umalize chuo kuliko kuja kunyanyaswa katika hizi ruzuku za shilingi milioni mia tatu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Fedha ninafikiri hayupo, hili yeye ndiye angelisaidia zaidi katika lile deni la ndani lingejionesha *at least* serikali ikatafuta namna ya kuweza kulilipa ili hiki chuo kikaweza kumaliza. Mhe. Mwenyekiti, hiyo tu ndio ilikuwa hoja, ndio nikasema hoja hii kwa kukusaidia wewe na kumsaidia Mhe. Waziri kulipwa fedha zake.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante tunaendelea tumechukua hoja hiyo na itafanyiwa kazi, serikali ipo inasikia. Tuendelee.

Kifungu 0402 Chuo cha Utawala wa Umma	shs.658, 000,000/=
Kifungu 0501 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu	shs.230, 267,000/=
Kifungu 0601 Idara ya Mafunzo ya Maendeleo ya Watumishi	shs.117, 188,000/=
Kifungu 0701 Idara ya Mipango na Raslimali Watu	shs.138, 868,000/=

Kifungu 0801

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hoja zake ambazo zilizokuwa nzuri na mwanana, na inshallah Mwenyezi Mungu amjaalie hivyo hivyo alivyokuja mara hii na aje tena mara nyengine kama hivi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu nilisema kuwa Tume ilimpa barua kijana ambaye kwa muda mwingi sana wanasema amehangaika katika rufaa yake, lakini kwa bahati mbaya wakasema wao sasa hawawezi kusikiliza rufaa hiyo, wanasikiliza rufaa ya mwaka 2007.

Lakini nimkumbushe Mhe. Waziri kijana huyo niliwahi kumpelekea na barua aliziona na akatujibu kuwa mpaka hivi sasa ngojeni kwanza nipange upya niwe na tume, halafu baadae nitaweza kusikiliza kesi yake.

Lakini cha kusikitisha katika hoja yangu leo sikumsikia Mhe. Waziri kuweza kumtetea huyo mtu maskini wa Mungu ana watoto na watu wengine wanaomtegemea ili kuweza kumsikiliza matatizo yake. Naomba Mhe. Waziri anijibu kuwa huyu mtu jee hii tume itatoa amri ya kuendelea kumsikiliza, hebu msikilizeni kama ana hatia mtamtia hatiani, kama hana hatia itabidi aachiwe aendelee. Naomba Mhe. Mwenyekiti, anijibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kama ni huyu mtu mfanyakazi wa Wizara ya Afya ndiye anayemzungumzia.

Mhe. Mwenyekiti: Ni mtu gani.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Huyo mtu ni wa KMKM, Wizara ya Afya si ameshaniambia kuwa ameshamuajiri, huyo sina tatizo naye. Ninayesema huyu ni mtu wa KMKM.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nilijibu tatizo la mramu wangu kuwa hakai ndani.

Mhe. Mwenyekiti: Si utaratibu wacha Waziri amalize na wewe utapata nafasi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Nilijibu Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo ndio *over roll* ya tume za utumishi zimeshaanza kuchukua hatua ya kuwasiliana na Idara Maalum.

Sasa mimi sifanyi kazi ya kamisheni bila ya wao kufanya, mimi ninachotakiwa nijibu baada ya kamisheni kulifanyia kazi lile jambo ambalo limelalamikiwa. Kwa hivyo kadhia hii kamisheni wameipokea na tayari wameshawasiliana na Idara Maalum waweze kumsikiliza huyu kijana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii ni Tume ya Utumishi Serikalini wala sio tume ya Idara Maalum. Tume ya Utumishi Serikalini haiwezi kumsikiliza mtumishi wa Idara Maalum. Ndio pale tunaposema kuna mgawanyo wa majukumu. Kuna Tume ya Utumishi ya Mahakama, Tume ya Utumishi ya Baraza, Tume ya Utumishi Serikalini na Tume ya Utumishi Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, ni Baraza hili hili wametwambia tume hizi zisiingiliwe na tume na mamlaka ya ajira nyengine. Sasa hii ni Tume ya Utumishi Serikalini itawezaje kuzungumzia suala la mtumishi wa Idara Maalum.

Isipokuwa Idara Maalum ambayo bajeti yake imeshapita italifanyia kazi hili. Kama Idara Maalum wakiona huyu mtumishi, maana sasa inabidi nisikukubalie kuniletea watu tu bila ya kufuata utaratibu. Lazima taratibu zipo kwa mujibu wa sheria zifuatwe.

Maana pengine imekuwa huu wema wangu sasa inakuwa unanichongea. Kwa hivyo mtumishi afuate utaratibu aende Idara Maalum, akiona hakuridhika afuate utaratibu wa kwenda Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba ninadhani Waziri anayehusika yupo na anasikia. Ningelikushauri ukenda kwa Waziri akalifanyia kazi suala hili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sasa Mhe. Mwenyekiti, hujanisikiliza ridhaa yangu pengine kama ningelisema tuendelee jee. Naona unaanza kuhukumu wewe.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilikuwa nimetoa maelezo ya ziada tu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaheshimu kiti chako kwa kuwa umeshakata ushauri huo tena mimi niseme nini, tuendeleeni.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua muda Mhe. Waziri aliopata ni mdogo na masuala yetu yalikuwa mengi, lakini nilikuwa ninataka nimkumbushe tu kwamba katika michango yangu nilipendekeza, tulipokuwa tukipata mafunzo tuliambiwa fedha za kodi za wananchi tuangalie vile vipaumbele.

Kwa hivyo tulishauri katika vipaumbele vya mwaka ujao, tujaribu kuangalia stahiki za madiwani. Kwa sababu madiwani na wao wanafanya kazi ya siasa kama sisi. Na kwa kuwa Mhe. Waziri yeye ndiye anayesimamia suala la utawala bora, utawala bora haiwezekani wanasiasa wengine wakawa wanalipwa mishahara, wanasiasa wengine wakawa wanaishi kwa posho.

Sasa hili ninamuomba kwa kuwa mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti na tushapendekeza kuwa bajeti ya mwakani mwezi wa Februari tuletewe ile rasimu ya mapendekezo ya vipaumbele, basi tuje tuone mapendekezo ya mishahara ya madiwani.

Hivyo ninadhani watakaa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala wa Umma na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tuangalie madiwani wetu, safari hii sisi tutakuwa hatuna maana ikiwa hatukuweza kuangalia stahiki zao Waheshimiwa Madiwani.

Hili Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wala sitaki anijibu, hili nilikuwa ninamkumbusha tu, na kwa kuwa wewe Mheshimiwa umeshawalea madiwani, Mhe. Waziri Afisi ya Rais ameshawalea madiwani. Sasa tunataka alau safari hii na wao wakiondoka waondoke na mkoba. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0801 Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri umejitahidi kuonesha nia nzuri lakini bado suala la walimu ni kitendawili ambacho hakijateguka kwa walimu wa sayansi na hesabati.

Umekaa na kujisifu kuwa walimu watafurahi lakini maslahi yao ni madogo. Baada ya hayo walimu 240 una lengo gani kuongeza kwa haraka haraka tena.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ya walimu na mishahara ilizungumzwa sijui ulikuwa hupo au wapi. Hoja ilizungumzwa kwa urefu na ufasaha sana. Sasa kama hukuridhika utaratibu unakaa ninazungumza mimi, halafu ninakupa ruhusa.

Sasa kama hukuridhika tunamwambia Mhe. Waziri atoe maelezo ya ziada. Kwa hivyo hukuridhika na maelezo ya mwanzo yaliyotolewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sijaridhika kabisa Mhe. Mwenyekiti, ndio nikainuka.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, rafiki yangu Mhe. Jaku lazima akiri kwamba wakati ninatoa hoja hii anasali hakuwepo. Sasa ataridhika vipi wakati hakusikia.

Kwa hivyo mimi sina maelezo ya ziada kama anataka maelezo ya ziada aende kwenye *hansard*. Maana yake itakuwa hivi sasa ni mchezo wa kitoto hatufuati utaratibu Mhe. Mwenyekiti. Sasa tunaoneshana nini.

Mhe. Mwenyekiti, unajua *sometime*s lazima Baraza lako lifuate utaratibu. Mhe. Spika, juzi alisema hapa na wewe Mhe. Mwenyekiti, umesisitiza. Sasa mimi sina maelezo ya ziada zaidi ya yale ambayo nimeyatoa kwenye maelezo yangu wakati ninajibu hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwepo alipokuwa anajibu lakini ninachosema mimi Mhe. Mwenyekiti, hao walimu 240 ninamsikia anavyosema yupo tayari na sisi tutafute wengine, lakini ninachosema maslahi yao Mhe. Mwenyekiti, bado ni madogo hayakidhi na wengine pesa wanakatwa, wanataka nauli wanapokwenda kwa sababu wanatumia baiskeli.

Anifahamu Mhe. Waziri mimi nilikuwepo alipokuwa anajibu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tusiendelee mpaka anijibu wengine ataajiri lini, watu wanaumia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuheshimu kiti chako. Mimi nilisema kwamba hata tofauti ya walimu wa *art* na sayansi imezingatiwa katika kipindi kilichopita.

Mshahara kwa mtumishi yeyote yule sidhani kama yupo kama anayesema huu unanitosha. Hata sisi na Tanzania Bara, maana vimetolewa vigezo hapa, vigezo tulivyochukua sisi tumekwenda kuchukua huko Bara ili tusitofautiane sana.

Hata sisi Wawakilishi hazitutoshi, mawaziri hazitutoshi, wafanyakazi wengine haziwatoshi, hakuna kinachotosha, tunafanya kwa mujibu wa uwezo wa serikali uliopo. Sasa Mhe. Mwakilishi mpaka anakuwa Mwakilishi hata hilo halielewi?

Unashona nguo kwa mujibu wa kitambaa ulichonacho. Tutaendelea kuzingatia maslahi ya watumishi kadri uwezo utakavyopatikana, na ndio maana safari hii tumeacha kupandisha mishahara kwa kima cha chini, tunatekeleza yale ambayo kwa muda mrefu hatujayatekeleza kutokana na uwezo tulionao.

Sasa mimi ninadhani Mhe. Jaku kama pale mwanzo hajaridhika na sasa aridhike kwa haya niliyomwambia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hapa hatukuja kufanya jazba, tumekuja kuelimishana, mimi ni mgeni lakini bado kilio cha walimu kimekuwa kizito hata kimepelekea mpaka kununua mitihani na mitihani yenyewe sio, hilo sio lengo lao, hiyo ni shida hawezi kupata masomo ya sayansi atueleze. Ni kitu rahisi ni kutueleza. Ni Kiswahili ninachokizungumza, mimi sijazungumza kihindi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninadhani Mhe. Waziri kaeleza kifasaha kwamba serikali itakapopata uwezo itarekebisha, na hali haijaridhisha kwa walimu tu lakini sehemu bado hazijatosheleza. Kwa hivyo serikali ikipata uwezo na maslahi yataongezeka.

Ninadhani Mhe. Waziri kasema kwa ufasaha kabisa. Yeye anapewa mafungu na serikali, na serikali uwezo wake ni mdogo. Kwa hivyo tuvumiliane, uchumi ukikua, tukichimba mafuta zogo hili litaondoka.

Kwa hivyo nadhani Mhe. Jaku umenielewa na mimi, nimesaidia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, umeingia wewe mtu mzima itabidi mimi nianguke tu.

Kifungu 0801 Tume ya Utumishi Serikalini 253, 218,000/=
Kifungu 0901

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika hoja mbali mbali ambazo nimezitoa, ninarejea tena kwamba nyingi kwamba Waziri alitusaidia majibu fasaha na ya kina katika vile vifungu vya matumizi. Kuna kifungu kimoja tu katika Idara hii labda binadamu inawezekana alighafilika au alikiruka. Naomba anisaidie.

Kuna fungu nimelitaja hapa la mkutano, nakumbuka alitoa maelezo ya kina kabisa lakini kuna fungu moja dogo tu kwenye ukurasa wa 17 vote 22050, hili linahusu vifaa vidogo vidogo, *sundry items* na niliiuliza kwamba mwaka jana ilikuwa milioni 6,750,000, lakini mwaka huu imekuwa 19,200,000. Lakini nikasema zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika buku kabla haijafanyiwa marekebisho ilikuwa kwenye milioni 8. Sasa imepanda ghafla imeongezewa katika marekebisho kufikia fungu hili la milioni 19.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa tafsiri ya *sundry items* tunayoijua sisi haiingii akilini, lakini labda kwa sababu ya maelezo yake kuwa katika huo *MTEF* kuna maelezo ya ziada, hebu atusaidie kwenye fungu la *sundry items* kunakuwa na vitu gani ambavyo vinafikisha bajeti kwa mwaka kwa jana moja kufika milioni 19, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Jussa. Lakini kama nilivyosema katika maelezo yangu ya jumla ni kwamba ukienda kwenye ile *MTEF*, lakini sasa hivi siioni hapa, nafikiri itakuwa nimeiacha ndani ya gari. Akubali tu Mhe. Mjumbe kwamba huu ndio uhalisia wa mambo na akubali ombi langu lile la mwanzo, nilolitoa niko kwenye *podium* pale, kwamba vifungu hivi, ukiviangalia kwa undani na tafsiri yake lazima Waheshimiwa waweze kuhoji na ni haki yao kuhoji. Lakini anikubalie kwamba hiyo orodha na *item* moja moja katika eneo hili nimpe baadae na nafikiri ataridhika. Kwa sababu yeye ni Mjumbe wa kamati ya katiba na sheria ambayo inafuatilia utendaji na ufuatiliaji wa matumizi ya wizara yangu, nafikiri atahakikisha na kuweza kufahamu kile ambacho kimekusudiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kwa sababu amesema kwamba nikiwa Mjumbe wa kamati nina nafasi ya kuliulizia na atatupa maelezo huko, basi nashukuru naomba tuendelee.

Kifungu 0901 Idara ya Utawala na Rasilimali watu Shs.893,908,000/=

Kifungu 1010

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilisema hiki kitengo ni kidogo, pesa hazikidhi hata kwa kununua gari, kama hatujawa tayari hiki kitengo bora tukiondoshe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, unajua yeye anasema ninazungumza kwa jazba, lakini inaonekana yeye ndiye anayezungumza kwa jazba. Nilisema sisi tumeomba milioni 650, lakini tukapewa hizi ziliopo. Sisi tungependa tupewe hizo tulizoomba, lakini hatukupewa tumepewa hizi. Sasa ulikuwa unataka 10, umepata 5, utasema 5 huitaki. Kwa hesabu ya haraka haraka, yeye ni mfanyabiashara na anaelewa taratibu za biashara. Lakini hapa hatuko kwenye biashara, tumekwenda kuomba bajeti wizara ya fedha na maombi ya milioni 600 kwa ajili ya *other charges* kwa kuanzia taasisi mpya. Tumepewa tulichopewa, sasa ndio tulichopewa na nimesema kwamba watumishi wa ofisi hii watatoka katika sekta ya umma, tutawapata ndani ambao tayari wana kasma zao za mishahara.

Kwa hivyo, hiki tulichonacho tutajitahidi kukitumia katika ofisi hii. Lakini hata hivyo, katika miradi minne tuliyoiomba kwenye *budget speech* yangu ni pamoja na mradi wa kitengo cha *anti corruption*, nimeeleza katika hotuba yangu humu. Kwa hivyo, mimi nadhani sisi hatuwezi kuwa chagizo kwa serikali kwamba madhali hamkutupa hiki, tufutuke tuseme basi na idara hatutaki tuiunde. Idara ina umuhimu wa kuwepo na michango ya Wajumbe wa Baraza hili inaonesha kwamba hii idara ni muhimu. Najua natetea ili nipate pesa nyingi zaidi, lakini ndio hali halisi. Kwa hivyo, Mhe. Jaku aelewe hiyo ndio hali halisi, tulikwenda na maombi ya milioni 650, lakini tumepata tulichokipata. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sikubali hata siku moja, hapa hapana *serious* kwa hili, hapa tutaelezana mpaka tufahamishane. Kwa shilingi 220 milioni atafanya kitu gani katika kitengo kama hiki. Leo mtu yuko shamba anatakiwa kuja kuripoti mjini, kwa shilingi 10,000/- atafikaje hapa huku. Hapa pazito Mhe. Mwenyekiti, kama hatukuwa tayari hiki kifungu kiondoshwe kabisa, lakini hapa hatuko *serious* kabisa kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe serikali inakwenda kwa *ceiling*, na *ceiling* iliyopelekwa wamepata hicho, kwa hivyo wataanzia hicho halafu wataendelea, baadae zikipatikana watamaliza mradi wao. Huo ndio utaratibu wa wizara zote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakuheshimu sana, lakini kwa hili bado mimi ni mzito.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hajui hata hiyo taasisi inafanya kazi gani, hajui hiyo taasisi kazi zake ni nini, na hajui hata serikali inaendeshwa vipi. Mimi naomba radhi sana Mhe. Mwenyekiti. Hoja yangu ni kwamba tuliomba milioni 650, tumepewa tulichopewa na

tunakaribisha wahisani. Kama yeye anaweza kuchangia namkaribisha aniletee, lakini uwezo wa serikali ni huu na haja ya kuwepo kitengo hiki na taasisi hii ipo. Sasa kama yeye anasema kwamba sio muhimu bora tuache kisianzishwe. Mimi nadhani sio mantiki hiyo, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kama kuna kiongozi wa serikali anaweza kutusaidia tunaomba msaada ili tuweze kuendelea mbele zaidi. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nafahamu *concern* ya Mhe. Jaku na Waheshimiwa Wajumbe wengine. Lakini mimi ni mmoja katika niliopata bahati nyengine ya kupewa heshima ya kuanzisha moja katika taasisi muhimu katika nchi yetu Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzisha taasisi ambayo haipo ni kazi kubwa sana, lakini kazi yenyewe unapoanza ni tofauti kidogo na pengine umeagiza kontena linakuja lote, hii unaanza kidogo kidogo. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mhe. Mjumbe nadhani akirudi nyuma anaweza kuona kwenye kumbukumbu, ilianza na bajeti ya milioni 100 wakati ule ilipoanza. Lakini sasa hivi Mjumbe akiangalia bajeti yake, nadhani inakaribia milioni 900, lakini ipo imesimama na inafanya kazi zake, ina wataalamu na ina miundombinu. Kwa hivyo, naomba na mimi nimtoe wasiwasi kwamba ni kweli pesa hazitoshi, lakini unapoanzisha taasisi kama hii unaanza kidogo utakachoweza kuanzisha. Kwa kawaida taasisi hizi unapata na kusaidiwa vile vile.

Kwa hivyo, ni kweli hii taasisi ina shughuli muhimu lakini inafanya hatua kwa hatua, haitofika kesho ikaanza kazi zote ambazo zinatarajiwa izifanye. Kwa hivyo, mimi nadhani kwa mustakabali huo na uzoefu huo tumeuona, tukubaliane kwamba hiki kitatumika kuanza na baadae kama tunavyokwenda tutaona maendeleo yake. Wasi wasi wake ni wa msingi, lakini naomba Mhe. Jaku afahamu kwamba hivyo ndivyo tunavyokwenda kutokana na uwezo wenyewe ulivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na hilo, lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwanza anitake radhi. Taasisi naifahamu, mimi ni Mwakilishi, naujua umuhimu wake na ndio maana nikakitetea hiki kitengo kuwa hizi pesa ni kidogo. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1001	Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa	Shs. 221,251,000
	Jumla ya Fungu	Shs.3,495,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 47 – KAMISHENI YA UTUMISHI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	Shs.856,484,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 44 – OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	Shs. 1,408,506,000
	Jumla ya Fungu	Shs. 1,408,506,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa kamati ya matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale waliokubali hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, wanyooshe mikono. Waliokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru kwa michango na hoja pamoja na kumshukuru Mhe. Waziri. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitisha hotuba hii, ili kuweza kumpa nafasi Mhe. Waziri kwenda kufanya kazi katika wizara yake. Nawashukuru sana.

Baada ya hayo naakhirisha kikao chetu mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 06/07/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 2:48 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 06/07/2012 saa 3:00 za asubuhi)